# Nipashe

Jumatano Januari 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581180

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS. 1,063,605,974

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Magari** ya IT yanaswa makosa ya ulevi, kughushi

UKURASA 4




UKURASA 13

# NURU MPYA YAANGAZA

• Mikutano ya kisiasa sasa ruksa, mchakato Katiba Mpya waja, Mbowe, maaskofu wanena ... *Endelea Ukurasa 2 & 3*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa kuhusu maamuzi ya serikali kuruhusu mikutano ya kisiasa katika kikao kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Serikali yatoa ufafanuzi wengi kukosa nafasi shule za bweni

UKURASA 8

## Samia: Ilikuwa vuta nikuvute kufikia maridhiano ya kisiasa

UKURASA 2


MICHEZO MARIOO AMKOSOA DIAMOND UK.27

MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na viongozi; Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango (wa tatu kushoto), Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (wa pili kulia), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), George Simbachawene (kulia), Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Mohammed Ally Ahmed na viongozi wa vyama vya siasa baada ya kikao Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Nuru mikutano kisiasa yaangaza

**Na Gwamaka Alipipi**

HATIMAYE serikali imeviruhusu vyama vya siasa nchini kufanya mikutano ya hadhara kuanzia sasa baada ya kuwapo kwa zuio la muda mrefu.

Marufuku ya kufanyika kwa mikutano ya vyama vya siasa ilitolewa mwaka 2016 muda mfupi baada ya kuingia kwa uongozi wa serikali ya awamu ya tano, huku ikisisitizwa kuwa kinachotakiwa kufanyika baada ya kumalizika uchaguzi mkuu ni kazi na mambo ya siasa yasubiri uchaguzi mwingine.

Mbali na kutokuwapo kwa mikutano ya vyama vya siasa jambo lililoonekana kuwa ni kuminywa kwa demokrasia na uhuru wa kukusanyika, jambo lingine lililolalamikiwa wakati huo ni kuminywa kwa uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza.

Hata hivyo, baada ya kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mwanga wa kuwapo kwa demokrasia ulianza kuonekana kutokana na ahadi iliyotolewa ya kuwapo kwa maridhiano ya kisiasa.

Rais Samia alitangaza kuondolewa kwa zuio hilo jana, Ikulu jijini Dar es Salaam, alipokutana na viongozi wa vyama vya siasa, hali iliyoibua shangwe kwa viongozi wa vyama waliohudhuria mkutano huo.

Akihutubia mkutano huo uliovishirikisha vyama vya siasa 19 vilivyo hai, Rais Samia alisema: "Uwapo wangu leo (jana) hapa nimekuja kufanya ruhusa ya mikutano hii. Nimekuja kutangaza kuondoa zuio la mikutano ya hadhara na ninasema kwamba sasa linaondoka."

Rais Samia alisema mikutano hiyo kisheria ni haki kwa vyama vya siasa kuiendesha, huku akisema serikali imejipanga kutekeleza wajibu wake wa kulinda mikutano hiyo.

Alisema jukumu sasa linabaki kwa vyama vya siasa kutoa taarifa kwa vyombo vya dola kama sheria na kanuni zinavyoelekeza ili vipatiwe ulinzi na kwamba hatua waliyoifikia katika mazungumzo baina ya vyama na serikali kwa sasa, mikutano hiyo haitazuiwa tena.

"Ruhusa ya mikutano ya kisiasa itatolewa. Wajibu wetu sisi serikali ni kuwalinda mfanye mikutano yenu salama, mmalize vizuri. Kufuata kanuni ndiyo wajibu wenu vyama vya siasa," alisema.

**ATOA ANGALIZO**

Hata hivyo Rais Samia alitoa angalizo kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya kistaarabu, kutotumia lugha za matusi pamoja na kufuata mila na desturi za Watanzania.

"Tunatoa ruhusa lakini tukafanye siasa za kistaarabu, za kupevuka, mikutano ya kujenga na si ya kubomoa. CCM (Chama Cha Mapinduzi) tunaamini kwenye kujenga, kukosoa, tukakosoane kwa staha," alisema na kuongeza:

"Unaweza kunitukana mimi (Samia) nikawa na moyo wa kustahimili. Lakini je, chawa wangu akisia natukanwa atakubali? Hawezi kukubali lazima atajibu mapigo na mwisho wa siku mnaingia kwenye mtafaruku. Kutukanana siyo mila zetu" alisema.

"Kama tunakosea haki za binadamu tuelezeni, lakini kama tukienda kutukanana nchi haitakalika. Isemeni serikali, ikosoeni, onyesheni mapungufu ya serikali, pale ilipofanya vizuri nendeni mkasifie. Uongo haujengi, ukweli unajenga," alisisitiza.

Rais Samia alisema atazungumza na vyombo vya dola ili kuhakikisha suala hilo linatekelezwa kwa ufanisi.

"Ni haki kwa vyama vya siasa kuendesha mikutano ya hadhara lakini ndugu zangu tuna wajibu. Kwa upande wa serikali, tumeshajipa wajibu wetu kuwa ni kulinda mikutano ya vyama vya siasa. Wajibu wenu vyama vya siasa ni kutupa taarifa kama sheria na kanuni zinavyosema kisha vyombo vinatoa ruhusa.

"Wakiona kuna hatari hawatoi ruhusa. Kwa hatua tuliyofika ruhusa za kufanya mikutano zitatolewa kwa sababu wajibu wetu ni kuwalinda mfanye mikutano kwa usalama, mmalize vizuri muondoke vizuri," alisema.

Hata hivyo, Rais Samia alisema mazungumzo baina ya serikali na vyama vya siasa bado yanaendelea na kwamba kuna mambo mengi ambayo wanapaswa kukutana, kuzungumza, kushauriwa, kukubali, kukataa kwa hoja.

**WAPINZANI WAPONGEZA**

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alisema wamepokea habari hizo kwa mtazao chanya.

Alisema CHADEMA kinaimani kwamba watakwenda kukaa kikao na kujadili maamuzi hayo.

"Tumepokea kwa mtazamo chanya, ukandamizaji uliokuwapo awali haupo tena, ilikuwa ni haki ya kikatiba kufanya mikutano. Ni matumaini yetu kwenye suala la Katiba mpya mengi yanakwenda kubadilika," alisema Mbowe.

Alisema awali kuna sheria zilikuwa zilikipishwa bila ya ushirikishwaji ikiwamo Sheria ya Takwimu, Sheria ya Taasisi zisizo za Serikali, Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Tume ya Uchaguzi.

Alisema kwenye utungaji au urekebishaji wa sheria ni lazima ushirikishwaji ufanyike, lakini miaka ya nyuma kulikuwa hakuna ushirikishwaji.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema Rais Samia amefanya uamuzi wa busara kuruhusu mikutano ya vyama vya siasa kwa sababu ilikuwa ni kiu ya muda mrefu.

Alisema hatua hiyo pia itaimarisha demokrasia nchini, kwa sababu lilikuwa ni jambo la kikatiba lakini lilikuwa halitekelezwi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF). Prof. Ibarahim Lipumba, alisema vyama vya siasa havitakiwi kuomba kufanya mikutano ya siasa kwa vyombo vya ulinzi na usalama bali vinatakiwa kutoa taarifa.

Alisema kufanya mikutano ya kisiasa ilikuwa ni takwa la Kikatiba, hivyo alimshukuru Rais Samia kutengeua zuia hilo.

**CHAUMA**

Mwenyekiti wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA), Hashimu Lungwe, alisema ni faraja kubwa na wanampongeza Rais Samia.

"Hii siku tulikuwa tunaingojea kwa muda mrefu. Kwa sasa tunaondoka kwenye zama za kutishana, wala polisi siyo wa upande mmoja watatulinda wote," alisema Lungwe.

# Samia asema ilikuwa vuta nikuvute maridhiano kisiasa

**Na Gwamaka Alipipi**

ILIKUWA vuta nikuvute wakati wa mazungumzo ya kutafuta maridhiano kati ya serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Rais Samia Suluhu Hassan alisema jana jijini Dar es Salaam.

Alisema hayo wakati wa mikutano na viongozi wa vyama vya siasa aliouitisha kutoa ufafanuzi na kutangaza masuala mbalimbali yaliyofikiwa katika mchakato mzima wa utangamano wa kisiasa nchini.

Samia alisema kwenye mazungumzo hayo, ilimpa wakati mgumu Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana dhidi ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

Rais Samia alisema wakati anaingia madarakani, busara ilimtuma ya kuhakikisha taifa linakuwa pamoja na kuzungumza lugha moja.

Alisema ili kutekeleza hilo, alisema alilazimika kuhakikisha kunakuwapo na maridhiano kwa kufanya mazungumzo na vyama vya siasa hali iliyosababisha kuunda kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia.

"Kuna chama kilisema sisi hatushiriki katika hayo mazungumzo, tunataka tuzungumze peke yetu na Rais. Watu wakasema mengi, wengine walisema usiwasikilize hao (CHADEMA). Nikasema hapana lazima niwasikilize.

"Niliwaita kuwasikiliza. Ilikuwa vuta ni kuvute kwenye hayo mazungumzo. Kinana alikuwa anarudi kwangu anasema 'Mwenyekiti mambo huko ni magumu,'" alibainisha lakini akasema mazungumzo hayo yalikwenda vizuri na leo wawili hao wanakaa pamoja.

"Kwenye mazungumzo hapakosi amani, mazungumzo, maridhiano bado yanaendelea, sisemi yameisha. Baada ya maridhiano sote tutoke kwenye jukwaa moja tukae kama Watanzania, kama taifa na tuijenge nchi yetu. Ni imani yangu tutaendelea kukaa na kuijenga nchi pamoja," alisema.

Rais Samia alisema alipoingia madarakani aliamua kufanya mabadiliko kwa kuzingatia miiko, mila, desturi za Watanzania, Katiba, sheria, baada ya hapo kuijenga nchi kiuchumi.

"Huku ndiko Mungu aliniambia nielekee. Mambo hayo yote nimepata baraka za chama changu. Nataka kuiona Tanzania iliyowahi kuwika huku nyuma, Tanzania ambayo ikiwika kuna nchi inataka kupewa haki yake," alisema.

Alisema serikali inapaswa kutenda haki kwa kuendana na mila na desturi ya Tanzania, lengo ni kujenga umoja na mshikamano.

Rais alisema serikali inawajibu wa kufanya kazi yake, hivyo hivyo kwa vyama vya siasa na vyombo vya ulinzi na usalama.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari kuhusu sekta ya ardhi na mwelekeo wa utekelezaji wa wizara hiyo kwa kipindi cha kuanzia mwezi huu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Mchakato wa Katiba wanukia

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imedhamiria kukwamua mchakato wa marekebisho ya Katiba kwa namna itakavyokubaliana na vyama vya siasa.

Rais Samia Suluhu Hassan aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano na viongozi wa vyama vya siasa 19 vilivyosajiliwa na kuwa hai. Alisema muda wowote kuanzia sasa itaundwa kamati itakayoishauri serikali namna ya kuuendeleza mchakato wa Katiba na kwamba serikali iko tayari kuukwamua.

Alisema kamati hiyo itajumuisha makundi mbalimbali kama vile vyama vya siasa, vyama vya kijamii, Watanzania, na vyombo vya ulinzi na usalama.

Rais Samia alisema moja ya mapendekezo ya kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi alichounda mojawapo ya maoni waliyopendekeza ni kuendelea kwa mchakato wa Katiba mpya.

Alisema kikosi kazi hicho kiliwasilisha mapendekezo makubwa matatu ambayo ni kuruhusu mikutano ya vyama vya siasa, marekebisho ya sheria mbalimbali na marekebisho ya Katiba.

"Kuna hoja ya kuangalia hali halisi ya siasa kwa sasa, yapi yarekebishwe yapi yaendelee kuwapo. Ni muda mrefu mchakato ulifanyika. Je, kilichopendekezwa wakati ule kinahitajika kwa sasa? Wengine wanataka Katiba mpya wengine wanataka marekebisho. Sasa hiyo kamati itakwenda kutushauri namna ya kuuendeleza," alisema.

Rais Samia alisema itakuwa kamati inayofanya kazi kwa maelekezo ya serikali, kwamba katika kuendeleza mchakato huo hakutakuwapo na vurugu vurugu. Alisema wako wanaotaka marekebisho ya Katiba na wengine wanataka mchakato wa Katiba mpya na kwamba muda wowote kuanzia sasa itaundwa kamati ambayo itashauri namna ya kuendesha mchakato huo.

"Kamati itakuwa inaendelea na kazi huku nchi inaendelea na shughuli za maendeleo. Tukisema kila kitu kisimame ili mchakato wa Katiba mpya uendelee Watanzania watatudai huduma za maendeleo, Watanzania hawatakula Katiba wanataka hospitali, wanataka shule, wanataka maji," alisema Rais Samia.

Alisema nia yake ni kuhakikisha taifa linakuwa na amani na utulivu na kwamba hilo ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha nchi inakuwa na amani.

Kuhusu marekebisho ya sheria mbalimbali, Rais Samia alisema serikali inaendelea kufanyia kazi na kwamba mchakato huo utakapokamilika vyama vya siasa vitaitwa katika mazungumzo.

# Viongozi wa dini watoa neno uamuzi wa Samia

**Na Elizabeth Zaya**

VIONGOZI wa dini wamesema uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan umeonyesha mwanga wa kurejea kwa demokrasia nchini na ni heshima kwa nchi.

Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padre Charles Kitima, alisema amefurahishwa na kitendo cha Rais Samia kurejesha na kukuza uwanda wa demokrasia nchini.

"Katika hilo anastahili sifa. Ukiangalia ndani ya miaka mitano iliyopita hali ya demokrasia nchini iliharibika, vyama vya siasa vilikuwa havifanyi kazi yake kama inavyopaswa na kama Katiba inavyosema, hakukuwa na mikutano ya hadhara, kwa hiyo kitendo cha Rais kurejesha imeipa heshima kubwa nchi yetu," alisema Padri Kitima.

"Miaka kama 25 iliyopita kupitia mfumo wa vyama vingi, vyama vya siasa vilikuwa vimezoea kufanya siasa kwa uhuru kwa ushindani, lakini katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, hali ilivurugika, hali ya demokrasia haikuwa nzuri, baadhi ya vyama vya siasa vilipotea kabisa."

"Mfumo wa vyama vingi ndio utaratibu wa Tanzania, ushindani wa kisiasa ndio kitu ambacho Watanzania wanakitaka, lakini kwa kipindi hicho ambacho hali hiyo ilivurugika walikuwa wanasikitishwa sana hasa vyama pinzani kunyanyasika. Kwa hiyo alichofanya Rais, amerejesha kitu ambacho kinaipa heshima nchi yetu.

"Sisi viongozi wa dini tumesimamia hili na tumeliona mara nyingi tangu tulipoanza kuona manyanyaso mwaka 2016/17 yalipoanza makubwa, kuna watu wamepoteza maisha, kwa hiyo hili ni jambo la kumpongeza Rais kwa jitihada kubwa alizofanya ndani ya mwaka mmoja.

Alisema kilichobaki ni kwa viongozi wa vyama vya siasa, kujipanga kufanya shughuli zao kwa kuzingatia utaratibu mzuri.

Kuhusu Katiba, Padri Kitima, alisema ni jambo linalohitaji utashi wa kiongozi binafsi kuzingatia na kutekeleza na kwamba wanategemea watakaosimamia mchakato huo watazingatia maoni ya wananchi wote.

"Kwa sababu hata upungufu uliopo au mazuri yaliyoko kwenye Katiba, unakuta yalikuwa hayaheshimiwi, viongozi kukubali kuongozwa na Katiba ni utashi, utawala wa sheria ndio unaoongoza serikali, kwa hiyo walipaswa kuongoza kwa utashi wa kutawaliwa na Katiba," alisema Padri Kitima. "Unaweza kuwa na Katiba nzuri sana, lakini ikabaki kwenye karatasi, kwa hiyo utashi wa kukubali kuongozwa na Katiba ni jambo jema sana na tuione Katiba kama utashi wa watu na hata vyombo vya dola vione kwamba vinaongoza na kutawaliwa na Katiba ambayo ni utashi wa watu. Na nzuri kuliko yote ni ile inayoheshimu haki na msingi wa binadamu.

Askofu wa Kanisa la Baptisti, Jimbo la Dodoma, Athony Mlyashimba, alisema ni jambo la kumpongeza Rais kurejesha mchakato wa Katiba na kuomba uanzie kwenye rasimu ya Warioba.

"Huwezi kujenga nyumba ambayo ina msingi mbaya halafu ukainua boma vizuri na ukapaka rangi nzuri usitegemee kwamba itadumu, ni lazima ipo siku itadondoka yote. Katiba ndio kitu ambacho kimebeba taifa."

"Mimi nashukuru Rais kuliona hili na kuingia kwenye mchakato wa kuhuisha, lakini ushauri wangu ni kwamba hakuna haja ya kuendelea kutumia gharama kubwa kwa sababu ipo rasimu ya Jaji Warioba ambayo ilibeba maoni yote mazuri waliyotoa wananchi.

"Ile ni rasimu ambayo ilibeba fedha za wananchi, makundi yote yalichangia maoni yao katika ile rasimu ya Warioba, kwa hiyo hakuna haja ya kuanza kutafuta maoni ya wananchi kwa mara nyingine, kama wanataka kuanza, mchakato uanzie tulipoishia kwa Warioba.

"Na kama kutakuwa na kamati itakayoteuliwa, ndio ianzie pale kwenye rasimu ya Warioba kuangalia kila kipengele, lakini ninaamini kwamba kwa namna ilivyosukwa ile rasimu, kazi iliyokuwa imebaki ni kuitisha tu mkutano wa kura za maoni kwamba wananchi wanaikubali au laa, tuichukue ile tuipeleke kwenye kura za maoni badala ya kurudi kuanza mchakato mwingine mrefu.

"Labda endapo watu wataikataa, ndio turudi tena kwenye mchakato, lakini ninavyoamini kwa sababu ilibeba mawazo ya wananchi wote hawawezi kuikataa na hata kama wapo ni wachache sana.

"Tunashukuru kwa utayari wa Rais kwa sababu alichokifanya ndicho kitu tulikuwa tunakihitaji, ule moshi umeanza kutoka sasa."



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation "ZMBF" (wa pili kushoto), akimkabidhi boti, mashine, kamba pamoja na vifaa mbalimbali katibu wa kikundi cha IPO Sababu, Tumbe Kaije Said Bakari na Bikombo Rashid Ali (kulia) katika hafla ya ugawaji wa vifaa vya kilimo cha mwani kwa vikundi vya Wilaya ya Michweni Mkoa wa Kaskazini Pemba jana. **PICHA: IKULU**

# Polisi, TRA wanasa magari 31 ya IT madereva wakikutwa na vilevi

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

JESHI la Polisi Iringa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Iringa, limekamata magari 31 ambayo yanapita nchini kwenda kusini mwa Afrika maarafu kama (IT) yanayotoka katika Bandari ya Dar es Salaam kwenda Malawi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Allan Bukumbi, hivi karibuni alisema kuwa magari hayo yamekamatwa kwa makosa mbalimbali yakiwamo ulevi wa madereva na kutokuwa na vibali.

Kamanda Bukumbi pia alisema magari hayo yamekamatwa kwa kuwa na kasoro mbalimbali ambazo husababisha kukithiri kwa ajali za barabarani.

Alisema baadhi ya madereva wamekutwa na nyaraka za kughushi kitendo kinachosababisha kuongezeka kwa ajali zinazohusisha magari hayo kutokana na kuendeshwa na madereva wasio na sifa na kukosa uzoefu wa kuendesha umbali mrefu.

ACP Bukumbi alisema kwamba wamefanya msako huo ambao ni endelevu kwa kushirikiana na TRA na LATRA ili kukomesha ajali zinazohusishwa na magari hayo kwa kubeba abiria kinyume cha sheria.

Meneja wa TRA Mkoa wa Iringa, Paul Walalaze, alikemea vikali kitendo cha mawakala kutumia madereva ambao hawana uzoefu lakini pia kughushi nyaraka na kuwataka kuacha mara moja.

"Sisi TRA tunashirikiana na Jeshi la Polisi ili kuhakikisha hakuna mizigo (damping) inayoshushwa nchini bila kulipa na haijathibitishwa na mamlaka ya kudhibiti ubora (TBS), ili kulinda soko la bidhaa za ndani kutokana na kuwapo kwa bidhaa ambazo hazijalipa kodi," alisema.

Walalaze alisema magari mengi ambayo yalikamatwa na polisi yana makosa ya kiforodha ambayo yanaepukika na mawakala kupitia kitengo cha 'transit monitoring unit.'

Alisema ikitokea gari hilo limepotea si rahisi kumpata dereva kutokana na magari hayo mengi kuendeshwa na madereva ambao hawana sifa na ikitokea hivyo, mawakala wanalazimika kulipa faini ya dola 50.

# Pele kuzikwa ghorofa ya tisa

**Na Halfani Chusi**

MWILI wa Gwiji wa Soka Duniani, Pele umeagwa jana katika uwanja wa klabu ya Santos wa Vila Belmiro na unatarajiwa kuzikwa katika ghorofa ya tisa ya jengo la mazishi lililoko karibu na uwanja huo.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari nchini Brazil, maziko yatafanyika katika eneo hilo linalomilikiwa na klabu hiyo aliyoitumikia kwa sehemu kubwa ya maisha yake ya soka.

Vyombo hivyo vimeripoti kuwa jeneza la gwiji huyo litapita mitaani hadi mbele ya nyumba "O Rei's" mahali anakoishi mama yake mzazi.

Kwa mujibu wa vyombo hivyo, mama yake Pele amelala kitandani na anaripotiwa kuwa na miaka 100.

Mwili wa Pele utakwenda kupumzishwa, huku vyanzo mbalimbali kutoka nchini Brazil, vikieleza kuwa familia pekee ndiyo itakayoruhusiwa kwenye hatua ya kuupumzisha mwili huo.

Makaburi hayo ambayo gwiji huyo wa soka duniani atakwenda kupumzishwa ni ya ghorofa na yaliingia kwenye rekodi ya kitabu cha Guinness mwaka 1991 kuwa kati ya makaburi marefu zaidi duniani yakiwa na ghorofa 14.

Mwili wa Pele utapumzishwa kwenye ghorofa ya tisa, mwanzoni jengo hilo lilijengwa ili kuwa makazi ya watu kabla ya kubadilishwa na kuwa nyumba ya wafu mwaka 1983.

# LATRA yatangaza nauli mpya mabasi mwendo wa haraka

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), imetangaza nauli mpya za mabasi ya mwendo wa haraka yanayofanya kazi zake jijini Dar es Salaam huku ikijiandaa kupanga nauli za reli ya kisasa (SGR).

Akizungumza jana jijini Dodoma Mkurugenzi wa LATRA, CPA Habibu Suluo, alisema nauli hizo zimepanda kutoka Sh. 750 kwa njia kuu, njia mlisho Sh. 500 huku njia mlisho ikijumlishwa na njia kuu ni Sh. 900.

Mkurugenzi huyo alisema nauli za teksi mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wanne safari isiozidi kilomita moja itakuwa Sh 4,000 kwa kiwango cha chini na juu Sh. 5,000.

Alifafanua kuwa kwa kilomita moja ni Sh 1,000 kiwango cha chini na kiwango cha juu itakuwa Sh. 1,200, wakati kwa dakika itakuwa Sh. 80 kwa kiwango cha chini na juu Sh. 159.

Mkurugenzi alisema kamisheni itakuwa asilimia 10 kwa kiwango cha chini na asilimia 25 kwa kiwango cha juu.

Kwenye pikipiki za mtandao alisema nauli itakuwa Sh. 1,000 kwa kiwango cha chini na Sh. 1,500 cha juu kwa safari isiozidi kilomita moja.

Nauli ya kuanzia safari ni Sh. 250, kiwango cha chini na juu Sh. 350 na nauli ya dakika kiwango cha chini ni Sh. 50 cha juu Sh. 70, huku ada ya kuita usafiri ni asilimia 2.5 na kamisheni asilimia 10 kwa kiwango cha chini na cha juu ni asilimia 25.

TEKSI MTANDAO

Mamlaka hiyo imechukua uamuzi huo ili kurudisha kampuni zingine zilizojitoa kwa madai ya kutopata faida kwenye huduma hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mkurugenzi wa LATRA alisema nauli hizo ni Sh. 3,000 na kiwango cha juu Sh. 4000 na magari yanayochukua abiria sita ni Sh. 4,000 kiwango cha chini na Sh. 5,000 kiwango cha juu.

Kuhusu usafiri wa mabasi alisema mamlaka inakumbusha mabasi yaendayo haraka kuzingatia kanuni zilizopangwa ili kufanya kazi kwa weledi.

Akizungumzia kuhusu nauli za reli ya kisasa, alisema wako katika vikao vya kupanga nauli itakayotumika.

Kuhusu tiketi mtandao kuandika jina abiria aliwasisitiza wananchi kuzingatia hilo ili ajali inapotokea waweze kutambulika kirahisi.

"Naomba jamii izingatie suala la majina kuandikwa kwenye tiketi," alisema Suluo.


**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

**DEED POLL**



The documents presented for registration on the **27-12-2022** at **3:00PM** herewith the original of the above mentioned documents registration having under folio/s **2003** and serial/s **972/2022** knowledge receipt of the enclosures here to.

**URES:**

**SIGNED AND DELIVERED BY SAID JONATHAN MAGAFU BWIRE**
Who is known to me personally
Identified to me by....the letter being known to me personally.
This **27** day of **12 / 2022.**

DEPONENT

**BEFOR ME:**

BEFORE ME
Name
Signature
Postal Address
Date
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

**DEED POLL**



The documents presented for registration on the **27-12-2022** at **3:00PM** herewith the original of the above mentioned documents registration having under folio/s **2000** and serial/s **969/2022** knowledge receipt of the enclosures here to.

**URES:**

**SIGNED AND DELIVERED BY SAID MWINGIRA JIGWIRA MALEKERA**
Who is known to me personally
Identified to me by....the letter being known to me personally.
This **27** day of **12 / 2022.**

DEPONENT

**BEFOR ME:**

BEFORE ME
Name
Signature
Postal Address
Date
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

**DEED POLL**



The documents presented for registration on the **27-12-2022** at **12:41PM** herewith the original of the above mentioned documents registration having under folio/s **1993** and serial/s **963/2022** knowledge receipt of the enclosures here to.

**URES:**

**SIGNED AND DELIVERED BY SAID SARYA MABEMBERE MATARE**
Who is known to me personally
Identified to me by....the letter being known to me personally.
This **27** day of **12 / 2022.**

DEPONENT

**BEFOR ME:**

BEFORE ME
Name
Signature
Postal Address
Date
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

**CHANGE OF NAME DEED POLL**

BY THIS DEEP I SELINA PETRO KOKUBELWA of P.O.Box ARUSHA.
DO HEREBY absolutly renounce and abandon the use of my former names SELINA PETER MISINGO which appear in NMB Card NO. 5161480005859945 in lieu thereof do assume the name, SELINA PETRO KOKUBELWA wich appear in Citizen ID Card NO. 19970402-23125-00002-14 in pursuance of such change of my names as aforesaid.

I HEREBY that I shall at all time hereafter and in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceeding and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of SELINA PETRO KOKUBELWA as my name in lieu of the name of SELINA PETER MSINGO reanounced as aforesaid.

AND, I HEREBY AUTHORISE and REQUEST all persons to designate and address me in the name of SELINA PETRO KOKUBELWA

I, SELINA PETRO KOKUBELWA make this decleration consdentiously beliving the same to be true and in accordande with the provisions of the Oaths (Judicial) and Statutory Decleration Act, No. 59 of 1966.
IN WITNESS WHEREOF I have here unto subscribed the name of SELINA PETRO KUKOBELWA on the day and in the manner herein after appearing.

SIGNED AND DELIVERED BY SAID SELINA PETRO KUKOBELWA
Who is known to me personally
Introduced to me by....the letter being known to me personally.
This **7TH day of 12 / 2021**

DEPONENT



BEFOR ME:

BEFORE ME
NAME
SIGNATURE
POSTAL ADDRESS
QUALIFICATION

HABARI KITAIFA

# Samia aridhia ekari mil. 1.5 kugawiwa wananchi

**Na Munir Shemweta**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan ameridhia ardhi yenye ukubwa wa ekari 1,492,703 iliyokuwa sehemu ya hifadhi na maeneo ya umma, zikiwamo ranchi za serikali kumegwa na kurasimishwa kwa wananchi.

Aidha, mapori tengefu 12 yenye ukubwa ekari 707,962 na hifadhi za misitu saba zenye ekari 46,715 nayo yamefutwa na ardhi hiyo kukabidhiwa kwa wananchi kupitia usimamizi wa serikali za mikoa katika kupanga na kuyapima maeneo hayo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alibainisha hayo wakati akizungumzia masuala mbalimbali ya sekta ya ardhi na mwelekeo wa utekezaji wa wizara hiyo kuanzia januari, mwaka huu.

"Kamati ya mawaziri wa wizara za kisekta imeielekeza mikoa kusimamia utekelezaji wa uamuzi wa serikali kwenye maeneo yao yote yalioainishwa na kutolewa uamuzi," alisema Dk. Mabula.

Miongoni mwa kazi zinazoendelea kutekelezwa sasa, kwa mujibu wa Dk. Mabula, ni uwekaji wa alama za mipaka baina ya maeneo ya hifadhi na maeneo ambayo serikali imeridhia yabaki kwa wananchi, upangaji na upimaji wa maeneo yaliyorejeshwa kwa wananchi, utambuzi, uhakiki na uthamini wa maeneo ambayo wananchi watatakiwa kupisha shughuli au maeneo yatakayotumika kwa matumizi ya umma na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

Kuhusu ulipaji kodi ya pango la ardhi hasa baada ya msamaha wa riba ya malimbikizo ya pango la ardhi uliotolewa na Rais ambao wananchi wenye malimbikizo walipewa nafuu ya kulipa deni la msingi bila riba, Dk. Mabula alisema, wizara imekusanya Sh. 90,907,939,421 sawa na asilimia 75 ya lengo la nusu mwaka.

Hadi kufikia Novemba, 2022 wananchi 2,819 wamenufaika na msamaha wa riba ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi yenye jumla ya Sh. 6,946,930,272. Idadi hiyo haijumuishi wananchi waliojitokeza ambao wamehudumiwa kuanzia tarehe 1 hadi 31. Desemba 2022.

Pia alisema katika mwezi Desemba pekee, wizara imeshuhudia idadi kubwa ya wamiliki waliojitokeza kulipa kodi na Sh. bilioni 22.6 zimekusanywa.

Kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi, Dk. Mabula amezitaka mamlaka za serikali za mitaa kusimamia kikamilifu mipango ya jumla, mipango kina na mipango ya matumizi ya ardhi vijijini kupitia kamati za ardhi za vijiji ili kudhibiti ujenzi holela usiozingatia mipango iliyoandaliwa na kuidhinishwa kupitia Kamati za Mipangomiji.

"Wizara imekuwa ikipokea taarifa na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu ukiukwaji wa taratibu mbalimbali zinazohusu Usimamizi wa Ardhi Mijini na Vijijini. Miongoni mwa malalamiko ni baadhi ya viongozi wa vijiji na mitaa kuuza ardhi kinyume cha utaratibu, kukosekana kwa udhibiti wa uendelezaji ardhi katika maeneo ya vijiji na miji. Hali hiyo imesababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi na uendelezaji ardhi kinyume na mipango iliyoandaliwa na kuidhinishwa," alisema.

Kutokana na malalamiko hayo, Dk. Mabula alisema wizara inaandaa programu maalum ya kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa mamlaka za upangaji na kwamba taarifa hizo zitatolewa kwa umma kama sehemu ya uwajibikaji wa mamlaka kwa wananchi.

## Vituo vya mafuta 195 vimejengwa kinyume cha kanuni

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema vituo vya mafuta 195 kati ya 1,868 vilivyojengwa nchini, vimejengwa kwenye maeneo yaliyo chini ya mita 200 jambo ambalo ni kinyume cha kanuni.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam akitoa tathmini na mwelekeo wa sekta za wizara hiyo kuanzia Januari Mosi, mwaka huu.

Alisema Novemba 10, mwaka jana, alitoa maelekezo ya kusimamisha utoaji wa vibali vya ujenzi na mabadiliko ya matumizi ya ardhi, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafuta kwa kipindi cha miezi mitatu, ili kuwezesha kufanyika tathmini ya uendelezaji wa vituo hivyo nchini.

"Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2022 wizara imepokea taarifa ya uendelezaji wa vituo vya mafuta kutoka halmashauri 129 kati ya 184 zilizopo nchini sawa na asilimia 70.1.

Uchambuzi uliofanywa na Wizara umebaini katika halmashauri 129, kuna vituo 2,063 kati ya hivyo, vya mafuta ni 1269 na vidogo 794.

"Vituo 1,868 vimejengwa katika umbali wa zaidi ya mita 200 kutoka kituo kimoja na kingine sawa na asilimia 90.5 kama inavyoelekezwa na kanuni ya viwango vya umbali; huku vituo 195 vikijengwa umbali wa chini ya mita 200 sawa na asilimia 9.5.

"Wizara inaendelea kufanya uchambuzi, ili kubainisha vituo ambavyo vimejengwa kabla au baada ya kanuni za mwaka 2018 zinazoendelea kutumika ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa," alisema.

Alisema tathmini alibaini pia Jiji la Dar es Salaam, kuna baadhi ya vituo vya mafuta vimeanza kujengwa katika eneo la Hifadhi ya Barabar, na kwamba suala hilo linafanyiwa kazi na mamlaka za serikali na wananchi wote wanaombwa kuwa watulivu.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ruhusa mikutano ya kisiasa idumishe demokrasia, amani

**WINGU** zito lililokuwa limetanda katika medani ya kisiasa nchini sasa limeanza kutoweka. Hii ni baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan jana kutangaza rasmi kwamba mikutano ya kisiasa iliyokuwa imepigwa marufuku tangu mwaka 2016, sasa inaruhusiwa kufanyika.

Mikutano hiyo ilipigwa marufuku sambamba na kuminywa kwa uhuru wa vyombo vya habari huku serikali iliyopita ikiweka bayana kwamba masuala ya siasa baada ya uchaguzi hayana nafasi na kwamba vyama visubiri hadi mwaka 2020 wakati wa uchaguzi mkuu ndipo vifanye siasa. Jambo hilo lililalamikiwa na vyama vya siasa kwamba huo ni ukiukwaji wa katiba na demokrasia kwa ujumla.

Kwa wale waliojaribu kufurukuta na kufanya mikutano ya hadhara kwa kile kilichoelezwa kuwa ni haki yao ya kidemokrasia, walijikuta wakitiwa matatani na hata kufunguliwa kesi za jinai kwamba walikuwa wakihatarisha usalama wa nchi.

Wakati mwingine Jeshi la Polisi lilikuwa likitumika kuzuia kwa madai ya kuwapo kwa taarifa za kiintelejensia za uwezekano wa kutokea uvunjifu wa amani. Jeshi hilo pia likiongozwa na wakuu wa polisi wa wilaya, lilisambaratisha watu waliokuwa wakikusanyika kwa ajili ya mikutano hiyo kwa madai ya kuhatarisha amani.

Baada ya Rais Samia kuingia madarakani, alionyesha mwanga kwamba kuna ulazima wa kuwapo kwa haki, amani na usawa miongoni mwa Watanzania na hatimaye kuunda kikosi kazi ambacho kiliibuka na mapendekezo kadhaa, ikiwamo kurejewa kwa uhuru wa kukusanyika na kujieleza.

Hatimaye siku iliyosubiriwa kwa hamu ilitimia jana baada ya Rais Samia kutangaza Ikulu, Dar es Salaam jana alipokutana na viongozi wa vyama vya siasa kuwa sasa ni ruksa kwa vyama hivyo kujimwayamwaya kwa kufanya mikutano huku vikieleza sera zao na kujijenga kwa ajili ya kuimarisha demokrasia nchini.

Pamoja na ruhusa hiyo, kama alivyosema Rais, Tanzania ni nchi ya amani, umoja na mshikamano, hivyo ni fursa kwa vyama vya siasa kuitisha mikutano na kueleza sera zao badala ya kushambuliana na kutukanana. Kwa kifupi, kinachotakiwa ni vyama vya siasa kufanya siasa za kistaarabu na kiungwana. Rais ameweka hadharani kwamba yeye, serikali yake na chama chake cha CCM wako tayari kukosolewa lakini si kutukanana na kuonyeshana ubaya.

Kwa mantiki hiyo, CCM ikiwa ndicho chama tawala na inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020- 2025, inapaswa kukosolewa juu ya yale yanayofanyika kulingana na ahadi ilizotoa. Pale kwenye upungufu au kasoro ikosolewe pamoja na serikali yake kwa misingi ya kuheshimiana.

Pamoja na hayo, Jeshi la Polisi linapaswa kutekeleza wajibu wake kwa kuhakikisha ulinzi na usalama vinatolewa wakati wa mikutano hiyo pamoja na kutoa vibali kama sheria inavyoagiza badala ya kuzuia na kuwakamata viongozi na wafuasi wa vyama vya siasa kwa visingizio vya hatari ya uvunjifu wa amani.

Katika misingi ya kidemokrasia hususan ndani ya vyama vingi kuna kupingana bila kupigana na kama ni kukosoana, ni lazima pande husika zifanye hivyo kwa hoja badala ya matusi, kejeli na maneno mengine ya kuudhi ambayo yanaweza kusababisha chuki na uhasama. Hivyo, milango imefunguliwa na tunatarajia kuona ile kiu ya wananchi kusikia hoja za kisiasa, inakidhiwa kwa hoja mujarabu na si matusi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# 2023 uwe wa wigo mpana wa uhuru

**WAKATI** mwaka 2023 ukiwa kwenye wiki yake ya kwanza, wadau wa haki za binadamu na wachambuzi wa siasa wanataka kuongezwe usimamizi wa haki za binadamu, demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari.

Wanaona kwamba 2022 unapomalizika ni wakati wa kuganga yajayo na kuyaacha ambayo awali yalijitokeza miaka kadhaa nyuma, ikiwamo kuminya uhuru wa vyombo vya habari, haki ya kujieleza na kutoa maoni na pia kukandamiza uwepo na mchango wa asasi za kiraia kuchangia maendeleo ya siasa, uchumi na jamii.

Hellen-Kijo Bisimba, mwasisi wa taasisi ya LHRC, anasema kuna haja ya kusonga mbele kwa kuhakikisha kwamba uhuru wa vyombo vya habari upo, kwa kuwa ndiyo mlango unaofungulia uhuru mwingine.

Uhuru wa vyombo vya habari ukiminywa, na mwingine wa aina yeyote utabanwa kwa sababu uhuru wake ndiyo unaofanikisha kujua mengine ambayo yalikuwa hayajulikani, ndiyo unaofichua mengi ambayo hayajulikani, unafundisha kwa wale ambao walikuwa hawayajui.

Mwaka huu unatakiwa kuachana na makandokando hasa vyombo vya habari kuminywa na watu wawe huru kujieleza.

Kwa kuangalia maoni yake uhuru wa kupata habari ni msingi wa uhuru mwingine na sasa uhuru wa kidemokrasia unapanuka zaidi kwa vyama vya siasa vya upinzani kupewa haki ya kujumuika ili kutoa fursa kwa vyama hivyo kuwa na uhuru na kujiandaa kwa ajili ya chaguzi zilizo mbele hususan ni wa serikali za mitaa hapo mwakani.

Mwaka huu umeondoa kiwingu wanasiasa wana haki za kujumuika, Rais Samia Suluhu, anapoingia madarakani, anasema ni lazima kuwe na maridhiano ya kisiasa na kujenga Tanzania moja.

Ni jambo la kujivunia baada ya kuwafungulia wanasiasa kifungo cha miaka mingi ambacho kilizorotesha demokrasia.

Mbali na hayo mwaka huu, hautaweza kuliweka pembeni suala la uhuru wa kiuchumi, kuhusu tozo, kufanya biashara na kutengewa maeneo na kuangalia mifumo ya kikodi iliyo rafiki.

Lakini, haya yote yataweza kusonga mbele, iwapo kuna katiba, na katiba mpya ndiyo suala la msingi na muhimu, haliwezi kuwekwa kando kwa kuwa ndio litaweka sawa haya yanayozungumzwa leo 2023 yakianzia 2022.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba (JUKATA), Bob Chacha Wangwe anasema matarajio kwa kipindi cha mwaka huu ni utekelezaji wa yale yaliyowakutanisha viongozi wa kisiasa ikiwamo Rais Samia ambayo leo yameanza kuzaa matunda.

Anakumbusha kuwa mwaka jana kiliundwa kikosi kazi kilicholenga kukusanya maoni ili kuweka mambo sawa.

Oktoba mwaka jana, Rais Samia alipokea Ripoti ya Kikosi Kazi cha Kuratibu Maoni ya Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Ikulu jijini Dar es Salaam.

Miongoni mwa mapendekezo yanayotolewa na kikosi kazi ni kuruhusiwa kufanyika kwa mikutano ya hadhara kwa mujibu wa katiba na sheria pamoja na kuzingatia ambayo yote yameruhusiwa

Rais Samia anasema anaunga mkono pendekezo la kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa kwani kutumia sheria na kanuni za awali zingeendelea kusababisha changamoto na dosari zilizokuwa zikijitokeza mwanzoni.

Pia anavitaka vyama vya siasa kutathmini mienendo ya vyama vyao hasa kuzingatia usawa wa kijinsia, matumizi mazuri ya fedha, utawala bora na kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa kuwawezesha wanawake kugombea nafasi muhimu.

Kikosi kazi hicho kilipendekeza utaratibu mpya wa kupata Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, utendaji wa Tume uruhusiwe kuhojiwa kwenye Mahakama ya Juu na pia isilazimike kufuata amri ya mtu, idara , chama chochote cha siasa au siasa.

Aidha, kinapendekeza matokeo ya uchaguzi wa rais yahojiwe kwenye Mahakama ya Juu mara itakapoanzishwa hayo ni miongoni mwa mambo yanayolalamikiwa na wananchi kwa hiyo 2023 ianze kuyafanyia kazi.

## TCRA: Zaidi ya asilimia 90 laini za simu zimehakikiwa

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema uhakiki wa laini za simu umefikia asilimia 99 huku akiwataka wasiokamilisha kufanya hivyo kabla ya muda wa mwisho uliopangwa wa Januari 31, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, lengo la uhakiki wa laini zinazotumika ni kuwalinda watumiaji huduma za mawasiliano dhidi ya matukio ya utapeli na wizi mtandaoni.

"Kila mmoja wetu akitekeleza kwa ukamilifu zoezi hili tutafanikiwa kuweka anga la Mtandao wa Mawasiliano, hasa mawasiliano ya simu nchini, kuwa salama zaidi kwa kila mmoja wetu," alisisitiza.

Meneja wa Kitengo cha Usimamizi wa Mawasiliano ya simu na intaneti wa TCRA, Sadath Kalolo, akizungumzia maendeleo ya uhakiki huo alisema kati ya laini za simu 60,076,000 zinazotumika ambazo hazijahakikiwa ni 2,062,000 sawa na asilimia 4.3.

Aidha, TCRA imetoa utaratibu wa kuhakiki ni kubofya namba *106# katika simu, ataweza kuhakiki usajili wa namba yake ya simu, pamoja na kutazama idadi ya namba zilizosajiliwa kwa namba yake ya Kitambulisho cha Taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na kufuata maelekezo.

Mamlaka hiyo imebainisha kuwa baadhi ya watumiaji huduma za mtandao wa simu wamekuwa wakikwepa kusajili laini za simu kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kukwepa kubainishwa kwa matendo ya jinai wanayotenda kwenye mtandao na hutumia mbinu ya kununua, laini za simu zilizosajiliwa tayari kwa utambulisho wa watumiaji wengine wa huduma za mawasiliano.

Mapema Novemba mwaka jana, TCRA ilitangaza kuzifungia jumla ya namba tambulishi 52,087, zikiwamo zinazohusishwa na wizi, utapeli na ulaghai kupitia mitandao ya simu.



Mkuu wa Kikosi cha Polisi wa Usalama Barabarani Mkoa wa Manyara, Regina Matagi (kulia), akimkabidhi mkazi wa mjini Babati Emmanuela John (wa pili kulia) Sh. 310,000 na kadi ya bima ya Sh. 200,000 zilizochangwa na askari polisi wanawake kwa ajili ya matibabu juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Maelfu kuuaga mwili wa Papa Benedict XVI

**Na Beatrice Moses**

MAELFU ya waamini wa Kanisa Katoliki wanatarajiwa kuaga mwili wa Papa mstaafu Benedict XVI katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Peter ikiwa ni hatua ya kutoa heshima zao za mwisho kwa kiongozi huyo.

Kwa mujibu wa mtandao wa Vatican News, mwili wa Papa Benedict XVI aliyefariki dunia Desemba 31, 2022 akiwa na umri wa miaka 95 unaagwa na waombolezaji kwa siku tatu.

Mwili huo umewekwa mbele ya kanisa hilo kwenye madhabahu ya kuungama, ukiwa umevishwa mavazi maalum ya kiaskofu pamoja na rozari katika vidole vyake, waombolezaji walipanga foleni kuanzia juzi (Jumatatu) alfajiri kwa ajili ya kuuaga kiongozi huyo.

Benedict anatajwa kuliongoza Kanisa Katoliki kwa takribani miaka minane, kabla ya kutangaza kujiuzulu mwaka 2013 kutokana na hali yake ya afya kudorora na kuweka historia ya kuwa papa wa kwanza kujiuzulu.

Ibada ya maziko ya Benedito XVI inatarajiwa kuongozwa na Papa Francis, itakayofanyika kwenye viwanja vya Mtakatifu Peter kesho, kabla ya mwili wake kuzikwa katika makaburi yaliyoko chini ya kanisa hilo.

# Madereva daladala watishia kugoma kutoa huduma

**Neema Emmanuel na Rose Jacob,**
MWANZA

MADEREVA wa daladala mkoani hapa wametishia kugoma kutoa huduma hiyo kutokana na serikali kuwatoza ushuru kila wanapovuka wilaya moja kwenda nyingine.

Wamesema kama hali itaendelea kuwa kama ilivyo watasitisha huduma hiyo kwa sababu kipato wanachopata ni kidogo ikilinganishwa na ushuru wanaolipa kwa kila siku.

Walitoa mfano wa daladala kutoka Nyashishi wilayani Misungwi kuelekea Kisesa wilayani Magu, zinalazimika kulipa ushuru katika vituo vinne kwa siku.

"Hii ni serikali moja hiyo hiyo, lakini unakuta daladala tunaonewa kwa kutozwa ushuru mkubwa kila tunapovuka wilaya moja kwenda nyingine, mbali na kodi zingine anazolipa mwenye gari," alisema.

Wakizungumza na Nipashe, madereva hao walisema Manispaa ya Ilemela kuanzia jana ilipandisha ushuru huo kutoka Sh. 1,000 hadi Sh. 1,500 kwa gari moja kwa siku.

Mmoja wa madereva waliozungumza na Nipashe, alisema magari yanayofanya safari zake katika wilaya nne wanalazimika kulipa ushuru kila kituo wanapovuka wilaya moja kwenda nyingine.

Alitoa mfano gari ikitoka Nyashishi kwenda Kisesa inalipa ushuru wilayani Misungwi, Nyamagana, Ilemela na Kisesa.

Dereva Allen Ladiansi, alisema Wilaya ya Ilemela ushuru wake kuanzia jana ulipanda na kufikia Sh. 1,500 badala ya Sh. 1,000, Nyamagana Sh. 1,000, Misungwi Sh. 500 na akifika Kisesa ambayo ni Wilaya ya Magu, analipa Sh. 500.

Alisema ushuru huo unalipwa na dereva na mwenye gari hahusiki nao wala hakubali fedha zake kukatwa kwa siku.

Madereva hao walisema kwa kuwa wanatoa huduma katika mkoa mmoja, ushuru huo ungekuwa unalipwa katika kituo kimoja badala ya kulipia kila wanapovuka wilaya moja kwenda nyingine.

Walisema licha ya kulipa ushuru huo, maeneo mengi ya vituo ni machafu na kuona fedha wanazolipa ni kubwa ikilinganishwa na kipato wanachopata kwa siku.

Akizungumzia suala hilo Makamu Mwenyekiti wa chama cha madereva wa daladala mkoani Mwanza, Emmanuel Deus, alisema kupandishwa kwa ushuru katika halmashauri ya Ilemela kutoka Sh. 1,000 hadi Sh. 1,500, walilkataa katika kikao chao na ofisi ya mkurugenzi.

"Katika kikao tulichokaa na ofisi ya Mkurugenzi wa Ilemela ambaye aliwakilishwa na ofisa mipango wa halmashauri hiyo, tulikubaliana mambo yafuatayo yaondolewe bajaji ambazo zimekuwa zikikwamisha biashara ya daladala na kusababisha tukose abiria, lakini tunashangaa hawajatekeleza badala yake wameanza kutoza ushuru wa Sh. 1,500, jambo ambalo sio sahihi," alisema Emmanuel.

Alisema walikubaliana kuitishwa kikao kingine kujadili suala hilo, lakini anashangaa kuona jana wameanza kupandisha ushuru bila kufahamu suala hilo.

Alisema wana wanachama 3,880, wote wanaendesha daladala mkoani Mwanza na yeye gari analoendesha kwa sasa analipa ushuru wa Sh. 5,500 kwa siku.


Alisema akitoka Wilaya ya Misungwi analipa Sh. 2,000, Nyamagana, Sh. 2000 na akifika Ilemela analipa Sh. 1,500 kuanzia jana.

Aliungana na wanachama wake kwamba ushuru huo ni mkubwa hawawezi kuendelea kuulipa kwa kila siku na watafanya kikao na madereva ili kuweka msimamo wa pamoja.

Akizungumzia sakata hilo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, Apolinary Modest alisema, suala la kupandisha ushuru lilitakiwa lianze mwezi Julai 2022, lakini walikaa kikao na viongozi wa daladala wakakubaliana lianze Januari 2023.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



# Serikali yafafanua sababu upangaji shule za bweni

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imesema sababu ya idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kwenda shule za serikali za bweni kuwa ndogo ni kutokana na ufinyu wa shule hizo.

Vile vile, imesema vilitumika vigezo maalum kuchakata wanafunzi wenye ufaulu mzuri ikiwamo wa alama za juu.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais- TAMISEMI anayesimamia Elimu, Dk. Charles Msonde, shule za sekondari zilizochukua wanafunzi wa kidato cha kwanza ni 4,307 na kati yake za kutwa ni 4,269 na bweni 38 ambazo zina uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,224.

"Wale wenye viwango vya juu sana ndiyo waliochaguliwa, lakini hata hivyo waliofaulu kwa viwango vya juu pia ni wengi, hapa tunasema waliochaguliwa kwenda bweni wamepata daraja la kwanza A, lakini ukiangalia waliopata daraja hilo wapo wanafunzi 50,475, hivyo hata kwenye daraja hili la kwanza ipo kanuni iliyotumika ya kugawa nafasi za wanafunzi waliofaulu vizuri," alifafanua.

Alibainisha kuwa shule za bweni zimegawanyika katika makundi matatu ambayo la kwanza ni lenye ufaulu wa juu, la pili ni shule za bweni za ufundi na la tatu ni shule za bweni kawaida.

Dk. Msonde alisema shule zenye ufaulu wa juu ziko saba hata hivyo hakuzitaja, zenye nafasi kwa wanafunzi 932 ambao waliopangwa.

Alisema pia shule za bweni za ufundi ziko tisa zikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,323 wakati shule za bweni za kawaida zimechukua wanafunzi 1,816 na bweni umiliki wa mkoa 153.

Dk. Maspnde alisema wanafunzi waliopata ufaulu wa daraja kwanza (A) wako 50,475 na kati ya hao waliochaguliwa ni 4,224, kwenye shule za bweni zenye ufaulu wa juu.

"Niweke wazi kuwa ufaulu wa daraja la kwanza yaani A unaanzia kwenye maksi 241 hadi 300 na wazazi au walezi wanaona daraja ambalo mtoto wake amepata, lakini sisi tunaoingia kwenye mfumo tunaona alama sasa mtaona kwamba takribani wanafunzi 46,251 wenye ufaulu wa daraja la kwanza (A) wamepangiwa kwenye shule za kutwa kutokana na uhaba wa nafasi za bweni.

Akizungumzia kuhusu shule za bweni kawaida, Dk. Msonde alisema kanuni yake ni uwiano wa watahiniwa wote wa darasa la saba katika shule za vijijini au mazingira magumu katika halmashauri mara idadi ya nafasi zote za bweni kwa wavulana na wasichana wa vijijini.

"Lakini wale waliopangiwa bweni wanaufaulu wa daraja la kwanza wa alama za juu zaidi kuliko wale 46,251 na ndio maana tulivyofika ukomo wa idadi ya wanafunzi wanaotakiwa kwenda bweni wale waliobakia wenye ufaulu wa daraja la kwanza wote waliopangiwa kwenye shule za kutwa."

Kadhalika wanafunzi 1,069,717 walichaguliwa kwenda kwenye shule za kutwa, iliyokaribu na shule ya msingi aliyosoma. Uchaguzi wa wanafunzi hao iwe bweni au kutwa unahusisha wote waliosoma shule za serikali na binafsi

Alisema wanafunzi waliofaulu na kuwa na sifa ya kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 ni 1,073,941 na kati ya hao waliochaguliwa kujiunga na shule za bweni ni 4,224 ambao ni sawa na asilimia 0.39 ya wanafunzi wote waliochaguliwa.



Baadhi ya viongozi na wananchi wa Kijiji cha Ngwinde, Kata ya Litola, wilayani Namtumbo wakishiriki katika wiki maalum ya upandaji miti mkoani Ruvuma. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

## Tarime yakamilisha vyumba madarasa kwa 100%

**Na Samson Chacha,** TARIME

HALMASHAURI ya Mji wa Tarime mkoani Mara, imekamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 41 kwa Sh. milioni 820 zilizotolewa na serikali katika shule za msingi na sekondari.

Wanafunzi 1,811 walifaulu kujiunga na shule za sekondari katika halmashauri hiyo wakiwamo 13 waliochaguliwa kujiunga na shule za bweni, wavulana 10 na wasichana watatu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Gimbana Ntavyo, alisema Halmashauri ya Mji Tarime mwaka 2022, ilipata Sh. milioni 820 kutoka serikalini kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 41 na kukamilisha madarasa hayo kwa asilimia 100 kwa kiwango kinachotakiwa.

"Tunatarajia kuwapokea wanafunzi 1,811 waliofanya mtihani wa kumaliza darasa la saba mwaka jana na kufaulu wamo wanafunzi 13 wakiwamo wavulana 10 na wasichana watatu watakaojiunga katika shule za bweni na kutwa.

Mkurugenzi huyo aliwataka wazazi wa

watoto 1,811 waliofaulu mtihani kuwafanyia maandalizi muhimu na kumpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia fedha za ujenzi wa madarasa hayo yatakayowezesha wanafunzi hao kuingia wote kwa awamu moja.

Pia walipongeza mfuko na Mbunge wa Jimbo la Tarime ambao wamechangia kila shule mpya Sh. milioni 3.4 ili kukamilisha ujenzi katika shule hizo mpya.

# Shahidi aeleza mahakama alivyomtambua mtuhumiwa

**Na Grace Gurisha**

MKAGUZI Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Jesca Malia (37) ameieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam jinsi shahidi alivyomtambua mtuhumiwa aliyemwekea kilevi na kumwibia mali zake katika gwaride la utambulisho.

Shahidi huyo alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalila, wakati akiongozwa na Wakili wa Serikali, Mosie Kaima kutoa ushahidi dhidi ya Borgias Augustine na wenzake wawili.

Alidai kuwa Februari 21, 2022 majira ya mchana alikuwa Kituo cha Polisi Kijitonyama akiendelea na majukumu yake ya kazi, alipigiwa simu na mpelelezi Mayunga kuwa kuna mlalamikaji ambaye kesi yake ipo kwake kuwa anaweza kumtambua mshtakiwa.

Alidai kuwa alimweleza kuwa mlalamikaji huyo ambaye ni Consolatha Alphonce aende siku inayofuata kituoni hapo kwa ajili ya gwaride la utambuzi.

Shahidi huyo alidai, Februari 22, 2022 majira ya mchana Mayunga alifika kituoni hapo akiwa na Alphonce na kumwelekeza ampeleke kwenye chumba maalumu ili na yeye atafute askari wa kusimamia gwaride.

Alidai kuandaa gwaride la watu wanane ambao wanaendana na Augustine, aliwapanga mstari mmoja na mtuhumiwa akachagua kusimama kwa mtu wa kwanza kutoka kulia.

Alijaza fomu ya utambuzi kwa kuandika majina ya watu wote waliokuwa kwenye gwaride likiwamo jina la mlalamikaji Consolatha Alphonce, ilipomaliza alimuita askari Ernest ili ampeleke shahidi.

"Shahidi aliweza kumtambua mtuhumiwa ambaye alimshika kwenye bega lake, ambapo nikamuita askari Nande ili amtoe nje shahidi, baada ya hapo nikamalizia kujaza fomu kipande cha utambuzi," alidai shahidi.

Pia alidai kuwa baada ya zoezi hilo, mshtakiwa alirudishwa mahabusu na akaandaa maelezo ya alichokisimamia. Kesi itaendelea kusikilizwa Januari 10, 2023.

Ilidaiwa kuwa Agosti 23, 2021 mshtakiwa akiwa eneo la Hotel Elegance iliyopo Sinza, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam kwa nia ovu alimuwekea kilevi Consolatha Alphonce.

Katika shtaka la pili, siku hiyo hiyo na eneo hilo mshtakiwa Augustine anatuhumiwa kuiba simu janja aina ya IPhone yenye thamani ya Sh. milioni 2.9, Nokia yenye thamani ya Sh. 50,000 na kwa kupitia ATM kadi ya CRDB aliiba Sh. 700,000 mali ya Consolatha Alphonce.

Katika shtaka la tatu linalowakabili Ally Kibuga na Abdallah Manti, wanatuhumiwa tarehe zisizofahamika za mwezi Agosti, walipokea simu aina ya IPhone ambayo ilikuwa inajulikana kama imeibwa.

## Bandari ya Shanghai yawa na mizigo mingi licha UVIKO-19

Na Mwandishi Maalum

TAKWIMU zimeonesha kuwa Bandari ya Shanghai imeendelea kuwa yenye mizigo mingi zaidi duniani kwa mwaka wa 13 mfululizo katika mwaka 2022, licha ya janga la UVIKO-19.

Takwimu zilizotolewa na Kampuni ya Kimataifa ya Bandari ya Shanghai, ambayo ni mwendeshaji wa bandari hiyo zimeonesha kuwa makontena yaliyopakiwa na kupakuliwa kutoka bandari yalikuwa zaidi ya milioni 47.3 yenye urefu wa sawa na futi 20 (TEUs) kila moja mwaka 2022.

Taarifa hizo ni kwa mujibu wa habari zilizochapishwa na Tovuti ya Gazeti la Umma ya nchini China.

Ilisema wakati ikikabiliana na janga, pamoja na mawimbi ya joto na baridi mwaka jana, bandari hiyo ilihakikisha utendakazi thabiti wa Kituo cha Kimataifa cha Usafirishaji cha Shanghai na kulinda uthabiti wa minyororo ya kimataifa ya viwanda na ugavi.

Aidha, ilisema kutokana na milipuko ya hapa na pale ya janga hilo katika robo ya pili ya mwaka huu, bandari hiyo ilifanikiwa kurejesha kwa haraka huduma za makontena mwezi Julai, iliposhughulikia rekodi ya juu ya mwezi ya makontena milioni 4.3.

**Taarifa hizo ni kwa mujibu wa habari zilizochapishwa na Tovuti ya Gazeti la Umma ya nchini China.**

# Wakazi Rorya waunda umoja kuisaidia serikali

Na Samson Chacha, RORYA

ZAIDI ya wakazi 400 wa vijiji vya Kowak wilayani Rorya wameunda Jumuiya ya kujiletea Maendeleo (JMK) itakayojikita kuunga mkono juhudi za serikali kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa, zahanati, vituo vya afya, maji na miundombinu ya barabara.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Prof. Julius Nyahongo, alisema kuwa Kowak ni kijiji kilichotoa mchango mkubwa wa maendeleo ya nchi hata kabla ya kupata uhuru, Shule ya Kowak imetoa wasomi wengi nchini akiwamo aliyekuwa Mbunge hayati Ayila Omolo. "Kumekuwapo na vikundi na jumuiya mbalimbali za kijamii katika wilaya hii ya Rorya, lakini vingi vimekuwa vikijikita kwenye mambo ya misiba na kusahau juhudi za kuunga mkono kujiletea maendeleo ya pamoja na kuunga mkono serikali," alisema. Alisema jumuiya ya JMK inaundwa na vijiji sita vinavyozunguka Kowak na ina wanachama zaidi ya 400, haijihusishi na mambo ya kisiasa wala dini, inajikita kuunga mkono juhudi za serikali na wananchi kuchangia shughuli za kujiletea maendeleo hususani katika ujenzi wa vyumba vya madarasa, zahanati, vituo vya afya, maji na miundombinu ya barabara.

Alisema Rorya inafanya juhudi za kuunga mkono serikali katika maendeleo kwa kuwa ilikuwa inasuasua na kuwataka wanachama kuwa na mshikamano, umoja na upendo na maendeleo yatapatikana.

"Jumuiya yetu inajumuisha wana Kowak na wana Rorya wote walipo ndani ya Mkoa wa Mara na nje ya nchi ili tuungane kuchangia maendeleo ya wilaya yetu kwa ajili ya wananchi wetu."

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kowak, Kapis Otieno na wanachama wenzake wakiwamo Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, James Elias na Lameck Oliko, walisema wanampongeza Prof. Nyahongo kwa kuwajumuisha kwa pamoja na kuunda JMK ambayo itasaidia kuleta maendeleo na kuwaomba wana Rorya kuacha malumbano ya koo kwa koo, kuacha ukabila na kubaguana ili kupata maendeleo na serikali itawaunga mkono.



Mfanyabiashara katika Mtaa wa Kongo jijini Dar es Salaam jana, Samli Mniuka (kushoto), akimpima kiatu mwanafunzi ikiwa ni maandalizi ya shule zinazotarajiwa kufunguliwa wiki ijayo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# DC awacharukia wanaoharibu vyanzo vya maji

Na Thobias Mwanakatwe, MANYONI

MKUU wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, amewaonya wananchi wanaofanya shughuli za kilimo na kuchunga mifugo kwenye maeneo ya vyanzo vya maji kuacha au wakikamatwa watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Alitoa onyo hilo juzi wakati akifungua mkutano mkuu wa wadau wa maji wilayani hapo.

Mwagisa alisema Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) inajitahidi kuhakikisha wananchi vijijini wanapata maji kila sehemu, lakini tatizo wananchi ni chanzo cha kuharibu vyanzo vya maji kwa kulima mazao yao, kukata miti ovyo na kuchunga mifugo.

"Jumuiya za maji nawaagiza hakikisheni mnatoa taarifa mnapoona wananchi wanaoharibu vyanzo vya maji ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika," alisema.

Aliwapongeza RUWASA kwa kuendelea kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi katika vijiji vyote na maeneo yote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Fadhili Chimsala, alisema wananchi lazima watambue kuwa maji ni rasilimali muhimu sana katika maisha ya binadamu na maji ndiyo uhai, rasilimali za maji zitunzwe ili zidumu na kutoa maji wakati wote.

Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilson Ntiro, alisema taasisi hiyo itaendelea kufuatilia miradi ya maji ili ikamilike kwa wakati na ikiwa na kiwango cha thamani ya fedha zilizotumika.

Alisema kufanya uharibifu wa miundombinu ya maji ni kosa la jinai na ni uhujumu uchumi viongozi wanatakiwa wawaeleze wananchi kutunza vyanzo vya maji ili vidumu na viendelee kutoa maji kila siku.

Ntiro alisema Jumuiya za maji zihakikishe watu au taasisi zinaouza maji zina vibali maalumu vya kufanya hivyo kwa kuwa Sheria ya Maji 2009 inasema haruhusiwi mtu yeyote kuuza isipokua wenye kibali maalumu.

Mkuu wa Kitengo cha Uendeshaji na Matengenezo RUWASA, Mhandisi Maduhu Shija, alisisitiza suala la kupanda miti kuzunguka vyanzo vya maji ili viendelee kuwa hali nzuri na kutoa maji wakati wote.

"RUWASA itapenda kupata taarifa ya kila chanzo cha maji imepandwa miti mingapi na pia hakikisheni jumuiya zote mnawasilisha taarifa za kila mwezi kwani kwa kutokufanya hivyo tunaweza kuichukulia hatua jumuiya hiyo kwa kuifuta," alisema.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Jumuiya za Huduma za Maji ngazi ya jamii (CBWSO), Binto Manyama, alisema; kuanzia 16 hadi 22 Machi 2023 na jumuiya zote za watumia maji ziandike mapendekezo ya shughuli zitakazofanyika wakati wa wiki ya maji.




Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali (wa pili kulia), akikabidhi bango la mfano linaloonyesha ushindi wa kutimiziwa ndoto ya kufunguliwa biashara yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa Leonard Mayala Joseph, katika hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi wa kampeni ya Amsha Ndoto Amsha Shangwe na Vodacom Tanzania Plc, jijini Mwanza juzi. Wengine ni Meneja Masoko na Mkakati wa Biashara wa Vodacom, Venance Chapaulinge (kushoto) na Meneja Mauzo Mwandamizi wa Kanda ya Ziwa, Ahmed Akbarali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge awakumbuka mahabusu, yatima

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MBUNGE wa Jimbo la Mpanda Mjini, Sebastian Kapufi, ametoa msaada wa thamani ya Sh. milioni 1.4 kwa mahabusu wa Gereza la Mpanda na watoto yatima ili makundi hayo yajione hayajatengwa na jamii.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, mbunge huyo alisema alipata nafasi ya kuzungumza na mahabusu na kumshukuru kwa msaada huo.

Alisema walimwagiza afikishe salamu zao kwa jamii na waliiomba iwapokee pindi watakapotoka katika gereza hilo wakiamini kuwa wamekuwa watu wema ambao wamejifunza kutokana na makosa yao.

"Wamenikumbusha jambo moja kitendo cha mimi kushiriki nao kuwapelekea chakula mtu katoka mbali hana ndugu kabisa kwa hiyo mimi naweza kufikiri kwamba ile soda niliyopeleka, dawa ya meno, sabuni labda ni kitu kidogo, wao wanasema ni kitu kikubwa sababu narejesha furaha yao.

"Ukiacha hawa wafungwa pia watoto yatima nimepita hapa nilichojaliwa kidogo na Mungu nimewafikishia maziwa, pempasi, mafuta ya mawese lita 20 na pesa kwa ajili ya kubadilisha chakula," alisema Kapufi.

Mbunge huyo aliwatembelea pia wagonjwa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Katavi na kuwapa msaada wa vitu mbalimbali kwa matumizi yao.

Kaimu Mkuu wa Gereza la Mahabusu Mpanda Mrakibu Mwandamizi SSP Christopher Fungo, alimshukuru mbunge huyo huku akiomba na wadau wengine kujitokeza kutoa walichonacho ili kurudisha furaha ya mahabusu hao.

Msimamizi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Mtakatifu Yohane wa Pili, Sista Rose Sungura, alisema wanawalea watoto hao kimaadili, kiimani mpaka watakapopata uwezo wa kujitambua na kujisimamia wenyewe ili wawe msaada mkubwa katika jamii.

Mwajuma Mmbaga, Muuguzi Mfawidhi wa hospitali hiyo, alimshukuru mbunge huyo kwa uthubutu wake na pia walimwombea aendelee kuwatembelea mara kwa mara na kuwaomba wadau wengine kuiga mfano huo.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Serafini Patrice, alisema pamoja na kutoa huduma kwa jamii bado hospitali hiyo inakabiliwa na ukosefu wa gari la wagonjwa na kumuomba mbunge huo kuwasaidia kupaza sauti katika vikao vya Bunge.

# Upelelezi kesi kusafirisha dawa za kulevya wakamilika

**Na Grace Gurisha**

UPELELEZI kesi ya kusafirisha gramu 1001.17 za dawa za kulevya aina ya heroin inayomkabili mfanyabiashara Hussein Hariri na wenzake wawili, umekamilika.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Wakili wa Serikali, Caroline Matemu, wakati kesi hiyo ikitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Matemu alidai, upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na wanasubiri kuwasilisha taarifa Mahakama Kuu.

Alidai, awali waliwasilisha taarifa hiyo, lakini ilishindikana kutokana na changamoto za mfumo.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa na kupangwa Januari 16, mwaka huu.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mkazi wa Mbezi, Benson Muro na mkazi wa Magomeni Mapipa, Ramadhani Almas.

Washtakiwa hao wanadaiwa kutenda kosa hilo Machi 17, 2016 eneo la Kituo cha mafuta cha Oil Com, Mbezi Chini, Kinondoni, Dar es Salaam.

Ilidaiwa kwamba, bila halali washtakiwa hao walikutwa wakisafirisha kiasi hicho cha dawa za kulevya aina ya heroin kinyume cha sheria.

## Ashauri ufanyike utafiti mito na maziwa kugundua gesi, mafuta

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Kituo cha Utafiti cha Kilimo, Mifugo na Mazao cha Shamba Darasa kilichoko Kibaha, Ephrahim Massawe, ameshauri kufanyika utafiti kwenye mito na maziwa makubwa nchini kujua kama kuna mafuta na gesi.

Massawe alipendekeza hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jana katika kituo chake cha shamba darasa Kibaha kuwa yapo baadhi ya maziwa na mito yamegundulika kuwa mafuta na gesi utafiti huo unatakiwa kufanyika katika maeneo mengine zaidi.

Alisema utafiti ukifanywa kuna uwezekano mkubwa wa kupatikana mafuta ghafi na gesi kama walivyofanya nchi ya Uganda kwenye Ziwa Albert na kupata mafuta na ukifanyika nchini nishati hizo zinaweza kupatikana na kupunguza gharama kwa watumiaji.

"Tunaishauri nchi kufanya utafiti kwenye maeneo hayo kwa kushirikiana na nchi zinazozalisha nishati hizo ili tuweze na sisi kuzalisha kwa wingi na nyingine iuzwe nje ya nchi," alisema.

Massawe alisema endapo utafiti huo utafanywa na ikigundulika, itainua Pato la Taifa kwa kuwa nchi zinazozalisha nishati hizo uchumi wake uko juu duniani.

Alisema nchi ina maziwa yakiwamo Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Duluti na mito mikubwa Wami, Ruvu na Rufiji.

Licha ya msisitizo wa kutumia gesi majumbani kupunguza uharibifu wa mazingira, bado bei ya gesi iko juu hali inayochangia baadhi ya wananchi kushindwa kumudu gharama na kuendelea kutumia kuni na mkaa.



## Serikali yavunja mkataba makandarasi kuchelewesha kazi

**Na Mary Mosha,** MWANGA

SERIKALI imevunja mkataba wa makandarasi wawili wa Kampuni ya Engineer Plus na Petra, wanaojenga mradi wa mfereji wa umwagiliaji wenye thamani ya Sh. bilioni 1.6 unaotegemewa kuwanufaisha wananchi zaidi ya 1,200 wa Skimu ya Kirya.

Wakulima hao wanaojishughulisha na shughuli za kilimo cha mpunga, wanautegemea mfereji huo wenye urefu wa mita 3,400.

Jana, Mkurugenzi Mkuu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Raymond Mndolwa, alikwenda katika eneo la mradi huo kukagua utekelezaji wake ambao umefikia asilimia 50.

"Mkandarasi mpaka sasa alitakiwa awe amekabidhi kazi ndani ya mwaka mmoja, lakini amechelewa kukamilisha mradi huo kwa sababu ya kukosa mitambo ya kufanyia kazi. Mkandarasi mwenye Kampuni ya Engineer Plus, aliungana na PETRA kwenye mkataba wa ujenzi wa mradi huu.

"Baadaye hakufanya kazi na kumwachia Mkandarasi Engineer Plus, alisaini mkataba na serikali, lakini amekuwa akisuasua kila mara kujenga mradi huo na sehemu alizojenga bado zinamapungufu ambapo yatarekebishwa kwa fedha alizokatwa."

Alisema, Tume ilichukua hatua kwa baadhi ya watumishi akiwamo aliyekuwa meneja wa mkoa.

"Makandarasi ambao hamna uwezo wa kufanya kazi hizi, tunaomba msije kuomba kazi za tume, hatupo tayari kupoteza fedha ya serikali, tutawachukulia hatua na kuvunja mikataba yenu kwa mujibu wa sheria kanuni na taratibu," alisema Mndolwa.

Akizungumzia mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdala Mwaipaya, aliitaka tume hiyo kujitahidi kuishirikisha hatua kwa hatua zinazofanyika kwenye miradi iliyoko wilayani ili kusaidia ufuatiliaji wa karibu.

"Sio huo tu bali miradi yote inayotekelezwa na wizara inapofika katika ngazi ya wilaya inapitia matatizo mengi yakiwamo ya usimamizi pamoja na makandarasi kukimbia maeneo ya tukio hali hiyo imepelekea ucheleweshaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kupoteza fedha nyingi za serikali," alisema Mwaipaya.

Diwani anayewakilisha wakulima wa Kata ya Kirya, Abbas Hassan, alieleza namna mkandarasi huo alivyokuwa na migogoro na vibarua wake, kuwa alikuwa hana vifaa vyakutosha.

"Hatujui huyo mkandarasi alipatikana vipi, hana wataalamu, na wakija wanakuja kutokana na jio wa viongozi , hali hiyo imepelekea mradi kuchukuwa miaka miwili badala ya mwaka mmoja, serikali iangalie watu wakufanya nao kazi ili kutopoteza fedha ya serikali, huyu mhandisi wa mkoa alikuwa ni msanii sana, naye amechangia mradi kukwama," alisema Hassan.

# Askari, wakaguzi 29 waenda India kujifunza kukabiliana uhalifu kimtandao

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ASKARI na wakaguzi 29 wa Jeshi la Polisi nchini, wamepelekwa nchini India kupigwa msasa ili kuja na mbinu mpya za kukabiliana na masuala ya uhalifu na unyanyasaji wa watoto katika mitandao ya kijamii.

Taarifa iliyothibitishwa jana na Msemaji wa Jeshi hilo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Misime David, inaeleza kuwa askari hao pia watanolewa kuhusu makosa ya kimtandao pamoja na ulinzi wa taarifa binafsi.

"Hao askari tayari wako India na watakuwa huko kwa mafunzo juu ya unyanyasaji wa watoto katika mitandao na kushughulika na makosa ya kimtandao. Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camilius Wambura, alipata fursa hiyo na akaamua kuelekeza askari hao na wakaguzi kujifunza kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

"Tutaendelea zaidi kuhakikisha askari na maofisa wetu, wanapata elimu na weledi zaidi wa kuzuia uhalifu, kupeleleza kesi pale zinapotokea. Tutawapa mafunzo ya ndani na ya nje na mwishoni mwa mwaka jana, tulishaanza mafunzo mbalimbali kila mkoa na tunaendelea nayo," alisema SACP Misime.

Misime alisema mkakati mwingine ambao jeshi hilo limejiwekea katika mwaka huu ni kuhakikisha hali ya usalama inazidi kuimarika zaidi kuliko mwaka uliopita, kwa kutoa elimu kwa umma.

Alisema ili kudhihirisha hilo, jeshi hilo limepeleka wakaguzi katika kata ili kwenda kushirikiana na viongozi wengine, kuwapa wananchi elimu kuhusiana na mambo ya ulinzi na usalama, vyanzo vya uhalifu ni vipi na jinsi ya kujipanga ili kuwanyima wahalifu fursa ya kufanya uhalifu wa aina yoyote.

"Sisi Jeshi la Polisi tunaamini elimu ni silaha kubwa, hivyo tutaitumia kupunguza uhalifu kwa kufanya mikutano katika vijiji, vitongoji katika nyumba za ibada ili wananchi watambue kuwa usalama unaanza na wao," alisema SACP Misime.

Pia, aliwaomba wananchi kushirikiana na jeshi hilo kuhakikisha wanabaini na kuzuia uhalifu, ambapo mwaka huu wanatamani kuhakikisha wanazuia zaidi kuliko kusubiria uhalifu utokee ndipo waanze kutafutana.

Alisema yapo matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto, ambayo ndiyo yanayoongeza matukio nchini, huku akitoa wito kwa kila familia kukaa na kupeana elimu ya ubaya na madhara ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto.



Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Manyara (MPC), Mary Margwe, akizungumza na waandishi wa habari mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali kukarabati makazi ya wazee, wasiojiweza

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI imepanga kuanza utekelezaji wa ukarabati na uboreshaji wa huduma na makazi ya wazee na wasiojiweza ili kuwawekea mazingira mazuri ya kuishi na kutatua matatizo yanayowakabili.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, alieleza mkakati huo jana, alipotembelea Kituo cha Makazi ya Wazee cha Misufini kilichoko Kijiji cha Umba, Kata ya Ngomeni, Wilaya ya Muheza.

Alisema kutokana na matatizo mengi, ikiwamo maeneo yenye makazi kuwa na migogoro ya mipaka na ukosefu wa huduma muhimu kama matibabu, serikali imeona ni vyema kuwaboreshea maeneo hayo ili kuwawezesha kuishi maisha yaliyo bora.


"Tunawashukuru sana wazee wangu pamoja na wenzenu kwa kazi kubwa mliyoifanya katika taifa hili, uzee haukwepeki kwa maana hata ninyi mlikuwa vijana, kwahiyo tuna jukumu na wajibu wa kuhakikisha mnakula na kunywa vizuri, lakini tunawaboreshea miundombinu ili muweze kuishi vizuri," alisema.

"Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, amepewa nafasi, kwa hiyo ameahidi kuitumia kuboresha maisha ya makazi ya wazee. Kwa sasa serikali ina mpango kabambe wa kukijenga upya kituo hiki kwa kufanya ujenzi mkubwa, tayari tunayo rasilimali fedha na mkandarasi ameshapatikana," alisema Mgumba.

Ofisa Ustawi Mfawidhi wa kituo hicho, Mwamvita Kilima, alisema makazi hayo yalianzishwa mwaka 1984 na kwa sasa yanahudumia wazee wasiojiweza 19, wakiwamo wanawake watano na wanaume 14. Kilima, alisema uongozi wa makazi hayo, unaipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za jamii kama kupatikana kwa majisafi.

"Ni jambo la kumshukuru Mungu, kwa sababu viongozi wetu wanaoongozwa na Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan wanakitupia macho kituo hiki. Mpaka kufikia sasa wameshafanya utambuzi wa eneo la makazi, lakini wazee wameanza kupatiwa huduma za afya kutoka kwenye hospitali ya wilaya," alisisitiza.

Hata hivyo, Kilima alieleza kuwapo kwa matatizo yanayoyakabili makazi hayo, kuwa ni pamoja na eneo hilo kuwa na utata wa mipaka. Inaelezwa kuwa wataalamu waliofanya utambuzi wamebaini mwingiliano mkubwa wa ekari 300 katika 523 zenye mgogoro na wananchi.





# H'shauri Kilindi yatenga ekari 6.8 uwekezaji kilimo

**Na Dege Masoli,** KILINDI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, imetenga ekari 6.8 kwa ajili ya uwekezaji mkubwa na kilimo cha mazao ya chakula na biashara.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa Idara ya Viwanda na Biashara, Ephron Mntambo, eneo hilo ni sawa na hekta 2,757.972 za ardhi zilizotengwa kwa ajili ya kilimo kwenye vijiji vinne vilivyoko wilayani humo.

Alitaja vijiji vitakavyonufaika na uwekezaji huo wa kilimo kuwa ni Sangeni, Mkuyu, Mbwego na Tobacco. Alisema fursa hiyo ya uwekezaji katika mazao ya biashara na chakula itayahusu mazao ya mahindi, mhogo, alizeti, mbaazi, mkonge, korosho, maembe na tumbaku.

Alisema Wilaya ya Kilindi, ina ardhi yenye rutuba inayojitosheleza kwa kilimo cha mazao yote ya chakula na biashara na wakulima wamenufaika kwa kilimo cha mahindi na maharage kama mazao ya chakula na alizeti, iliki na maembe kwa biashara.

"Wilaya ina eneo la hekta 612,900 na 290,030 kati ya hizo zinafaa kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara...eneo linalolimwa kwa sasa ni hekta 117,220 sawa na asilimia 40.4 ya eneo linalofaa kwa kilimo," alisema Mntambo.

Eneo la wilaya ni hekta 621,984 na la kilimo ni hekta 294,232 (48%), linalolimwa ni hekta 191,251 (65%). Hata hivyo, alisema kilimo cha mkono ni hekta 124,313 (65%), kilimo cha ng'ombe ni hekta 28,688 asilimia 15 na hekta 38,250 (20%) ni kilimo cha tractor.

Aidha, alitaja maeneo ya kilimo cha umwagiliaji kuwa ni jumla ya ekari 2855 ambazo zinaweza kulimwa nyanya, bilinganya, ngogwe, pilipilihoho, tikitimaji, bamia, vitunguu, mpunga, mahindi na miwa na kwamba sekta ya mifugo inayochangia halmashauri kwa asilimia 28 kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo kimkoa.

Sekta ya uvuvi, Mntambo alisema kwa sasa wilaya ina mabwawa 72 ya kufugia samaki yenye eneo la mita za mraba 14,400 yanayomilikiwa na watu binafsi 142 vikiwamo vikundi 11 kwenye kata 10 wilayani hapa.



Mfanyabiashara katika soko la wamachinga Msikiti Mkuu wa Ijumaa, Muheza Mjini mkoani Tanga, Ally Rajabu (kushoto), akimuuzia sare za shule Idd Mussa (kulia) ikiwa ni maandalizi ya kufunguliwa kwa shule wiki ijayo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wananchi walioezuliwa nyumba watakiwa kuwa watulivu

**Na Hamida Kamchalla,** MUHEZA

WANANCHI wa kijiji cha Songa Batini, Kata ya Songa wilayani Muheza, wametakiwa kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho wamepata maafa baada ya nyumba zao kuezuliwa kutokana na mvua iliyonyesha ikiambatana na upepo mkali.

Mbunge wa Muheza (CCM), Hamisi Mwinjuma, alisema mvua inayoendelea kunyesha imesababisha hasara hiyo ya makazi na mali, baada ya kuzuka upepo mkali uliosababisha nyumba 16 kuezuliwa paa.

Kutokana na athari hiyo, serikali imelipokea jambo hilo na viongozi wa kijiji husika, wameanza utekelezaji kutafuta fedha kwa hali na mali, kwa ajili ya kuanza ujenzi mpya kwa kila aliyepata maafa hayo.

"Nimechelewa kupata taarifa hii, lakini baada ya kusikia nimekuja hapa ili tuliweke sawa hili kwa kuanza ujenzi wa nyumba zilizoharibiwa, wananchi wameshaanza kuchanga fedha, lakini na sisi tumeongeza zaidi ili kukamilisha ujenzi wa nyumba imara.

"Lakini hapa mbele ya wananchi nimemuagiza Mkurugenzi wa halmashauri yetu asimamie suala hili na ameahidi kesho atafika na kuona namna ya kuanza ujenzi kwa wananchi, nitoe wito kwa wananchi waliopata mtikisiko, wawe wavumilivu katika kipindi hiki cha maafa, kila kitu kitakwenda sawa."

Aidha, ameagiza kwa serikali ya kijiji kufanya tathmini ya samani za waathirika zilizoharibika ili kuona watawafidia vipi kulingana na idadi ya samani hizo.

Diwani wa Songa, Boniface Edward, alibainisha kwamba serikali ya kijiji imekaa na kujadiliana na wananchi hao na tayari wanaanza harakati za ujenzi wa nyumba kwa waathirika huku akitoa wito kwa wananchi kuwa wamoja hasa katika kipindi hiki.

Baadhi ya wananchi waliopata maafa hayo walisema wanamshukuru Mungu hawajapata madhara makubwa ya watu kujeruhiwa zaidi ya kuharibikiwa na samani za ndani, pia serikali ya kijiji chao pamoja na mbunge kuwa mstari wa mbele kwa kushirikiana na kuwaunga mkono katika suala hilo.

"Mvua haikuwa kubwa sana, ilinyesha kama dakika 10 tu na ilipokata ulikuja upepo mkali sana ambao ulianza kufumua nyumba na mapaa kuanguka bila mpangilio, watu tulijihami kwa kujificha, lakini hatuna uhakika paa litaangukia wapi," alisema Saidi Mpimbili, mwathirika wa tukio hilo.

"Baada ya tukio hili kutokea, kwanza tulihamaki kujua tunaweza kupata madhara makubwa tukihofia hata kupoteza maisha lakini Mungu amesaidia, pia tunawashukuru viongozi wetu kwa kuwa karibu na kushirikiana na sisi," aliongeza.

Alisema baadhi ya watu wameharibikiwa na samani zao za ndani na kudai kuwa yeye ni mmoja wao ambaye amepata hasara hiyo.

## Fedha zatengwa uwekezaji wananchi kufanya kilimo

**Na Oscar Assenga,** TANGA

HALMASHAURI ya Jiji la Tanga, imeanza mikakati ya kuanza kutenga fedha kwa ajili ya uwekezaji wa ardhi ili wananchi wake waweze kufanya shughuli mbalimbali za kilimo.

Mkakati huo ulitangazwa jana na Meya wa jiji hilo, Abdurhaman Shiloow, alipokuwa akizindua mradi wa kilimo biashara unaotekelezwa na Shirika la Economic and Social Research Foundation (ESRF) kwa kusimamiwa na SUGECO.

Uzinduzi huo ulikwenda sambamba na majadiliano ya Mradi wa Tanga Yetu, wenye lengo la kuinua vijana kupitia sekta ya kilimo katika jiji hilo, ambapo shughuli zitakazofanyika ni kuunda makundi yatakayowafanya kuwa pamoja katika kukamilisha na kusimamia miradi.

Shirika hilo linasimamia utekelezaji wa miradi ya Tanga Yetu, ambapo mradi huo utasaidia vijana wanaojihusisha na shughuli za kilimo kufanya kilimo chenye tija ikiwamo kutambulisha kilimo cha kisasa kupitia teknolojia ya hydroponic.

Alisema wanafanya uwekezaji kutokana na ufinyu wa ardhi na wameanza kujipanga kutafuta maeneo ya uwekezaji nje ya jiji hilo na wanaamini itawasaidia vijana wanaohitaji ajira na kujiajiri kupitia kilimo.

"Katika mpango wetu wa bajeti wa mwaka 2023/2024 tukishirikiana na mbunge wetu Ummy Mwalimu, Baraza la Madiwani, tuna mpango wa kufanya uwekezaji kwenye kilimo na ardhi itakayotumika katika kilimo," alisema Mstahiki Meya.

Alizitaja wilaya za pembezoni, ambazo wameanza kuonyesha nia ya kufanya uwekezaji kuwa ni Mkinga, Muheza na Pangani.

Awali, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mtafiti kutoka Shirika la Economic and Social Research Foundation (ESRF), Patrick Waziri, alisema mradi huo utawasaidia vijana wanaojishughulisha na kilimo kwa kufanya kuwa cha kisasa na chenye tija kupitia teknolojia ya hydroponic katika jiji hilo.

Alisema lengo lao sio kuangalia kilimo pekee bali wanataka kiweze kuwa cha kibiashara na wanaona namna ya uwezeshaji wa vijana kiuchumi ili waweze kujikwamua kimaendeleo.

"Tulikaa na vijana wanaofanya kilimo kuwauliza changamoto zao na tukagundua tatizo kubwa ni namna ya kupata masoko kwa bidhaa wanazozalisha hazikidhi masoko ya ndani na nje kwa sababu ya ubora mdogo," alisema waziri.

Alisema kupitia mradi huo utawapa mbinu mbalimbali zitakazowawezesha kufanya kilimo kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

"Katika mradi huu wa kilimo tutatumia Modern Agriculture Technology ambayo mojawapo ya umwagiliaji wa kisasa nyingine ni kilimo kwa kutumia Green House ambao watakuwa wanalima mwaka mzima bila kutegemea mvua kwa kuwa wanafanya umwagiliaji," alisema Waziri.

Alisema katika mradi huo wa kilimo watatambulisha teknolojia hiyo ambayo inafanya kilimo bila kutumia udongo na kupanda mazao, ambayo itakuwa ni mpya mkoani humo na Tanzania na ni watu wachache wanaoitumia.

Ukurasa 14




**Jumuiya ya Afrika Mashariki inaposuasua, ikiahirisha mpango sarafu moja hadi 2024**

Ukurasa 15



Funzo kwa wazalisha nishati Afrika, wanalosoma vita Ukraine na Russia

Ukurasa 19



**DONALD TRUMP Ana 'jambo lake' ni Ikulu tena 2023, adaiwa kuwa mfupa mgumu hazuiliki**



# Ndivyo Samia Suluhu Hassan anavyoakisi 'suluhu' ya kisiasa

• Adhihirisha upinzani na serikali uvumilivu kisiasa haukwepeki

**Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameonyesha ukomavu wa kisiasa na kufungua ukurasa mpya kwa kuleta 'suluhu' sawa na jina lake linavyosomeka.

Ni suluhu inayoruhusu kurejeshwa tena mikusanyiko, harakati na mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, iliyokuwa imefungiwa kuanzia 2015 na awamu ya tano ya John Magufuli.

Kwa ujumla Tanzania ilikuwa inalalamikiwa kwa kupungua kwa nafasi ya kiraia( civic space), kubinywa demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari mambo yakiwa magumu zaidi kuelekea kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28,2020.

Rais Samia tangu kuingia madarakani ameleta jambo jipya ni baada ya kuondolea mbali katazo la kuruhusu mikusanyiko na harakati za kisiasa ilikuwa ikiviminya vyombo vya habari na kufungia magazeti na taasisi nyingine za kuhabarisha umma.

Anaanza hatua kwa hatua kuachilia uhuru wa habari, akishauri kuwe na ukosoaji lakini wenye kujenga na kuleta maoni mbadala, kushirikiana na wana habari hata akikutana nao mwaka jana na kuzungumza mengi kuhusu hali halisi.

Ukawa mwanzo wa kupokea ushauri wa wanahabari na kuunda Wizara ya Habari, Mawasialino na Teknolojia ya Habari kutoka iliyokuwa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Jana anaufungua ukurasa mpya kisiasa baada ya kujua kuwa kukataza mikusanyiko ya kisiasa na mikutano ya hadhara kunadhoofisha uwezo wa vyama vya siasa kufanya kampeni na kutafuta haki, kukosa serikali, kushauri na kuendeleza demokrasia.



Rais Samia 'si wakati wa kurudi tulikotoka'. **PICHA: IKULU**

Katika awamu ya tano kuanzia Januari 2019, serikali ilifanyia marekebisho Sheria ya Vyama vya Kisiasa na kuweka rasmi msingi wa kuzuia haki ya kukusanyika

Januari 2019, bunge lilipitisha marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo yaliweka mazingira magumu ya kufanya kazi kwa vyama vya siasa, na kukandamiza uhuru wa kukusanyika au kujumuika na kuanzia hapo hata mikutano ya ndani ya vyama ilikuwa vigumu kufanyika.

Marekebisho ya sheria hiyo yalileta ugumu kwa vyama vya upinzani na mojawapo ilikuwa kuharamisha kutoa elimu ya uraia bila kibali kutoka kwa Msajili wa Vyama na kosa hilo lilibeba adhabu ya faini ya hadi Shilingi milioni 30 au kifungo cha hadi mwaka mmoja.

Kwa ujumla kitendo hicho cha kuwa na sheria inayokandamiza demokrasia kililalamikiwa kuwa kinakiuka katiba, lakini pia Mkataba wa Afrika na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa ambavyo vyote vinatoa haki ya uhuru wa kupata habari, kujieleza na kujumuika.

**2023 YA SAMIA**

Rais Samia anapiga hatua nyingine baada ya kuamuru kuondoa zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa, pamoja na kukwamua mkwamo wa mchakato wa katiba mpya uliosimama zaidi ya miaka minane sasa.

Anapozungumza na viongozi wa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu Dar es Salaam jana, anasema: 'Serikali inadhamiria kukwamua mchakato wa marekebisho ya katiba, kwa jinsi tutakavokuja kuelewana huko mbele. Wengine wanasema tuanze na katiba ya Warioba, wapo wanaoishauri katiba pendekezwa, lakini kuna mambo ya ulimwengu yamebadilika".

Anasema itaundwa kamati maalumu kwa ajili kutoa ushauri wa namna ya kwenda kupata katiba akiongeza kuwa si muda mrefu, kamati itaundwa na kushauri.

"Nataka kusema katiba hii ni ya Watanzania si ya vyama vya siasa," anasisitiza.

Anaongeza kuwa ukiacha katiba mpya, kwa muda mrefu kulikuwa na kilio hasa kutoka kwa wanasiasa na jamii za kimataifa kuhusu haki ya kufanya siasa hasa mikutano ya siasa kuruhusiwa, ambayo ipo kisheria na kikatiba.

'Hii ni haki kwa sheria zetu, ni haki kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara', uwepo wangu leo mbele yenu

INAENDELEA UK. 20

# Jumuiya ya Afrika Mashariki inaposuasua, ikiahirisha mpango sarafu moja hadi 2024

Na Nimi Mweta

WANACHAMA wa Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), wamesogeza mpango wa kuunda sarafu ya pamoja ifikapo mwaka 2024, ambao ulikubaliwa tangu 2014 na kuweka lengo la kufikia azma hiyo katika kipindi cha miaka 10.

Ni mojawapo ya malengo ya uwepo wa EAC ambayo yamekuwa yakiangaliwa upya au kusogezwa mbele kutokana na mazingira ya utekelezaji wake kutokuwa wa kiwango cha kuridhisha, kinachoendana na lengo lenyewe.

Lengo la kwanza ambalo ni wazi halipo kwa sasa ni kuwepo kwa mfumo wa shirikisho lililokuwa liundwe mwaka 2012, ambalo lilikataliwa na Tanzania katika kura ya maoni miaka mitano kabla ya hapo.

Ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki ni jambo linalotokana na hali halisi pamoja na historia, ila mikwamo ya kina inazuia kufikia malengo ya kipindi fulani, hivyo kulazimika kubakia katika malengo ya msingi bila kuwa na uwezo wa kufuatilia malengo makubwa ya ziada.

Mwaka 1999 wakati jumuia inaundwa upya kutoka pale ilipoanguka mapema mwaka 1977 ilikuwa na malengo makubwa ya kufikia umoja, kwa dhana ile ile ya jadi kuwa sisi ni ndugu na tuna haja ya kurudisha umoja, kwani ukivuka mipaka unakuta ndugu wale wale.

Hiyo ni kweli, ila hali ya mifumo ya siasa na aina za migongano hadi uhuru na baada ya hapo imehakikishwa kuwa kila nchi italinda uhuru ilionao.

Nje ya suala hilo la sarafu ya pamoja, au lile la kuundwa kwa serikali ya shirikisho, lengo la soko la pamoja limetekelezwa kwa kiasi, tena kwa kivuli cha Umoja wa Forodha ambayo pia inabeba dhima ya soko la pamoja.

Siyo rahisi kutenganisha 'umoja wa forodha' na 'soko la pamoja' kama dhana bila kuingia katika kina cha maeneo hayo, na ni katika kuyafuatilia kwa undani ndipo unaona mkwamo ulipo. Dhana ya umoja wa forodha ni kuingiza vitu ili viuzwe katika eneo lote husika bila kodi za ziada, hivyo ni soko la pamoja.

Lengo la soko halisi la pamoja ni mifumo ya uzalishaji wenyewe iunganishwe, hivyo mtu aweze kupanga kwenda huku au kule ndani ya jumuiya ili anunue anachotaka iwe ni kuanzisha kiwanda, mgahawa au duka, mradi awe na hati ya kusafiria ya Afrika Mashariki, au ya nchi mojawapo.

Ni kutoa uhuru mpana wa mzunguko wa watu, fedha na mitaji na bidhaa, wakati ambapo katika umoja wa forodha ni bidhaa tu zinazoweza kupelekwa eneo lolote katika ukanda huu, mengine yote yanabakia chini ya himaya ya taifa linalohusika.

Hatua ya soko la pamoja haipo; juhudi kubwa za Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani ni kustawisha umoja wa forodha.

Kuweka lengo la sarafu ya pamoja ilikuwa ni sehemu ya kustawisha hatua ya soko la pamoja na siyo ile ya umoja wa forodha ambayo ilifikia aina ya ukamilifu wa kutekelezwa, licha ya kukwama mwaka 2006. Ina maana nchi za jumuia zimefanikiwa kiasi kidogo cha lengo hilo, kwani ni miaka 16 tangu hatua hiyo imefikiwa na inaboreshwa hatua kwa hatua.

Ziko nchi zimejitahidi kuingia katika hatua ya soko la pamoja lakini ukichunguza unakuta migogoro hata katika utekelezaji wa umoja wa forodha, hivyo si rahisi kusema kuwa ipo kambi ya nchi zilizoko tayari kwa suala hilo, kama ilivyodhaniwa hapo awali.

Kuna wakati Tanzania ilikuwa inasakamwa moja kwa moja kama kizuizi cha soko la pamoja, na hasa hitaji la kuelekea shirikisho la Afrika Mashariki, na kwa upande fulani madai hayo yalikuwa na ukweli. Jambo la kushangaza ni kuwa nchi hizo hazikuweza kupiga hatua kwa masuala bila ushiriki wa Tanzania anayejivuta miguu, wakati ilikuwa inawezekana wakaanza hatua hizo kwa dira ile ile ya soko la pamoja. Ingetazamiwa kuwa Tanzania itajiunga baadaye pale ikijisikia kuwa imejiandaa vya kutosha, au faida za hatua hizo hazipingiki.

Hatua ya msingi ni kutumika kwa hati ya kusafiria na kuweza kuweka maskani popote mradi nchi hiyo ni mwanachama wa Jumuia, anunue mali ambayo haihamishiki kwa minajili ya kufanya biashara. Anaweza pia kuajiri watu ambao anawataka, kwani si wenye mitaji tu wanakuwa na haki ya kusafiri ili kuingia nchi nyingine na kujistawisha ila hata wafanyakazi. Tanzania ikaanza kupata woga ikijua kwa mfano kuwa Wakenya na Waganda wanaomanya Kiingereza 'wangepora' sehemu kubwa ajira sekta binafsi, kampeni ya 'hapana' ikatawala.

> Siyo rahisi kutenganisha 'umoja wa forodha' na 'soko la pamoja' kama dhana bila kuingia katika kina cha maeneo hayo, na ni katika kuyafuatilia kwa undani ndipo unaona mkwamo ulipo. Dhana ya umoja wa forodha ni kuingiza vitu ili viuzwe katika eneo lote husika bila kodi za ziada, hivyo ni soko la pamoja.



Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. **PICHA: MTANDAO.**

Suala shirikisho liliingizwa katika mdahalo mwaka 2007 kwa nia ya kufikiwa mwaka 2012 kama njia ya kutatua kusitasita kisiasa na kuunganisha dhamira, kwa njia ya utaifa wa pamoja kuondoa hitilafu hizo. Ila hapakuwa bado na mazingira ya mzunguko au mahamisho ya mitaji kimataifa ambayo yanahitaji Afrika Mashariki iwe eneo moja ili ifaidike na mazingira hayo.

Ni hali tofauti ambayo sasa inaanza kujitokeza, kwa mfano bomba la mafuta kutoka Uganda kuingia Tanzania kufika bandarini, au bomba la gesi kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa, Zambia kuanza kutumia bomba la mafuta (TAZAMA) kupeleka gesi asilia nchini humo.

Ziko benki kadhaa zinaunganisha nchi tofauti. Miunganiko ya kiuchumi huwa inahitaji misingi sawia ya kisheria, mikataba wezeshi kuondoa hitilafu mwekezaji kudhulumiwa na sheria za nchi nyingine.

Kutaka iwepo sarafu ya pamoja ilikuwa ni njia ya ziada kuunganisha shughuli za uchumi na kuweka mifumo ya usimamizi wa fedha (bajeti, urari wa malipo nchi za nje na deni la nchi kwa jumla, thamani ya fedha) katika mpangilio unaofanana. Ingebidi mifumo hiyo ya usimamizi wa thamani ya fedha (sarafu) ya kila nchi uwekwe ili hata ukioanishwa kuwa kitu kimoja (sarafu mpya) kusiwe na mvutano wa thamani ya vitu madukani, uwezo wa serikali kulipia miradi ya maendeleo, n.k. Mikwamo ilianzia hapo, kuoanisha viwango vya ujazo wa bajeti, deni la taifa, thamani ya sarafu na vizuizi kuzuia kupanda bei za bidhaa; nchi zilikuwa ziingiliwe kwa kiasi kikubwa, bila faida iliyo bayana.

Ni katika mazingira hayo ambako mradi wa sarafu ya pamoja umewekwa pembeni kwani maandalizi bado ni haba, yaani utayari wa kitaasisi hautoshi kuweka lengo halisi la kufikia sarafu ya pamoja hapo Januari 2024. Kwa upande mwingine mkakati huo unaanza kupitwa na wakati, hasa kutokana na hatua ya kufungua mipaka ya biashara kati ya nchi za Afrika, na mwelekeo mkubwa wa kutafuta masoko ya kimataifa, hivyo kuboresha mifumo ya kikanda ni suala la ziada.

# Funzo kwa wazalisha nishati Afrika, wanalosoma vita Ukraine na Russia

## • Ni kuzalisha, kuuziana kwenye soko la ndani



Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Danstan Kitandula.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Lulu George,TANGA**

ATHARI za mgogoro wa Ukraine na Urusi ulioanza Februari mwaka jana, unaendelea kuumiza uchumi wa dunia, lakini pia kuna fursa ni ya kuziamsha nchi za Afrika zinazozalisha mafuta na gesi kujipanga, kuungana, kuweka mikakati ya pamoja katika kuwekeza na kuongeza uzalishaji wa nishati ili kukabiliana na changamoto za vita hivyo na uhaba wa nishati ndani ya nchi zao.

Vita vya Ukraine na Urusi vimekuwa na athari kwa Afrika kwa kupandisha gharama za mafuta na gesi kwenye soko la dunia, hali inayoathiri maisha ya watu kutokana na kupanda maradufu kwa bei za vyakula ikiwamo ngano, mafuta na mchele, mbolea huku sekta ya utalii nayo ikitetereka, anasema Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Danstan Kitandula.

Katika mazungumzo na Nipashe, ana ushauri, akitaka kuwe na kuchangamkia fursa, miongoni mwa nchi za Afrika wazalishaji mafuta na gesi wanapaswa kuja na mkakati mmoja wa kupata suluhu ya athari za vita vya Ukraine na Urusi.

Anasema hawa ni pamoja na Algeria, Angola, Equatorial Guinuea, Libya, Nigeria, Senegal, Uganda na Tanzania, akiongeza kuwa kwa pamoja zikiibua mkakati wa pamoja itakuwa ni hatua itakayowezesha kudhibiti bei kwenye soko la dunia sambamba na kujiwekea akiba kwa mahitaji ya sasa na baadae.

Kitandula ambaye pia ni mbunge wa Mkinga (CCM) anasema ni wakati sasa wa nchi za Afrika kujiimarisha kufanya biashara wenyewe kwa wenyewe kwenye soko la ndani na kama mataifa wazalishaji licha ya kuwa hatua hiyo itachukua muda mrefu lakini itatoa matokeo chanya na endelevu.

"Mafuta ni bidhaa ambayo wazalishaji wake wameweka mkakati wa kudhibiti soko na kimsingi biashara hiyo inafanyika kwenye masoko yaliyowekwa kikanda ikiwamo Marekani, Ulaya, Uarabuni, India na China na kufungamanishwa na viwanda vya kusafisha mafuta ghafi."

Anasema katika hali hiyo nchi za Afrika zinazozalisha mafuta nazo zingejiingiza kwenye mfumo huo ili kuwa na nguvu ya pamoja kama wazalishaji katika kudhibiti soko na itapendeza zaidi kama sasa biashara hiyo itafanyika kwa Waafrika wenyewe kwa wenyewe.

Anafafanua kuwa dunia ipo mbioni kupunguza na hatimaye kuachana na matumizi ya mafuta na kujielekeza katika matumizi ya nishati safi isiyochafua mazingira. Hatua hii kwa upande wa nchi za Afrika itahitaji zaidi busara itumike katika kuweka mikakati ya kutambua, kuendeleza na kudhibiti rasilimali yao inayohitajika katika uzalishaji wa nishati safi.

**KITUO CHA MAFUTA**

Kwa upande wa baadhi ya wadau na wafanyabiashara wa mafuta wanasema kuwa upo uwezekano kwa Tanzania kuweka mazingira wezeshi na kuwekeza kwa kujenga maghala makubwa ya kuhifadhi mafuta mradi utakaowezesha wauzaji wa nje kutumia kama kituo kikuu cha uuzaji na usambazaji wa nishati hiyo kwa nchi jirani hasa zisizo na bahari.

Anwar Abeid mmoja wa wadau wa sekta ya mafuta hapa nchini anasema: "Nchi za Afrika zikiweza kuungana na kuwekeza kwa kufanya biashara wenyewe kwa wenyewe hali itakuwa nzuri na gharama za nishati hii zitashuka na hata serikali yenyewe itaweza kuingiza kodi nzuri kupitia sekta hii, kila mmoja atafaidika na kile kitakachopatikana kuanzia mzalishaji, mfanya biashara mpaka mlaji."

Anaeleza kuwa mfumo unaotumika kwa sasa hapa nchini kwa usimamizi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umekuwa na manufaa kwa kuwepo wa uhakika wa nishati hiyo nyakati zote sambamba na unafuu wa bei ingawa tatizo ni kukosekana kwa utoshelevu wa maghala ya kuhifadhi kwa kipindi cha miezi mitatu hadi sita.

"Ukweli ni kwamba kwa sasa wauzaji wote wa mafuta wananunua nishati hiyo kutoka nchi za Ghuba baada ya Urusi kuwekewa vikwazo vya kiuchumi. Hali hii inapaswa kuwa ni somo kwenye nchi za Afrika kuondoa utegemezi huo kwani zipo nchi ambazo zinazalisha mafuta na gesi ni suala tu la kujiimarisha na kuongeza uwekezaji kwenye sekta hiyo," alisema .

Abeid anaongeza kuwa kutokana na kukosekana kwa maghala makubwa ya uhifadhi gharama za meli zinazokaa nje ya bandari kusubiri kutia nanga kusubiri upakuaji ni kati ya dola za Marekali 20,000 mpaka 22,000 zaidi ya Shilingi milioni 50 kwa kwa siku ambapo meli moja inaweza kusubiri kwa zaidi ya siku 30.

Anafafanua kuwa hali hiyo inasababisha kutoonekana kwa unafuu wa gharama za mafuta licha ya serikali kuweka punguzo la kuondoa shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta inayouzwa hapa nchini.

Aidha, wafanyabiashara wa vyakula wanasema mpaka sasa bado gharama za usafirishaji wa mazao mbalimbali kutoka shambani mpaka kufika sokoni zipo juu, iwapo bei hizo zitashuka itasaidia kuondoa mfumuko wa bei.

Joyce Mkonyi mmoja wa wafanyabiashara anasema: "Sisi pia tunaumia sana na hatupendi kupandisha bei za vyakula lakini ukiangalia gharama za usafirishaji zilivyo kubwa hakuna namna lazima na wewe upandishe kidogo ili ufidie angalau kupunguza maumivu ya hasara tunayopata,vita imetuletea janga kubwa sana na kupandisha gharama za maisha."

Mapema hivi karibuni Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky amezitolea wito nchi tajiri duniani za kundi la G7 kuipatia nchi yake gesi ya ziada pamoja na silaha ili kuisadia nchi hiyo kujinusuru na baridi kali ya msimu ambayo inatishia kusababisha mateso zaidi kwa mamilioni ya raia walioko kwenye nchi hiyo inayokabiliwa na mashambulizi ya Urusi.

Rais Zelensky akizungumza na viongozi wa nchi tajiri kiviwanda duniani za kundi la G7 Disemba 13 mwaka jana anasema nchi yake inahitaji mita za ujazo bilioni mbili za gesi ya ziada itakayowasaidia katika kipindi hiki cha baridi kali.

"Nawatolea wito muongeze msaada kwa ajili ya Ukraine katika suala la gesi. Ugaidi dhidi ya mitambo yetu ya umeme umetufanya tutumie kiasi kikubwa cha gesi kuliko tulivyotarajia. Na ndio sababu tunahitaji msaada zaidi katika kipindi hiki cha baridi. Tunazungumzia kiasi mita za ujazo bilioni 2 za gesi,ambazo zinahitaji kununuliwa ziada",alinukuliwa akisema.

Kadhalika viongozi wa kundi la G7 wamekubaliana kuhusu maeneo muhimu ya kushirikiana katika msaada wa fedha kwa ajili ya Ukraine, kwa mujibu wa Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz ambaye ameyasema hayo kabla ya mkutano wa kilele wa wafadhili wa kimataifa wa kusaidia ujenzi mpya wa Ukraine. Mkutano wa Paris unatarajiwa kuchangisha mabilioni ya dola kwa ajili ya kuwasaidia raia wa Ukraine kukabiliana na msimu wa baridi kali.

Scholz analiambia bunge la Ujerumani kuwa Umoja wa Ulaya (EU) unaungana kwa dhati kuisaidia Ukraine, na kuongeza kuwa jaribio lolote la kudhoofisha maadili ya EU kwa kuzuia sera za mambo ya nje na usalama halitafanikiwa.

Kiongozi huyo wa Ujerumani ameongeza kuwa Rais wa Urusi, Vladimir Putin amepiga hesabu zake vibaya katika vita hivyo kwa kuamini kuwa wanajeshi wake wangeisambaratisha Ukraine ndani ya siku chache na kudhani kwamba mataifa ya Magharibi na washirika wake walikuwa wamegawanyika sana kiasi cha kushindwa kuisaidia Ukraine.

# UN yagundua upya mbinu za Rwanda kusaidia waasi M23

## •DRC yatamani jirani huyo awekewe vikwazo kiuchumi



Migogoro ya kivita imeangamiza maisha na mali nchini DRC. **PICHA: REUTERS**

**Na Gaudensia Mngumi**

UMOJA wa Ulaya (EU) umetuma salamu za mwaka mpya kwa Rwanda, ikiitaka kuacha kuwaunga mkono waasi wa M23 nchini DR Congo.

Maoni ya Umoja wa Ulaya yanakuja baada ya ripoti ya wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN) kuthibitisha kuwa kuna uingiliaji wa moja kwa moja na vikosi vya Rwanda ndani ya DR Congo.

Umoja wa Ulaya umeitaka Rwanda kuacha kuunga mkono kundi la waasi la M23, ambalo hadi mwaka unakwisha limeteka maeneo mengi katika jimbo la Kivu Kaskazini nchini DRC.

DRC pamoja na Marekani na nchi kadhaa za Ulaya mara kwa mara imekuwa ikishutumu jirani yake japo ni nchi ndogo kwa kuwaunga mkono M23, ingawa Kigali inakanusha mashtaka hayo na kusisitiza kuwa ni tatizo la Wakongo wenyewe, lakini sasa UN imepata ushahidi unaoongeza nguvu.

Hadi mwaka unapomalizika kundi la waasi la Kitutsi au Machi23 lilikuwa limesonga mbele hadi ndani ya kilomita kadhaa kutoka mji mkuu wa Kivu Kaskazini wa Goma, ambao ni kitovu cha biashara.

Akitoa salama za kuionya Rwanda, Mkuu wa Sera za Mambo ya Nje wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrell, anaisema EU imeitaka Rwanda "ikome'kuunga mkono M23 na kutumia njia zote kushinikiza M23 kufuata maamuzi yaliyochukuliwa na EAC Jumuiya ya Afrika Mashariki" na yale yaliyokubaliwa katika mkutano wa kilele wa Novemba mwaka jana huko Angola.

"Pia inahimiza kwa uthabiti mataifa yote ya eneo hilo kuzuia utoaji wa msaada wowote kwa makundi yenye silaha yanayofanya kazi nchini DRC," anasema Borrell.

Anatoa wito kwa Kinshasa "kuchukua hatua zote muhimu kulinda raia katika eneo lake.

Chini ya shinikizo kubwa la kimataifa la kupokonya silaha, M23 ilijiunga na sherehe wiki iliyopita kuwasilisha mji wa kimkakati wa Kibumba kwa jeshi la Afrika Mashariki kama "ishara ya nia njema" ya kufikiwa kwa amani.

> "Pia inahimiza kwa uthabiti mataifa yote ya eneo hilo kuzuia utoaji wa msaada wowote kwa makundi yenye silaha yanayofanya kazi nchini DRC," anasema Borrell.

Lakini pia EAC ilisema kundi hilo lililazimika kujiondoa kwenye mpaka kati ya DRC, Uganda na Rwanda, hata hivyo, jeshi la Kongo mara moja liliita makabidhiano ya Kibumba kama ya kiudanganyifu au kejeli.

Maoni ya Mkuu wa Sera za Mambo ya Nje wa EU, Borrell yanakuja baada ya ripoti ya wataalamu wa Umoja wa Mataifa kuhusu DRC kueleza kuwa imekusanya uthibitisho unaoonyesha kuingilia moja kwa moja kwa vikosi vya ulinzi vya Rwanda ndani ya ardhi ya DRC kati ya Novemba 2021 na Oktoba 2022 na kuhusika na shughuli za M23.

Ripoti ya UN inasema wanajeshi wa Rwanda walianzisha operesheni za kuimarisha M23 dhidi ya Wahutu wanaojiita FDLR hasa kwa kusambaza silaha, risasi na sare na mahitaji muhimu.

Serikali ya Rwanda inaona FDLR kama tishio ambalo linahalalisha majeshi ya nchi hiyo kuingilia kati ndani ya DRC ili kulifurusha.

Katika hatua nyingine Rwanda pia inaishutumu DRC ambako uchaguzi wa rais unatarajiwa kufanyika Desemba mwaka huu ikisema inautumia mzozo huo kwa madhumuni ya kujinufaisha kisiasa na kutengeneza habari za uzushi kuhusu mauaji ya raia 131, Novemba mwaka jana ili kujipatia mtaji wa kisiasa.

.Kabla ya mauaji hayo, Angola ilikuwa ikifanya upatanishi katika mazungumzo ya amani yaliyopangwa kuweka njia ya makubaliano ya kusitisha mapigano.

Katika taarifa yake ya mwisho wa mwaka DRC ilikaribisha matokeo ya wataalam wa Umoja wa Mataifa, ambayo inasema ni kukomesha uwongo na udanganyifu wa Rwanda, uliodumu kwa muda mrefu.

Kwa kuzingatia uzito wa mambo yaliyofichuliwa inalitaka Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuchunguza ripoti ya wataalam kwa lengo la uwezekano wa kuiwekea vikwazo dhidi ya Rwanda.

**KAGAME ALIANZISHA**

Wakati huo huo, Rais wa Rwanda Paul Kagame, anailaumu Kinshasa kwa machafuko katika maeneo yake ya mashariki yenye hali tete katika hotuba yake ya kuukaribisha mwaka mpya, akisema licha ya juhudi za kuweka amani kinachoonekana ni hasara zaidi..

"Baada ya kutumia mabilioni ya dola katika ulinzi wa amani katika miongo miwili iliyopita, hali ya usalama Mashariki mwa Kongo ni mbaya zaidi kuliko hapo awali," Kagame anasema katika taarifa yake Jumamosi Desemba 31.

"Ili kuelezea kushindwa huko, baadhi ya viongozi wa jumuiya ya kimataifa wanailaumu Rwanda, ingawa wanajua vyema kwamba jukumu la kweli ni la serikali ya DRC. Ni wakati mwafaka sasa udhalilishaji usio na msingi wa Rwanda ukomeshwe." Anasema Kagame.

Mwezi uliopita EU iliweka vikwazo kwa mfanyabiashara wa Ubelgiji, waasi wa M23 na wengine kutokana na mapigano ya DRC na katika orodha hiyo m, watu wanane waliongezwa kwenye orodha ya vikwazo, wakiwemo waasi, mwanasiasa, mwanajeshi na mfanyabiashara wa kigeni.

Watu 17 sasa wako chini ya vikwazo vya EU hadi Desemba 2023, ambayo inajumuisha marufuku ya kusafirisha na kufungia mali zao, Baraza la EU linasema katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, mwishoni mwa mwaka jana..

Watu wanane walioorodheshwa hivi karibuni ni pamoja na wanachama watano wa makundi yenye silaha ya ADF, CODECO, FDLR, Mai-Mai Yakatumba na M23 na mwanajeshi la Kongo, mwanasiasa wa nchi hiyo na mfanyabiashara wa Ubelgiji.

"Wengi wao wanawajibishwa kutokana na ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na kuendeleza vita nchini DRC.

Wengine wameorodheshwa kwa kuchochea ghasia na kutumia migogoro hiyo kupitia unyonyaji na uvunaji haramu na biashara haramu za maliasili za Congo," inasema EU katika taarifa hiyo ya katazo.

"Uamuzi wa leo umechukuliwa katika muktadha wa mbinu jumuishi ya EU katika kuunga mkono juhudi za mamlaka ya DRC kujenga amani ya kudumu na kuleta utulivu eneo la mashariki mwa nchi hiyo." Inaongeza EU.

***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa***

# Uchaguzi mikoa CCM ulivyowaacha kando kinamama, yupo mmoja pekee

## • Mshindi asema safari 50/50 ina mabonde, mbigiri si nyepesi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA Cha Mapinduzi kimemaliza uchaguzi wa kupata viongozi mbalimbali watakaoshika nyadhifa wanazopewa kwa muda wa miaka mitano huku nafasi nyeti za uongozi mbali na Mwenyekiti wa CCM Taifa , nyingi zimechukuliwa na wanaume. Na swali uwapi usawa wa kijinsia ndani ya uchaguzi CCM, likiibuka.

Kwa upande wa Visiwani Zanzibar kati ya mikoa sita kichama nafasi za uenyekiti kwa mikoa mitano zinashikiliwa na wanaume na mkoa wa Kusini pekee ndiyo unaoongozwa na mwanamama Mwaka Mrisho Abdallah.

Hali hiyo sio kwa nafasi za uenyekiti wa mikoa pekee hadi nafasi za uenyekiti wilaya 10 za CCM kichama nafasi hizo zimeshikiliwa na wanaume licha ya wanawake kujitokeza kugombea kuchaguliwa kushika majukumu hayo.

Wakati nchi inapigania usawa wa kijinsia katika ngazi mbalimbali ikiwamo nafasi za uongozi kichama na kiserikali bado wanawake hawajaaminiwa na kupewa fursa  na kufikia usawa wa kijinsia wa asilimia 50 kwa 50 hata ndani ya chama, anasema mshindi Mwaka Mrisho Abdallah.

Mwenyekiti huyo wa CCM pekee katika mikoa , Zanzibar anasema katika kinyang'anyiro cha uchaguzi aligombea na wanaume zaidi ya nane huku wanawake wakiwa wawili katika mkoa huo.

Mwaka anasema kati ya wagombea 12 majina yao yaliyopelekwa katika ngazi za juu za chama kwa ajili ya kupendekezwa, majina ya wagombea wanne yalipendekezwa likiwemo la kwake na kuwa mwanamke pekee kati ya hao ambao wanaingia katika mchakato wa kuomba kura.

Aidha, anakumbusha kuwa katika uchaguzi huo aliibuka na ushindi wa kishindo kwa kupata kura 159 sawa na asilimia 75 ambapo anayemfuatia alipata kura 69.

Mwenyekiti huyo anasema siri ya mafanikio ya kuibuka na ushindi huo ni kuwa karibu na wanachama wenzake, mapenzi kwa chama chake na ujasiri, lakini pia ukakamavu na upinaganaji au kuwa 'hustler'

Akiwa mwanajeshi mstaafu wa polisi, anasema ukakamavu na ujasiri wake unaompa nguvu umejengwa na kazi ya upolisi na baada ya kumaliza muda wake wa kulitumikia jeshi hilo mwaka 1915 ndipo alipoingia katika siasa.

Anasema hadi kufika kuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini haikua kazi rahisi na aliaza kugombea nafasi za uongozi tangu ngazi za chini za wadi ndani ya chama hicho na hatua kwa hatua akafikia hapo aliposasa.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja, Mwaka Mrisho Abdallah ,akisalimiana na Makamu Mwenyekiti mstaafu wa CCM,Dk. Ali Mohamed Shein, alipotembelea Mkoa wa Kusini Unguja.**Picha :RAHMA SULEIMAN**

Anaeleza kuwa licha ya kipindi cha nyuma kugombea nafasi za uongozi katika siasa na kutobahatika kuchaguliwa lakini hakukata tamaa wala kuvunjika moyo na amepambana hadi kupata nafasi hiyo ya uenyekiti.

"Siri na mafanikio yangu hadi kushinda katika nafasi hii ni kuwa karibu na wanachama, kujitolea kukitumikia chama, kuwa na mapenzi na chama pamoja na wanachama wenzangu"anasema Mwaka maarufu Mwaka Polisi.

Mwenyekiti huyo anasema ili kuongeza idadi ya wanawake katika uongozi ni vyema wanawake kujitoa tokea katika ngazi za chini ili wanapogombea nafasi za juu iwe rahisi kutambulika na uwezo wao kuonekana.

"Mimi nimekuwa kiongozi tangu nikiwa nalitumika taifa katika Jeshi la Polisi nimeshawahi kuwa mkuu wa kituo cha polisi Dunga Mkoa wa Kusini Unguja"anasema mwenyekiti huyo akitaja sababu zinazochangia wanawake kushindwa kupata nafasi za uongozi hasa za kugombea katika siasa.

Anasema kwanza ni uwezo mdogo wa kifedha kwa sababu wanawake wengi hali zao za kiuchumi ni duni ikilingnaishwa na wanaume na kwamba uchaguzi unahitaji fedha na bila ukwasi unaweza usifanikiwe.

Baadhi ya nafasi za uongozi zinazohitaji gharama mfano wa kupita kijiij hadi kijiji kuomba kura kwa wajumbe huku wengi wao wakitumia usafiri wa umma."Binafsi nimegombea nafasi hii nikiwa sina usafiri wangu binafsi imenilazimu nitembee vijiji vyote vya Mkoa wa Kusini Unguja kuomba kura kwa wajumbe wa chama na vijiji vingine hafiki gari za abiria hunilazimu kuchukua usafiri wa bodaboda,"anasema Mwaka.

### KEJELI ALIZOPATA

Mwaka anaeleza kuwa changamoto alizokumbana nazo ni maneno ya kukatishwa tamaa yanayotoka kwa baadhi ya wanachama na wananchi.

Mfano, alikwenda katika kijiji kimoja kuomba kura kwa wajumbe akitumia bodaboda jambo la kusikitisha wakati anaondoka mwananchi mmoja alimsikia akisema mgombea mwenyewe kaja kwa bodaboda kweli ataweza kuongoza? "

Anasema kauli kama hizo na nyingine ikiwemo ya kuambiwa badala ya kulea familia yake anagombea nafasi ya uongozi hazikumkatisha tamaa na zilimpa ujasiri zaidi wa kupambana na kushinda nafasi hiyo.

Mwaka pia ni miongoni mwa wagombea ubunge katika uchaguzi wa mwaka 2020 kupitia wazazi Mkoa wa Kusini Unguja lakini alishindwa na mpinzani wake kwa kura moja na kukwama kuwa mbunge.

Mwenyekiti huyo anasema, ndani ya Chama Cha Mapinduzi sio kikwazo kwa wanawake kuwa viongozi lakini tatizo lipo kwa jamii na wanawake wenyewe kutokuwa kitu kimoja, na wananchi hawana utayari wa kuwapa nafasi za kuongoza..

Anasema idadi ya wapiga kura wengi CCM ni wanawake, hivyo ushindi wake aliupata kwa nafasi hiyo imetokana na umoja na mshikamano kwa wanawake na wanaume kuwa kitu kimoja na kumuamini kuwa anaweza kuwaongoza.

Aidha, anawataka wanawake wenzake kutokata tamaa wala kurudi nyuma wanaposhindwa kupata nafasi za uongozi na badala yake kupambana kugombea kila wakati unapofika.

Hata hivyo, ana angalizo kwa washindi,akiwawashauri wale wote waliogombea nafasi za uongozi na kushinda katika ngazi mbalimbali wajitoe kwa wnaanchi kushiriki harakati za kijamii na sio kukaa ofisini pekee.

"Wananchi wanahitaji umoja na ukaribu wa viongozi wao,niwasihi viongozi wezangu tujitowe kwa jamii na tuwe nao karibu kwa hali na mali, kwa raha na shida"anasema.

Mwenyekiti huyo anakipongeza chama chake pamoja na wananchama wa chama hicho kwa kumuamini na kumpa nafasi hiyo ambapo ameahidi kukitumikia chama vizuri ili kufikia malengo ikiwamo ya kuendelea kushika dola katika chaguzi zijazo.

"Pia nisiwe mwizi a fadhili naishukuru familia yangu akiwemo mume wangu kwa kuniunga mkono katika harakati hizi za kugombea nafasi za uongozi kwa sababu baadhi ya muda hulazimika kuicha familia yangu kukitumikia chama,"anasema.

Mume wa Mwenyekiti huyo Daudi Ame Msimu, anasema kuwa wanawake wanajituma na wanapigania haki zao ikiwamo nafasi za uongozi ili kutoachwa nyuma.

Anawataka wanaume wezake kutowanyima fursa wake zao za kugombea nafasi za uongozi kwa sababu baadhi ya wanaume ni vikwazo kwa wanawake kuwa viongozi.

"Mimi mke wangu nimemruhusu na nimemuamini katika harakati zake zote za kisiasa na uongozi kwa sababu maendeleo hayaletwi na mwanaume pekee"anasema Mume huyo.

Bahati Issa Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa Tawi la CCM Kikungwi Mkoa wa Kusini Unguja, anasema wanawake wengi wamehamasika katika chama hicho kugombea nafasi mbalimbali za uongozi lakini waliopata ni wachache ikilinganishwa na wanaume.

Anautaja mfumo dume kuwa bado ni kikwazo kwa wanawake kupata nafasi nyingi za uongozi.

Anasema sababu nyingine ni waliopata nafasi za uongozi hawajawa tayari kuachia njia ili kuwapisha wengine na hatimae kuendelea kugombea nafasi hizo hasa kwa zile ambazo hazina ukomo wa kuongoza.

### WALIOSHINDWA WAZUNGUMZA

Mariyam Omar Ali aliyegombea nafasi ya uenyekiti wilaya ya Micheweni Pemba anasema kushindwa kufanikiwa kwenye kinyanganyro hicho siyo kwamba hana uwezo lakini kura hazikutosha.

Anasema bado hajakata tamaa na anaunga mkono wote waliofanikiwa  na anaamini kuwa kilichoshinda ni chama na sio wao, akiwataka wanawake waliogombea nafasi za uongozi na kushindwa wasivunjike moyo na wajipange kwa uchaguzi ujao ili kufikia ndoto zao.

# Peru; nchi isiyotawalika, ina 'bunge matata' humuondoa rais lipendavyo

## •Yupo aliyeongoza siku sita, akatumbuliwa



Rais wa sasa Dina Boluarte



Jose Pedro Castillo alianza Julai 28, 2021 hadi Desemba 7, 2022 yuko gerezani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Pedro Pablo Kuczynski, PPK 2016 hadi 2018.



Manuel Arturo Merino de Lama, aliongoza siku sita, Novemba 10 hadi 15, 2020.

**Na Mwandishi Wetu**

PERU ni taifa lililo Bara la Amerika Kusini au Latino , ni taifa lisiloongozeka likitajwa kuwa limekuwa na marais sita ndani ya miaka minne na kuhoji kwanini nchi hiyo ni vigumu kuiongoza? Swali linaulizwa na makala ya BBC Swahili, muda mfupi baada ya aliyekuwa rais wa Peru Pedro Castillo, kutumbuliwa Desemba mwaka jana.

Pedro Castillo alikuwa rais wa mwisho kuondolewa, lakini yeye na watangulizi wake wanne wanagawana muda mfupi walioongoza nchi kwa kukaa madarakani kwa muda mfupi na kutumbuliwa wala si kung'atuka . Mrithi wake ni Dina Boluarte aliyeapishwa hivi karibuni, tena anakuwa rais wa kwanza mwanamke katika historia ya Peru, lakini pia kiongozi wa sita wa taifa hilo la Peru tangu 2018.

Marais watangulizi ni pamoja na Pedro Pablo Kuczynski, Martin Vizcarra, Manuel Merino, Francisco Sagasti, Pedro Castillo na Dina Boluarte.

Hali ya hatari ni kwamba watu wengi wa Peru wamezoea kuishi nje ya siasa na misukosuko yake ya kudumu na kuondoa marais kila wakati bila kujali, kwa kutumia maandamano ya umma.

Maandamano ni silaha na hivi karibuni Desemba mwaka jana rais mpya wa Peru Dina Boluarte, anawataka raia wa nchi hiyo kuwa watulivu na kuonyesha nia ya kuandaa uchaguzi mkuu katika muda wa mwaka mmoja. Ni baada ya maandamano ya kutaka uchaguzi mkuu kufanyika mara moja kumchagua rais na wabunge wakimpinga mrithi wa Castilo.

Rais wa zamani Castillo amewekwa gerezani huku maofisa wakitayarisha kesi ya mapinduzi dhidi yake. Waziri wa ulinzi, Luis Otarola Penaranda ametangaza kwamba polisi wa kitaifa na jeshi la nchi hiyo watahakikisha kwamba kuna hali ya utulivu na kulinda mali ya umma kote nchini humo.

Castillo aliondolewa madarakani Desemba 7 alipojaribu kuvunja bunge lililokuwa linatayarisha mswaada wa kupiga kura ya kutokuwa na imani naye. Kiongozi huyo alikamatwa katika barabara za Lima akiwa pamoja na walinzi wake, na waendesha mashtaka wanasema alikuwa anajaribu kutorokea nchini Mexico.

**KWANINI HAWATAWALIKI**

Swali jingine ni hili , lakini ni nini kinachoifanya Peru isiongozeke? Hali ya wasiwasi inayoendelea bungeni inajirudia katika miaka ya hivi karibuni. Vita vya kudumu kati ya bunge au congress na rais huisha na kushindwa kwa rais, ambaye anaishia kuondoka madarakani. Castillo alikuwa wa mwisho kuteseka.

Katika jaribio la wazi la kusimamisha kura ya hoja ya nafasi iliyo wazi dhidi yake katika Congress, alitangaza kwa kushangaza kuvunjwa kwa bunge na kuundwa kwa serikali ya dharura, bunge likilenga kutokuwa na imani naye.

**KATIBA NGUMU**

Saa chache baadaye kwa kupuuza tangazo la rais, wabunge walikutana na kumuondoa rais, ambaye aliachwa mikononi mwa polisi na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, akishutumiwa kwa uasi. Hali hiyo inatokana na Katiba ya Kisiasa ya Peru, iliyoidhinishwa mwaka wa 1993, ambayo inathibitisha kuwa urais wa nchi unabaki wazi kutokana na "kutoweza kuhudumu kwa maadili au kimwili, iliyotangazwa na congress au bunge" .

Hii imefungua mlango kwa nafasi hiyo kuwa aina ya upanga ambao unaning'inia juu ya kichwa cha rais na ambao unaweza kumwangukia mara tu kura 87 zinazohitajika zitakapokusanywa bungeni.

Hivi ndivyo ilivyotokea kwa Castillo, Vizcarra mnamo 2020 na wakati Alberto Fujimori alipokimbilia Japan mnamo 2000 bunge au congress likalazimika kutangaza kuondolewa madarakani.

Wataalamu wanasema upekee huu wa kikatiba unaeleza kwa nini marais wa Peru wana nafasi dhaifu zaidi.

Wabunge waliofuatana wamegundua kuwa utaratibu wa nafasi hiyo unawapa uwezekano wa kumkabili rais na hawajasita kuutumia.

Hadi imefikia wakati ambapo wataalamu wanaeleza kuwa maana ya asili ya sheria hiyo imepotoshwa.

**NI KAMA WEHU**

Omar Cairo, Profesa wa Sheria na Katiba katika Chuo Kikuu cha Kipapa cha Kikatoliki cha Peru, anaiambia BBC Mundo, kuwa "Peru ndiyo nchi pekee duniani ambayo ina taasisi ya nafasi ya watu wasio na maadili. Lakini ukosefu wa maadili, ambao uko kwenye katiba za Peru tangu 1839, inadai kutokuwa na uwezo wa kiakili wa rais".

"Sasa wakati wowote wabunge wanaona rais hana maadili, wanaweza kumuondoa kwa hiari yao kwa nguvu ya kura tu, na neno hilo lisilo la maadili ni jambo la kipuuzi sana siku hizi."

Na hili linaongeza mgawanyiko unaopatikana ndani ya vikundi vya kisiasa vya Peru katika miaka ya hivi karibuni.

Cairo anaeleza kuwa "bunge halijumuishi kambi imara za bunge, bali ni wingi wa makundi madogo yanayojibu zaidi maslahi fulani kuliko mipango au itikadi, na hii inafanya kuwa vigumu sana kwa marais kupata uungwaji mkono katika congress."

Kwa njia hii, taifa la Peru limekuwa adimu kwenye ramani ya mifumo ya kisiasa ya Amerika Kusini, ambapo tawala za mihula ya urais zinatawala.

"Peru sio utawala wa kibunge kama Waingereza au Wahispania, ambapo waziri mkuu au rais wa Serikali anachaguliwa na manaibu bungeni, bali rais anachaguliwa moja kwa moja na kura za wananchi."Kuwepo kwa nafasi hiyo kumeruhusu utaratibu wa hiari wa kumwondoa madarakani rais, sheria ambayo haipo katika nchi nyingine za ukanda wetu"

**KAA CHONJO**

Hata Rais Dina Boluarte, anatakiwa kukaa chonjo na bunge. Rais huyo anaanza muhula akitaka maridhiano katika bunge la Congres na kujenga serikali ya umoja.

Lakini,ikitokea idadi kubwa ya wabunge wamepiga kura ya kumuondoa Castillo na kumfanya kuwa rais mpya sio kwamba atapata uungwaji mkono kuanza serikali thabiti.

Hata Dina hana wabunge wanaomuunga mkono katika bunge, uongozi wake huenda ukakabiliwa na matatizo kama hayo ya Castillo.

Huku sheria ikiendelea kutumika, ni wazi kwamba pia yeye huenda atakabiliwa na meno au upanga wa bunge kumuondoa ikulu.

***Kwa mujibu wa taarifa kimataifa***

JUKWAA LA VIONGOZI

DONALD TRUMP

# Ana 'jambo lake' ni Ikulu tena 2023, adaiwa kuwa mfupa mgumu hazuiliki

**Na Ani Jozeni**

DONALD TRUMP, anamalizia mwaka 2022 akiwa ana jambo lake, ametangaza azma yake ya kuwania urais kwa mara ya tatu, licha ya kuwa kiongozi wa zamani wa Marekani, kutia nia ya kutaka kuingia tena Ikulu ya White House baada ya kushindwa katika uchaguzi.

Pamoja na mkakati huo ripoti ya kuhusika na uvamizi dhidi ya kikao cha Senate kuthibitisha matokeo ya uchaguzi wa urais 2020 nchini Marekani, imetoka na kuweka wazi kuhusika kwake.

Baada ya kamati maalum ya Baraza la Wawakilishi kufikia uamuzi wenye ushahidi mwingi kuwa rais aliyepita Donald Trump alichochea na kuandaa uvamizi wa jengo la Bunge la Marekani - Capitol Hill - kuzuia kutangazwa rasmi na Baraza la Senate matokeo ya uchaguzi wa urais Januari 6 mwaka jana, ugumu sasa unaanza. Nani atakayemvisha paka kengele ndilo swali; vyama vikuu vya siasa vya Democratic na Republican vinajiuliza kupitisha sheria asigombee tena.

Kielelezo kimojawapo cha ugumu wa suala hilo ni uchunguzi kuhusu suala hilo hadi kutolewa taarifa ya kina yenye kurasa 800 na ziada, na kuwasilishwa maelezo hayo bungeni imechukua takriban miaka miwili. Kwa kalenda ya uchaguzi nchini humo, kila miaka miwili Baraza la Wawakilishi linachaguliwa upya, na miaka minne ni uchaguzi wa rais ukiendana na theluthi ya Bunge ambayo ni miaka miwili kwani maseneta wanatumikia miaka sita muhula mmoja.

Katika uchaguzi wa mwezi Septemba wa Baraza la Wawakilishi, chama cha Republican kimerudisha Baraza la Wawakilishi;Democratic wanaendelea kushikilia Baraza la Senate.

Ni mazingira haya mapya Baraza la Wawakilishi yanayoleta utata katika suala la kushughulikia ripoti hiyo, hasa kwa maeneo mawili, la kwanza ni rai kuwa rais huyo wa zamanai ashtakiwe kwa kosa la jinai la kuchochea uasi, kutaka kuzuia kikao rasmi cha Baraza la Senate kwa shughuli muhimu ya kikatiba.

Aidha, la pili ni kujadili, kupiga kura na kupitisha pendekezo kuwa Trump avuliwe rasmi haki yake ya kiraia, ya kugombea uongozi katika ngazi yoyote, ikiwamo ya urais. Mfano hai ni kuwa wakati akichochea uasi, maandamano na uvamizi dhidi ya Bunge la Marekani, ukurasa wake wa twitter ulifungwa; hivi majuzi bilionea Elon Musk, rafiki yake, ameinunua twitter na sasa Trump anaandika.

Katika kampeni za kupata wagombea wa Republican kwa viti vya ubunge kote nchini kuanzia mwanzo wa mwaka hadi katikati ya mwaka jana, ilionekana wazi kuwa wafuasi wake walikuwa wana uhakika zaidi wa kuungwa mkono na wanachama wa Republican zaidi ya wanaomkosoa hasa kwa kuchochea uvamizi huo wa jengo la bunge, kudhihirisha kutokuwa na imani ya kutosha na mfumo wa siasa nchini humo.



Ni kulazimisha ushindi, jambo ambalo raia wa Marekani wameaminishwa kuwa ni tabia za watawala wa Afrika, Asia na Amerika ya Kusini, na siyo Ulaya au Amerika ya Kaskazini, ilipo Marekani.

Mtihani wa kwanza uko hapo, kuwa kamati maalun ya bunge inayoshughulika na masuala ya sheria, imejitahidi kutoa taarifa yake na mapendekezo kabla ya Januari 6, mwaka jana muda ambako wanabadilishana madaraka Baraza la Wawakilishi. Baraza la Senate halina mabadiliko yoyote ila kwa upande wa uongozi wa kundi la Republican watakaochagua kiongozi mwingine.

Katika Baraza la Wawakilishi ni spika mpya anayechaguliwa kutoka kundi la Republican. Itafurahisha kuona kama spika huyo na Republican wakiwa wengi zaidi watafuata mapendekezo ya kamati hiyo na kupitisha maazimio hayo.

Baraza la Seneti ndiyo lenye mamlaka zaidi katika kusimamia utawala, kwa mfano kupitisha uteuzi wa rais.Seneti inachaguliwa kwa mafungu, theluthi moja kila uchaguzi hadi mzunguko mzima kwani wajumbe wa baraza hilo wana vipindi vya miaka sita.

Baraza la Wawakilishi husimamia shughuli za kila siku za utawala, kuangalia na kupitisha vifungu vya bajeti ya rais aliyeko madarakani, na zipo kanuni za miswada kuandaliwa na wajumbe angalau wa pande mbili wa Democrats na Republicans. Wajumbe wa baraza hili wana vipindi vya miaka miwili na kila uchaguzi unapofika viti vyao hugombewa upya, na hakuna kikomo.

Siyo jambo lenye uhakika, ushawishi wa kutosha kwani siasa za mrengo mkali wa kulia zinaongezeka, si kupungua. Moja ya vianzio vinavyoweza kuleta nguvu upya kwa upande wa wafuasi wa Trump na Republican kwa jumla ni wimbi la wahamiaji wasio na hati za kusafiria au ruhusa ya kuingia nchini humo, wanaopitia njia za panya na kutafuta vipenyo katika kuta na seng'enge zao katika mpaka wa Marekani na Mexico.

Mahakama moja ya rufani ilitoa amri ya kuondoa amri ya kurudishwa makwao bila hitaji la amri ya mahakama, yaani kwa kufunguliwa kesi, kwa wahamiaji wote wa aina hiyo. Ila wapo wengi wanaotaka wahamiaji waingie ili wapatikane wafanyazi shambani na viwandani kwa gharama ndogo, wimbi la kudai mishahara mikubwa lisijevuka mpaka.

Kati ya hisia mbili, ile ya wafuasi wa Trump ya kurudisha Marekani kwa raia wake wa awali siyo wao asili, na hii ya kutaka faida ya wafanyakazi au vibarua kufanyakazi kwa unafuu na soko kubwa zaidi la bidhaa nchini humo, au hata vipaji kutoka kwa wahamiaji, bado kuna mchuano mkali.

Marekani imeundwa kwa sehemu kubwa na wahamiaji katika karne kadhaa na hasa iliyopita, lakini wanapitishwa katika tanuru la kihisia na kufikia utii kwa mojawapo kati ya mielekeo mikuu ya kijamii, uliberali au uhafidhina.

Uliberali ni pamoja na 'ruksa' ya kutoa mimba na 'ndoa za mashoga,' wakati uhafidhina ni pamoja na kuchukia uhamiaji holela kwa kuhofia unahatarisha tunu za jadi za Marekani, inaanza kuzorota au kuparaganyika kihisia. Kuyumba kwa demokrasia baada ya uchaguzi mkuu 2020 ni kielelezo cha kuchoshwa na uliberali, kuifanya Marekani iwe vyovyote vile.

# Ndivyo Samia Suluhu Hassan anavyoakisi 'suluhu' ya kisiasa

INATOKA UK. 13

ni kuja kutangaza, lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara sasa linaondoka', anasema na kushangiliwa.

Itakumbukwa kuwa mikutano hiyo iliondolewa muda mfupi baada ya kuingia ikulu rais wa awamu ya tano, John Magufuli mwaka 2015.

"Lakini ndugu zangu tuna wajibu, wajibu wetu serikali ni kulinda mikutano ya vyama vya siasa, wajibu wenu vyama vya siasa ni kufuata sheria na kanuni zinavyosema', twendeni tukafanye siasa za kistaarabu, tukafanye siasa za kupevuka, tukafanyeni siasa za kujenga sio za kubomoa, si kurudi nyuma hapa tulipofika, 'sisi ndani ya CCM tunaamini katika kukosolewa na kujikosoa', anasema.

**SAMIA ALIDHAMIRIA**

Dhamira ya suluhu, ilionekana baada ya Rais Samia kuingia madarakani 2021, kufuatia kifo cha Magufuli, akionyesha dhamira ya kuleta maridhiano kwa kuunda kikosi kazi cha kukusanya maoni.

'Wakati mnanikabidhi kuongoza nchi hii, busara zilinituma kwamba jinsi nilivyolipokea taifa hili, kuna haja ya kulifanya liwe kitu kimoja, wote tuzungumze lugha moja," anasema na kuongeza:

"Ili taifa liwe moja, lazima tuwe na maridhiano, nikasema kwanza tuwe na mazungumzo kwenye vyama vya siasa.Kikosi kazi kilichoundwa kilileta maoni kwenye maeneo tisa. Makubwa matatu yaliyojitokeza ni kutaka kuruhusiwa kwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, mchakato wa katiba mpya na marekebisho sheria mbalimbali."



Baadhi ya viongozi wakuu wa vyama vya siasa wakimsikiliza Rais Samia Ikulu jana. **PICHA: IKULU**

Wanasiasa, akiwemo Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe , Mwenyekiti CHADEMA Freeman Mbowe ni miongoni mwa viongozi walioshiriki mkutano na Rais.

Kabwe akizungumza kuhusu uamuzi wa huo wa Rais kukwamua mchakato wa katiba na kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa anasema ni hatua kubwa na kwamba wana furaha.

Mbali na Makamu wa Rais Dk.Phillip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mkutano huo wa Rais na vyama vya siasa uliofanyika Ikulu, Jijini Dar es Salaam, ulihudhuriwa na viongozi wa vyama 19 vya siasa vyenye usajili wa kudumu.

Rais anahimiza kuwapo na maridhiano na wanasiasa kukubali kukaa kama Watanzania kwa ajili ya mustakabali wa kujenga nchi.

"Tuendelee kukaa kujadili kuhusu hatma ya nchi yetu. Tufanye mabadiliko yanayoonekana kwa kuzingatia katiba, mila na desturi na sharia. Kwa kuzingatia uwezo wa wetu wa kiuchumi." Anasisitiza.

**CHA KUJIFUNZA**

Katika maelekezo hayo ya Rais Watanzania wanajifunza kuwa ili kufikia taifa lenye umoja , upendano na kuheshimiana miongoni mwa serikali, wanasiasa na vyama au asasi za wananchi (NGOs) pamoja na vyombo vya habari , uvumilivu na kuchukuliana ni suala lisilokwepeka.

Kuwapo kwa mvutano kunakochangiwana tofauti za mitazamo, hoja, fikra na maoni miongoni mwa wanachama na viongozi wao na hilo ni jambo la kawaida kwenye uwanja wa siasa hivyo ni lazima kuwepo na maridhiano.

***Imeandaliwa na Moshi Lusonzo na Gaudensia Mngumi***


---

Dondoo: Kulia
1. nchi ambayo ni mkulima mkubwa wa mahindi duniani
6. pengine
7. hali ya mtu kuwa mchafu baada ya kufanya ngono
10.kujiunga na kikundi fulani
11.mwanasiasa mashuhuri Kenya
12.Jiji kubwa kusini mwa Uturuki
14.dhamira
16.mojawapo ya madude makubwa angani yanayozunguka jua

Chini:
1. watu wa karibu
2. tunu
3. chokaa ya kupaka nyumba
4. sema kwa heri
5. japokuwa
8. ahali
9. halafu, mwishowe
13.kitaya
15.kanya

## CHEMSHABONGO NA -00 39 00-


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MUNGU
MBUNI
NYUMA
UZIMA
AMBONI
ZUMA
UJUZI
ZAKARIA
MAMBO
ISAKA
SANAAN
NJAA, AMUA,
WASIKIVU, NIA

maoni SMS: 0787 00 97 94




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | O | M | A | | B | A | A |
| A | D | A | M | U | | N | |
| T | A | K | A | | O | G | A |
| A | | A | N | A | S | A | |
| | M | Z | I | M | A | | |
| U | Z | I | | I | M | B | A |
| | I | | | N | A | A | M |
| I | M | A | N | I | | S | I |
| | U | | | | | I | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| P | A | N | G | A | | T | |
| A | G | A | | J | A | A | |
| P | O | M | B | E | | P | |
| A | | B | O | N | D | E | |
| | M | A | N | D | E | L | A |
| | B | | D | A | R | I | |
| K | E | T | E | | E | | S |
| | G | | | | V | A | A |
| T | E | M | B | E | A | | A |



## Wakazi wa Rungwe sasa wageukia vanilla

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANANCHI wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wameanza kuchangamkia kilimo cha vanilla baada ya wataalamu wa kilimo cha zao hilo kutoa elimu na kugawa miche bora.

Aidha, wakulima hao wamehamasika baada ya kupata soko la uhakika la zao hilo ambalo linanunuliwa na Kampuni ya kizalendo ya Ney yenye makao makuu yake mkoani Kilimanjaro.

Wakizungumza juzi wakulima hao walisema awali walikuwa hawalijui zao hilo na walikuwa hawajui sehemu ambayo wangeweza kupata mbegu.

Mmoja wa wakulima hao, Mboka Mwakatumbula, mkazi wa Kijiji cha Kyimo, alisema walihamasishwa na kampuni inayonunua kuzalisha zao hilo na wakapewa mbegu za kisasa na elimu ya namna ya kuzalisha.

Alisema kwa sasa imefika miaka miwili tangu walipoanza kuzalisha zao hilo na baadhi ya wakulima walioitikia mapema kulima tayari wameshaanza kuvuna kiasi kidogo huku wengine wakitegemea kuanza mwaka huu.

"Zao hili ni rahisi sana kuzalisha hasa kwa huku kwetu, tunapanda kwenye migomba maana zao hili linahitaji sana kivuli, kazi ngumu huwa ni kuchavusha maana zao hili ni tofauti na mazao mengine hili lazima uchavushe mwenyewe kwa mikono," alisema Mwakatumbula.

Mtaalamu wa zao hilo, katika Wilaya ya Rungwe, Juma Mnzava, alisema vanilla inakubali kwenye eneo lolote lenye wastani wa nyuzi joto 25 mpaka 35 na mwinuko wa kati ya mita 100 mpaka 1,300 kutoka katika usawa wa bahari.

Pia alisema zao hilo linastawi kwenye eneo ambalo linapata wastani wa mililita 2,500 mpaka 5,000 za mvua kwa mwaka na kwamba sifa zote hizo ziko katika wilaya ya Rungwe.

Aliyataja maeneo ya wilaya ya Rungwe ambayo yanazalisha zao hilo kwa sasa kuwa ni Kata za Kyimo, Ikuti, Bagamoyo, Kinyala, Iponjola, Nkunga, Malindo, Suma, Masoko, Kisondela, Msasani, Makandana na Lufingo.

Alisema baadhi ya maeneo hayo yanafaa kulima zao hilo lakini bado wananchi hawajahamasika ipasavyo ndiyo maana bado hawajaanza kuzalisha.

# Wananchi wafurahia uchumi kuimarika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Kikondo, Kata ya Ilungu Wilaya ya Mbeya, wamesema uchumi wao umeanza kuimarika kwa kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara baada ya mgogoro baina yao na serikali kumalizika.

Wananchi hao walikuwa na mgogoro wa muda mrefu na serikali na walikuwa hawajulikani kama wako katika Mkoa wa Mbeya au Njombe.

Vilevile wananchi hao walikuwa na mgogoro wa mipaka kati yao na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo na kwa muda mrefu walikuwa wanatakiwa kuondoka katika eneo hilo ili kupisha shughuli za uhifadhi.

Sababu nyingine iliyokuwa inawafanya wananchi hao watakiwe kuondoka ni kuwa jirani na chanzo cha mito miwili ambayo ni chanzo cha Mto Ruaha na Mto Lufilyo ambayo na walikuwa wanaonekana kuwa wanahatarisha mito hiyo.

Hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, walifanya mkutano wa hadhara na wananchi wa kijiji hicho na kukubaliana waendelee kuishi katika eneo hilo kwa masharti ya kutoharibu mazingira.

Aidha, viongozi hao waliridhia wananchi hao watambulike kuwa ni wa upande wa Mkoa wa Mbeya jambo ambalo wananchi hao walikuwa wanalihitaji kwa muda mrefu.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wananchi hao walisema baada ya mgogoro wao kumalizika kwa sasa wanaishi kwa amani na utulivu na wanaendelea na shughuli zao za uzalishaji.

Mmoja wa wananchi hao, John Mpole, alisema awali walikuwa wanaamini kwamba maofisa wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) ndio waliokuwa wanasababisha serikali itake kuwaondoa na hivyo kuwachukiza.

Alisema kwa sasa baada ya maofisa hao kuwatetea na kubakishwa kwenye eneo hilo wanaishi nao vizuri na wanashirikiana katika masuala mbalimbali ya kijamii.

Kwa sasa, alisema wameanza kuimarika kiuchumi kwa kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ambayo hapo awali walikuwa wanaogopa kuyazalisha kwa wingi wakihofia kuondolewa na serikali.

"Sisi uchumi wetu hapa unategemea sana kilimo cha viazi, tulikuwa tunalima kiasi kidogo kwa sababu tulikuwa tunaogopa kutumia gharama kubwa halafu tuondolewe na kuyaacha hapa, sasa hivi kama unavyoona mashamba yote yaliyokuwa yanalala sasa hivi yamelimwa," alisema Mpole.

Naye Stella Seme alisema wamekubaliana kuhakikisha wanalinda vyanzo vya maji vilivyoko kwenye eneo lao ili viwasaidie wao na Watanzania wa maeneo mengine ambayo maji hayo yanaelekea.

Alisema kwa sasa wameshaweka alama maalumu zinazoonyesha mipaka ya maeneo yanayostahili kulimwa na yasiyostahili kwa ajili ya kulinda vyanzo vya maji na misitu iliyoko jirani na maeneo yao.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, Theodora Batiho, alisema uhusiano wa wahifadhi na wananchi wa kijiji hicho umeimarika hivi karibuni baada ya kuzungumza nao kupitia wazee wa mila.

Alisema kwa miaka ya nyuma walikuwa maadui na maofisa wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) walikuwa wanaogopa kupita kwenye kijiji hicho lakini kwa sasa wanashirikiana kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.



Wajasiriamali wakiendelea kuuza nyama jana kwenye machinjio ya Uyole jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC aagiza kasi usambazaji mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imeagiza mbolea zilizowasili mkoani hapa kusambazwa mapema kwa wakulima hasa maeneo ya vijijini ili kuwasaidia kuendana na msimu wa kilimo unaoendelea sasa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo juzi aliposhuhudia ushushaji wa shehena ya kwanza ya mbolea iliyozalishwa na kiwanda cha ndani ya nchi kilichoko mkoani Dodoma.

Aliiagiza Kampuni ya Ben Agro Star ambayo ni msambazaji mkuu wa mkoa wa mbolea hiyo kwa mkoa wa Mbeya kuhakikisha inasambaza katika halmashauri zote kwa usawa ili kuepusha migogoro ya wakulima na serikali.

Alisema mkoa kwa sasa unahitaji tani 11,000 za mbolea ili kukidhi mahitaji ya wakulima na hivyo akaiagiza kampuni hiyo kuongeza kasi ya usafirishaji wa bidhaa hiyo kutoka Dodoma na kuifikisha kwa wakulima.

"Mna kazi kubwa sana hapa mmeleta tani 30 pekee kwa hiyo natoa maelekezo, hakikisheni mnaongeza juhudi ya kuisafirisha mbolea hii kutoka Dodoma na kuileta hapa ili wakulima waipate kwa wakati," alisema Homera. Aliiagiza kampuni hiyo pamoja na wasambazaji kuhakikisha inasambaza mbolea hizo kwa bei iliyoelekezwa na serikali kwa maelekezo kuwa wakikiuka watachukuliwa hatua za kisheria.

Homera aliwataka wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kufuatilia hali ya upatikanaji wa bidhaa hiyo kwenye maduka yaliyosajiliwa na kutoa taarifa ya hali ilivyo na kufuatilia kujua kama wananchi wanauziwa kwa bei inayotakiwa.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Ben Agro Star, Dk. Israel Mwampondele, alisema shehena ya mbolea iliyowasili mkoani hapo ni ya utangulizi na shehena zingine ziko kwenye magari zinasafirishwa kutoka Dodoma kwenda Mbeya.

Alisema waliamua kupeleka mbolea hiyo baada ya kupata malalamiko ya uhaba wa bidhaa hiyo katika baadhi ya mikoa nchini ukiwamo Mkoa wa Mbeya ambao ni miongoni mwa mikoa inayozalisha mazao kwa wingi.

Alimhakikishia mkuu wa mkoa kuwa watasambaza mbolea hiyo katika maeneo yote ya mkoa huo na kwa bei elekezi ya serikali huku akisisitiza kuwa watawasimamia wasambazaji wao katika maeneo yote ili wasikiuke taratibu.

"Hizi mbolea zote zina ruzuku ya serikali kwa hiyo sisi tumeaminiwa kuisambaza, ni lazima tuhakikishe tunalinda imani hiyo tuliyopewa na serikali, tutazingatia taratibu zote ikiwamo kuuza kwa bei elekezi," alisema Dk. Mwampondele.

Hivi karibuni, yaliibuka malalamiko ya wakulima katika baadhi ya maeneo kuhusu kukosekana kwa mbolea jambo ambalo lilimlazimu Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kufanya ukaguzi maalumu.

Akiwa katika ziara hiyo ya kukagua bidhaa hiyo madukani, Dk. Tulia alishuhudia misururu mirefu ya wakulima wakisubiri kuhudumiwa huku wakidai kuwa mbolea hizo hazipatikani kirahisi jambo lililomlazimu kuwasiliana na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe akimtaka kushughulikia tatizo hilo.





# Msonde akunwa ujenzi vyumba madarasa

**Na Renatha Msungu,**
KONGWA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde, ameeleza kuridhishwa na ujenzi wa madarasa wilayani Kongwa mkoani hapo yatakayotumiwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza katika mwaka huu wa masomo.

Akiwa katika ziara ya kikazi kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa, Dk. Msonde alieleza kufurahishwa na halmashauri hiyo ilivyotumia fedha ilizopata kikamilifu kujenga shule mbili za sekondari kwenye maeneo ambayo wanafunzi walitembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Dk. Msonde alitembelea shule mbili za sekondari ambazo zimejengwa kwa fedha zilizotolewa na serikali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya kupokea wanafunzi wote walichaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari mwaka 2023.

Akiwa katika Shule ya Sekondari Ihanda, alikagua madarasa matano yaliyojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 100 yakiwa kwenye hatua za ukamilishaji tayari kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Pia alikagua shule mpya ya sekondari ya Masena ambayo imejengewa madarasa matano na iko tayari kupokea wanafunzi katika mwaka huu wa masomo.

Akizungumza katika ziara hiyo, Dk. Msonde alisema ameridhishwa na ujenzi wa madarasa ya shule hizo ambazo zitawapunguzia wanafunzi adha ya kutembea umbali mrefu kufuata.

"Nakumbuka wakati tumepata fedha hizi, viongozi wa Kongwa waliomba mjenge shule kutoka kwenye fedha tulizopewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na tukaridhia. Sasa leo (jana) nilikuja kuona hizo shule, kwa hakika nimeridhika na naridhia shule hizi kuanza mara moja," alisema Dk. Msonde.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remedius Emmanuel, alisema shule hizo zilishapangiwa wanafunzi na maandalizi mengine yote yamekamilika.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa fedha hizi pamoja na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kuridhia tuweze kuanzisha shule kwa fedha za madarasa tulizopewa.

"Shule hizi ni msaada mkubwa kwa wananchi wetu na kwa ile ya Ihanda itachukua wanafunzi kutoka vijiji vya Ihanda, Masinyeti na Vihingo na ile ya Masena itachukua wanafunzi toka Masena, Kilimani na Songambele," amesema mkuu huyo," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akipanda mti katika Hospitali ya Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma alipofika kwa ajili ya kutembelea miradi ya maendeleo wilayani humo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## DC apongeza mchango viongozi wa dini kitaifa

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Remidius Mwema, amesema serikali inatambua mchango mkubwa wa viongozi wa dini kwa kuwa mstari wa mbele kuliombea taifa na viongozi wake.

Mwema alisema hayo juzi baada ya kufanya mazungumzo na uongozi wa Kanisa la Moravian Tanzania wilayani Kongwa, mchungaji Wema Kibona, kuhusu masuala mbalimbali ya kidini na kijamii.

Alisema amejiwekea utaratibu wa kukutana na viongozi mbalimbali wa dini wilayani Kongwa na kuwashukuru kwa namna ambavyo wamekuwa mstari wa mbele kuliombea taifa na serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Mnafanya kazi kubwa. Serikali inatambua hilo. Ushirikiano mkubwa mnaoendelea kuonyesha matokeo yake ni pamoja na amani, upendo na utulivu katika wilaya yetu na taifa kwa ujumla. Mwendelee kutuunga mkono na kueleza umuhimu wa elimu hasa kukemea tabia za utoro wa wanafunzi maana maandiko matakatifu yanafundisha umuhimu wa elimu.

"Pia mtoe elimu kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira, maadili katika jamii zetu, kukemea vitendo vya ukatili, upendo miongoni mwetu pamoja na agenda zote za maendeleo. Wilaya ya Kongwa tunaahidi ushirikiano wakati wote," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Kanisa la Moravian Wilaya ya Kongwa, Mchungaji Kibona alisema wanapongeza utaratibu wa kiongozi huyo kwa kutambua na kutenga muda wa kukutana na viongozi mbalimbali wa kidini na kwamba kwa kufanya hivyo atadumisha upendo na mshikamano wilayani Kongwa.

# Wataka vituo vya watoto vimulikwe

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WATOTO wanaoishi katika mazingira magumu Kituo cha Shirika la Malezi Dodoma Makulu, jijini hapo wameiomba serikali kuviangalia kwa jicho la pili vituo hivyo kwa kuwa vilivyo vingi vinawanufaisha wamiliki badala ya walengwa.

Ushauri huo ulitolewa jana na mtoto Veisa Hassani (13) kwa niaba ya wenzake wa kituo hicho baada ya kukabidhiwa zawadi mbalimbali zilizotolewa na wahisani zikiwamo sare za shule, madaftari, kalamu na kadi za bima za afya.

Alisema kuwa vituo vilivyo vingi vipo kwa ajili ya kujinufaisha wahusika na si kama inavyokusudiwa, hivyo wanaiomba serikali kuvitupia macho kwa ajili ya ukaguzi zaidi na kuona kama vigezo vinavyotakiwa wanazingatia.

"Kuna vituo vingi misaada inapokuja watoto ambao ndiyo walengwa hupatiwa kidogo tofauti na wenyewe ambao huchukua kwa sehemu kubwa kwa kweli tunaiomba serikali kuvifanyia uchunguzi wa mara kwa mara na wakibainika wachukuliwe hatua za kisheria," alisema.

Pia watoto hao waliiomba serikali kuhakikisha vituo vinavyoanzishwa wamiliki wake wanafuata sheria ili waweze kupata vibari halali na siyo vya kitapeli na wakibainika wachukuliwe hatua zinazostahili ili kumlinda mtoto anayeishi katika mazingira magumu hatima yake ijulikane.

Naye Mkurugenzi wa Kituo hicho, Zawadi Mgeni, alisema ili kuondokana na uanzishwaji holela wa vituo vya kulelea watoto, maofisa maendeleo ya jamii wanatakiwa kuvitembelea na kufanya ukaguzi badala ya kusubiri kupelekewa taarifa wakiwa ofisini.

Alisema kero kubwa inayojitokeza ni kuwa baadhi ya maofisa maendeleo ya jamii hawana muda kuvitembelea na kuviangalia badala yake hukaa ofisini kusubiri nyaraka za uanzishaji wa vituo hivyo ambavyo havina vigezo vya kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Alisema vituo vingi vinaanzishwa lakini hakuna matokea yanayoonyesha kupunguza tatizo la kuwapo kwa watoto wa mitaani, kinyume chake tatizo hilo linaonekana kukua zaidi.

Katibu wa Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) Mkoa wa Dodoma, Richard Mabula, aliwataka Watanzania kujiwekea tabia ya kusaidia makundi mbalimbali yenye uhitaji ili waweze kujimudu katika kujikwamua na kero zinazowakabili.

Aliwaomba Watanzania kujiwekea utaratibu wa kuwasaidia watu wenye uhitaji wakiwamo watoto wanaoishi katika mazingira magumu, yatima, wajane na wazee wasiojiweza badala ya kusubiri mpaka kutokee matukio kama vile sikukuu.

"Tusisubiri mpaka matukio yatokee ndipo tuyakumbuke haya makundi yenye uhitaji bali tujijengee tabia ya kujitokeza mara kwa mara kusaidia. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunawawezesha kutatua baadhi ya changamoto wanazokabiliana nazo kwenye maisha yao ya kila siku," alisema.





## Watoa mbinu za kuboresha elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAENDELEO ya elimu mjumuisho Zanzibar yanaweza kufikiwa iwapo vikwazo vinavyoikabili sekta hiyo vitaondolewa na kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi.

Hayo yalisemwa jana na washiriki wa mkutano wa walimu wa vituo vya elimu mjumuisho Unguja uliofanyika katika ukumbi wa Kituo cha Walimu Kiembesamaki, Wilaya ya Magharibi B Unguja.

Kawthar Abdalla, Mwalimu wa Shule ya Kisiwandui, ambaye ni mmoja wa washiriki hao, alisema licha ya mafanikio yaliopatikana katika sekta hiyo, bado kuna haja ya kutatua vikwazo vilivyoko ikiwamo vifaa vya kufundishia.

Alisema vikwazo vingine ni muda wa ziada kwa wanafunzi wa vituo na mbinu mpya na utayari wa walimu wanaosomesha nje ya vituo.

"Bado baadhi ya walimu wanaosomesha madarasa ya nje ya vituo hawana utayari wa kuwasaidia wanafunzi hao hali inayowanyima fursa za kujifunza," alisema.

Akizungumzia changamoto za wanafunzi viziwi, Ofisa Elimu Mjumuisho wa Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Jide Khamis, alisema wanahitaji kupata vifaa na mbinu za kutosha ili kufanya vizuri katika masomo yao.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Juma Salum, alisema mkutano huo una lengo la kujadiliana na walimu ili kujua changamoto na mafanikio yanayozikabili elimu mjumuisho.

Mkutano huo umewajumuisha walimu wa vituo vya elimu mjumuisho vya Jang'ombe, Kisiwandui, Mwembemakumbi na Mwanakwerekwe H na F.

# Shein asema Mapinduzi yameongeza kasi maendeleo sekta utalii Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, amesema sekta ya utalii imefanyiwa mageuzi makubwa kwa sababu Zanzibar baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ilikuwa na hoteli mbili pekee.

Dk. Shein aliyasema hayo jana wakati akizindua hoteli mpya ya kitalii ya Toa hoteli yenye hadhi ya nyota tano huko Uroa Pongwe Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kabla ya Mapinduzi hayo, Zanzibar ilikuwa na hoteli moja na nyumba moja ya wageni kwa sababu harakati za kitalii hazikuwa kubwa wakati wa ukoloni.

Dk. Shein alizitaja hoteli hizo zilizokuwapo baada ya Mapinduzi hayo ni Afrika Hause na Hoteli ya Zanzibar lakini kwa sasa kuna hoteli nyingi na kwa Mkoa wa Kusini Unguja pekee kuna hoteli 347.

Alisema jambo hilo ni la kujivunia kwa Zanzibar na litoe kasi ya mabadiliko na mageuzi zaidi katika sekta ya utalii na serikali ina jukumu kubwa la kufanikisha kuongeza ujenzi wa hoteli nyingi zaidi.

Jitihada za kujenga hoteli baada ya Mapinduzi, alisema zilianza mwaka 1970 kwa kujenga hoteli ya Bwawani na hoteli tatu Pemba, hoteli ya Mkoani, Chakechake na Wete na ndipo harakati zikapamba moto kuukaribisha utalii.

Dk. Shein alisema, mwaka 2013 akiwa Rais wa Zanzibar, aliandaa mpango mkubwa wa utalii ulioitwa Utalii Kwa Wote ili kila mwananchi wa Zanzibar apate haki ya kupata tija, faraja na maendeleo kuhusu utalii.

Alisema baada ya hapo idadi ya watalii ikazidi kuongezeka kutoka mwaka 1986. Alisema mwaka huo watalii walikuwa 29,211 na hadi kufikia mwaka 2019, walifikia watalii 588,264.

"Lakini kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo maambukizi ya UVIKO-19, tulipata mtihani mkubwa sana. Idadi yetu ya watalii ilishuka sana kutoka watalii 538,000 hadi kufika 339,000 na mapato yetu ya utalii yalipungua sana. Tuliingika kwenye matatizo ya uchumi, nguvu za kuendesha serikali zikapungua lakini serikali ikajitahidi ili Zanzibar kupata afueni ya uchumi na kuimarisha uchumi wake," alisema.

Pia alisema hadi kufikia mwaka 2022, watalii walianza kuongezeka na hadi kufikia Oktoba, mwaka jana, watalii waliofika Zanzibar ni 425,908.

Alisema utalii ndiyo sekta mama ya uchumi wa Zanzibar, hivyo sekta zote kuhakikisha inaisaidia sekta hiyo na nchi zenye visiwa utalii ndio unaoimarisha uchumi wake.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwezekazji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, alisema wanapiga vita kitendo cha baadhi ya wawekezaji kuchukua ardhi kwa ajili ya uwekezaji bila kufanya lolote, hivyo serikali itawanyang'anya maeneo hayo.

Alisema mwenye mradi wa hoteli ya Poa, gharama kamili ni dola milioni 3.5 lakini hadi sasa washatumia dola milioni 2.7 sawa na asilimia 77 ya uwekezaji, hivyo wameruhusiwa kuendelea na uwekezaji.

Hoteli hiyo, alisema imetoa ajira 85 na kati ya hao watu sita ndio waliotoka nje ya nchi na ajira zote zimechukuliwa na wazawa.

Alisema katika ukanda huo wa Kusini Unguja kwa kipindi cha miaka miwili ijayo kutafurika hoteli nyingi zaidi, hivyo wale ambao wenye maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji ambayo hawayafanyii kazi serikali itawanyang'anya maeneo hayo na kupewa wengine walioyayari kuwekeza.

Pia aliwataka wananchi wa ukanda huo kusoma ili kupata ajira katika miradi ya uwekezaji katika ukanda huo ili ajira hizo zisichukuliwe na wageni.

Alisema serikali kupitia ZIPA ina mipango yake ikiwamo kuwa na sera na sheria mpya ya uwekezaji ambayo itakuwa rafiki katika kusimamia masuala ya uwekezaji katika hali ya kisasa ikiwamo huduma kwa kidigitali.

Naye Waziri wa Nchi, Kazi na Uwekezaji, Mudriki Ramadhan Soraga, alisema sekta ya uwekezaji iko katika hali nzuri na Zanzibar imefunguka katika nyanja za kimataifa na imekuwa na warsha na makongamano mbalimbali lengo ni kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika visiwa vya Zanzibar.



Wafanyakazi wa Hoteli ya Bluebay Beach Resort na Sultan Sands iliyoko Kiwengwa Zanzibar wakimsikiliza Mkurugenzi, Andrew Smith (hayuko pichani) wakati wa sherehe ya wafanyakazi wa hoteli hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Hemed aipongeza JKU ujenzi wa shule

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amelipongeza Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa kuendeleza kutoa elimu ya ufundi ili kurahisisha upatikanaji wa elimu ya ufundi nchini.

Hemed aliyasema hayo jana wakati akifungua jengo la Shule ya Ufundi ya JKU Mtoni ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za kusherehekea miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema ujenzi huo ni hatua ya kupongezwa kwa kusimamia vyema suala la upatikanaji wa elimu na kueleza kuwa jambo hilo linatofautisha kikosi cha JKU na vikosi vyengine.

Pia alisema amefurahishwa kuona jengo hilo la ghorofa mbili limejengwa na mafundi wa JKU jambo ambalo ni kielelezo tosha cha jeshi hilo kuunga mkono jitihada za serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Pia alisema amefurahishwa na mitaala ya shule hiyo kujumuisha masomo yanayohusiana na dhana ya uchumi wa buluu, muhtasari wa somo la uvuvi na ubaharia hatua ambayo inakwenda sambamba na dhana ya serikali ya kukuza uchumi wa buluu.

Makamu huyo aliwaomba wadau wa maendeleo kuendelea kubuni miradi mbalimbali ambayo italeta tija kwa maslahi mapana ya wananchi.


Aidha, aliwasihi wanufaika wa shule hiyo ya ufundi kulinda miundombinu ya majengo ili libaki katika haiba yake pamoja na kutunza vifaa ili viweze kuwanufaisha vijana wengi.

Akizungumzia Mapinduzi ya Januari 1964, Hemed alisema lengo la kufanyika kwa Mapinduzi ni kurekebisha hali za wananchi kwa kuondosha ubaguzi na unyanyasaji uliokuwa ukifanyika kwa kuwakosesha haki wananchi ikiwamo elimu, fursa za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Muhamed, alisema ujenzi wa jengo hilo unaakisi azma ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kujisimamia katika nyanja tofauti na kuhakikisha kuwa wizara itaendeleza azma hiyo ili kuwaletea manufaa wananchi wa Zanzibar.

Mkuu wa JKU, Kanali Makame Abdalla Daima, alisema kuanzishwa kwa Shule ya Ufundi JKU Mtoni ni kusaidia vijana waliokosa sifa ya kujiendeleza na taasisi za elimu ya juu ili kuwapatia ujuzi wa ufundi kujikwamua kimaisha.

Aidha, alisema jengo hilo litapunguza uhaba wa nafasi kwa wanafunzi ambao watapata ujuzi katika mazingira mazuri zaidi na kuiomba serikali kujenga jengo kama hilo kisiwani Pemba kwa kuwarahisishia vijana wanaoishi kisiwani hapa.





# Akimbiwa na mumewe madai kuzaa mtoto mwenye ulemavu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Kata ya Kinamapula katika Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, Neema Makoye, amedai kukimbiwa na mume wake, Peter Busungu na kuachiwa familia baada ya kujifungua mtoto mwenye ulemavu wa viungo.

Akisimulia mkasa huo jana wilayani hapa, Makoye alisema yeye ni mama wa watoto watatu na kati ya hao, mmoja Boniphane Peter alizaliwa miguu yake imejikunja hali iliyosababisha mume wake kumkimbia na kumwachia majukumu ya kulea familia bila usaidizi.

Alisema baada ya kumpata mtoto huyo alimwanzishia matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama ili kuangalia namna ya kuweka sawa viungo vyake na alikabidhiwa katika kitengo cha mifupa cha miguu kifundo na kupewa viatu vya kuvaa, lakini havikumsaidia.

Makoye pia alisema alipewa rufani hadi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, lakini walimtaka kufika katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando kwa ajili ya upasuaji mdogo wa mifupa, lakini mpaka sasa miaka miwili hajafika huko kutokana na kukosa fedha za matibabu.

"Mtoto wa kwanza nilijifungua salama akiwa mzima. Tatizo lilianza baada ya kujifungua mtoto wa pili akiwa mwenye ulemavu. Nimekimbiwa na mume na sina msaada wowote kutoka kwenye familia yake na wanadai mtoto si wao kwa sababu ukoo wao hawana mtu wa namna hiyo.

"Taarifa nilizo nazo anaishi wilaya jirani ya mkoani Geita na familia nyingine. Naomba serikali kupitia ustawi wa jamii wamchukulie hatua za kisheria na aungane nami katika kuhakikisha mtoto anapata matibabu kama nilivyoshauriwa na madaktari," alisema.

Mmoja wa majirani zake, Bahati Kassim, alisema wamekuwa wakimsaidia mahitaji familia hiyo na kwa umri alio nao mtoto huyo ni muda wa kufanyiwa upasuaji na jinsi umri unavyozidi kwenda itashindikana kwa sababu mifupa yake itakuwa imeshakomaa.

Mjumbe wa Nyumba 10 wa Kinamapula, Mpemba Makomba, alisema majirani zake wamemchangia fedha kwa ajili ya kupata bima ya afya ili kumtibu mtoto wake.

Alisema maisha ya mama huyo ni magumu na sehemu anayoishi ni nyumba ya ukoo wa familia anayotoka mume wake aliyemkimbia na bado wanamnyanyapaa na kushindwa kumsaidia mahitaji kwa madai mtoto si wao na ukoo wao hawana mtu mwenye ulemavu wowote.



Fundi Bajaji, Paschali Elias, mkazi wa Shinyanga akitengeneza bajaji na kuwataka vijana wajitume kufanya kazi ikiwamo kujiajiri na kuacha kukaa vijiweni. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Machinga waomba miundombinu bora

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAFANYABIASHARA kutoka katika masoko mbalimbali mkoani Mwanza wameiomba serikali kurekebisha miundombinu ya masoko hayo ili kuwasaidia kufanya kazi katika mazingira rafiki yatakayowawezesha kuendelea kubaki katika maeneo hayo na kuacha kukimbilia kuuza bidhaa barabarani pamoja na pembezoni mwa maduka.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti kufuatia wimbi la wafanyabiashara kurejea kuuza bidhaa zao barabarani licha ya kupangiwa maeneo katika masoko ndani ya Halmashauri za Manispaa ya Ilemela na Jiji la Mwanza kwa ajili ya kufanyia biashara zao.

Mfanyabiashara katika soko la Milongo jijini Mwanza, Makubi Athumani, alisema ndani ya soko hilo kuna tatizo la miundombinu ya barabara inayosababisha wafanyabiashara hao kushindwa kufikisha bidhaa zao ndani ya soko na hivyo kutumia gharama kusafirisha bidhaa zao.

Alisema soko hilo linahitaji kuwa na barabara inayoingia moja kwa moja ili kuepusha kuingia gharama mara mbili.

Mfanyabiashara wa soko eneo la Maduka Tisa katika Manispaa ya Ilemela, Amina Hussein, alisema licha ya wafanyabiashara ndogo ndogo kuhamishiwa katika masoko bado wafanyabiashara hao wamekuwa wakifunga vibanda na vizimba vyao na kurejea mjini kati na kufanya maeneo hayo kubaki kuwa ya kutunzia bidhaa.

Alisema hatua hiyo inasababisha hali ya biashara kuendelea kuwa ngumu katika masoko hayo kutokana na wateja wote kuishia katika maeneo walipo wafanyabiashara hao na kuacha kuingia ndani ya masoko hayo yaliyopangwa.

Mwenyekiti wa Masoko mkoani Mwanza, Hamad Nchola, aliwataka wafanyabiashara hao kuwa wavumilivu katika maeneo hayo waliyopangiwa wakati serikali ikiendelea na utaratibu wake wa kurekebisha miundombinu.

Akizungumza baada ya kutembelea soko la Milongo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, aliagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuhakikisha inakarabati barabara hizo.

# Polisi yachunguza kifo cha aliyefia ndani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linachunguza kifo cha Daudi John, ambaye alikutwa amefariki dunia chumbani kwake katika nyumba aliyokuwa amepanga mtaa wa Kambarage, Manispaa ya Shinyanga.

Kijana huyo aligundulika akiwa amefariki dunia chumbani kwake juzi, majira ya saa 4:00 asubuhi baada ya wapangaji wenzake kuona haamki huku muziki ukilia kwa sauti ya juu kutoka ndani kwake.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kambarage, Malick Juma, akielezea tukio hilo jana, alisema alipopata taarifa juu ya kifo cha kijana huyo, alifika eneo la tukio na kumkuta amefariki dunia akiwa amelala juu ya kitanda ndipo akatoa taarifa polisi. Alisema alipowauliza wapangaji wenzake nini kilitokea juu ya kifo cha kijana huyo, walisema hawafahamu lolote kwa sababu alikuwa ndani peke yake huku akipiga muziki kwa sauti ya juu hadi kulipokucha asubuhi muziki uliendelea kulia ndipo majira hayo ya saa 4:00 asubuhi, ikagundulika alikuwa ameshafariki dunia.

"Kijana huyu hajulikani kwao ni wapi kwa sababu alikuja mjini kutafuta maisha na sisi kama serikali ya mtaa hatuna taarifa zake, hivyo tunaomba vijana walete taarifa zao kwenye ofisi zetu ili linapotokea jambo lolote iwe virahisi kuwasiliana na ndugu zake," alisema Juma.

"Serikali ya mtaa tutaendelea kuwatafuta ndugu zake kupitia marafiki zake ili waje wauchukue mwili wa ndugu yao na kwenda kuupumzisha kwenye makazi yake ya milele," aliongeza.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa kifo cha kijana huyo na kueleza mwili wake umehifadhiwa katika chumba cha maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga.

Alisema jeshi hilo linaendelea na upelelezi ili kubaini chanzo cha kifo cha kijana huyo na hakuna mtu ambaye anashikiliwa kwa sasa na ikigundulika aliuawa wahusika wote watasakwa na kuchukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.

# Waziri wa Israel azuru msikiti wa Al-Aqsa

**JERUSALEM, Palestina**

WAZIRI mpya wa Usalama wa Taifa wa Israel, Itamar Ben-Gvir, amezuru kwa muda mfupi eneo la msikiti wa Al-Aqsa mjini Jerusalem.

Ziara hiyo aliifanya jana katika eneo ambalo pia linaheshimiwa na Wayahudi, na kusababisha kulaaniwa kutoka kwa Wapalestina na nchi jirani ya Jordan.

Waziri huyo baada ya kukamilisha ziara hiyo aliandika kupitia ukurasa wake wa Twitter "Hekalu la Mlima liko wazi kwa wote,"

Picha za video zilimuonyesha akitembea pembezoni mwa msikiti huo, akiwa amezungukwa na ulinzi mkali.

Ofisa mmoja wa Israel alisema ziara ya Gvir ya dakika 15 katika eneo la Al Aqsa ilizingatia kile kinachoitwa mpangilio wa hali ilivyo, wa miongo kadhaa iliyopita, ambao unawaruhusu wasio Waislamu kuzuru kwa sharti la kutoswali.

Kujiunga kwa Gvir, kiongozi wa chama cha Jewish Power chenye msimamo mkali wa mrengo wa kulia, kujiunga na Waziri Mkuu aliyechaguliwa tena Benjamin Netanyahu kumezidisha hasira ya Wapalestina kuhusu juhudi zao za muda mrefu za kupata taifa.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Palestina ilisema inalaani vikali kuvamiwa kwa msikiti wa Al-Aqsa na waziri mwenye itikadi kali Ben-Gvir na inaona kuwa ni uchochezi usio na kifani na ongezeko la hatari ya mzozo.

Msemaji wa Hamas, kundi la Kiislamu la Palestina ambalo linakataa kuishi pamoja na Israel, alisema ziara ya Ben-Gvir, ni kuendelea kwa tabia ambayo kutazileta pande zote karibu na mzozo mkubwa.

Mvutano kati yake na Israel ambao ulizidi kuwa ghasia katika eneo hilo Mei 2021 na kushuhudia Hamas wakirusha makombora kuelekea Jerusalem, na kusababisha mzozo wa siku 11 na Israel.

Ziara ya mwaka 2000 ya kiongozi wa mrengo wa kulia wa Israel Ariel Sharon, kiongozi wa upinzani wakati huo, iliwakasirisha Wapalestina. Ghasia zilizofuata ziliongezeka na kuwa maasi ya pili ya Wapalestina, au maarufu intifada.

Jumba la Al Aqsa, linalojulikana kwa Waislamu kama Patakatifu, ni eneo la tatu kwa Uislamu kwa utakatifu. Pia ni eneo takatifu zaidi la Uyahudi, mabaki ya mahekalu mawili ya kale ya imani.

**BBC**



Wakazi katika mji wa Malawi, Blantyre wakijiandaa kupata chanjo dhidi ya kipindupindu. **PICHA:REUTERS.**

# Askari wa Uganda wauana Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

Uchunguzi umeanza baada ya askari wa Uganda anaelinda amani nchini Somalia chini ya Kikosi cha Mpito cha Umoja wa Afrika (Atmis) kuwaua kwa kuwapiga risasi wenzake watatu mjini Mogadishu.

Ufyatuaji risasi huo ulifanyika katika makao makuu ya kikosi cha jeshi la Uganda. Msemaji wa jeshi la Uganda, Felix Kulaigye, alithibitisha tukio hilo na kukamatwa kwa mwanajeshi huyo.

Inasemekana kuwa alivamia na kumpiga risasi askari wa kwanza kifuani.

Wanajeshi wengine hapo awali walidhani kuwa kambi yao ilikuwa imeshambuliwa.

Mwathiriwa wa pili alipigwa risasi tatu kichwani alipokuwa akijaribu kujua kinachoendelea. Askari wa tatu alipigwa risasi ya mgongoni alipokuwa akijaribu kukimbia.

Milio ya risasi ilikoma baada ya kiongozi mmoja kumpokonya bunduki mtuhumiwa huyo.

**BBC**

# Russia yakiri kuuawa wanajeshi 63

**MOSCOW, Russia**

RUSSIA imekiri kwamba makombora ya Ukraine yamesababisha vifo vya zaidi ya wanajeshi wake 60 katika mashambulizi yaliyofanyika siku ya mkesha wa mwaka Mpya katika eneo linalodhibitiwa na nchi hiyo mashariki mwa Ukraine.

Katika tangazo la nadra, Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema askari 63 wa Urusi waliuawa katika mji wa Makiivka kwenye shambulizi la makombora manne. Taarifa hiyo ilisema mifumo ya makombora ya Himars inayotoka Marekani ndiyo ilitumika katika mashambulizi hayo.

Idadi ya wanajeshi wengi kuawa ndiyo ya kwanza kubwa kutangazwa na Russia tangu kuanza kwa vita hivyo miezi kumi iliyopita.

Jeshi la Ukraine limedai kufanya mashambulizi hayo, likitaja idadi ya vifo kufikia karibu askari 400 wa Russia.

Baadhi ya waandishi wa habari wa Russia walitilia shaka idadi ya vifo iliyotolewa wakisema idadi kamili huenda ni kubwa zaidi.

**DW**

## Maelfu wamuaga papa Benedict XVI

**VATCAN, Roma**

MAELFU ya waombolezaji walijitokeza katika siku ya kwanza ya kutoa heshima kwa papa Benedict XVI ambaye mwili wake umelazwa katika kanisa la Mtakatifu Petro mjini Vatican kwa ajili ya kumuaga.

Polisi wa Vatican na jeshi la ulinzi wamekadiria hadi jana jioni kuwa karibu watu 65,000 walifika kanisani hapo. Miongoni mwa waombolezaji wa kwanza ni Waziri Mkuu wa Italia Giorgia Meloni.

Watu waliruhusiwa kuutizama mwili kwa saa 12, na leo papa huyo mstaafu atazikwa katika makaburi yaliyoko chini ya kanisa la Mtakatifu Petro.

Ibada ya mazishi itaongozwa na Papa Francis.

Litakuwa tukio la kihistoria ambapo Papa mmoja atamzika mwingine na hali hiyo ni kutokana na kujiuzulu kwa Benedict, mnamo 2013.

Kiongozi huyo wa kidini alifariki dunia kwenye mkesha wa Mwaka Mpya akiwa na umri wa miaka 95.

Alizaliwa katika kijiji kimoja cha jimbo la kusini mashariki la Bavaria nchini Ujerumani na kuwa papa mwaka wa 2005

## Wabunge wafungwa jela kumpiga mwenzao bungeni

**DAKAR, Senegal**

MAHAKAMA moja nchini Senegal, imewahukumu wabunge wawili kifungo cha miezi sita gerezani kwa kumshambulia mwenzao mwanamke ambaye ni mjamzito.

Wanaume hao wawili walimpiga mbunge mwenzao wa kike wakati wa vurumai iliyotokea bungeni Desemba mosi. Massata Samb na Amadou Niang, wabunge kutoka chama cha upinzani cha PUR, wamekabiliwa na adhabu hiyo. Waliamriwa kulipa jumla ya faranga milioni 5 kama fidia kwa mbunge huyo wa kike Amy Ndiaye.

Ndiaye ni mbunge wa muungano wa chama tawala Benno Bokk Yakaar. Akizungumza kwenye kesi hiyo, wakili wake alisema mteja wake alilazwa hospitali baada ya tukio hilo na nusura ampoteze mtoto.

Katika picha zilizoonyeshwa kwenye televisheni ambazo zilishtua Wasenegal, Samb alionekana akimzaba kofi Ndiaye baada ya kukejeli matamshi yake.

Alijibu kwa kumrushia kiti na wabunge wengine kisha wakamsukuma Ndiaye sakafuni, kabla ya kupigwa mateke kwenye tumbo na mmoja wa watu waliohukumiwa.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MWAJUMA HUSSEIN MASSORO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S2301-0021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BUNJU SEKONDARY** November, 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/489756/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HUBERT THEODORY MPETE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 507 BAP – SCANIA.** Chassis namba **4399558.** Engine namba **4032206.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **TR/RB/693/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CORNEL JOACHIM MINJA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 113 DHY – TOYOTA RAV 4.** Chassis namba **SXA117156752.** Engine namba **2693139.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/4206/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SUNVIC EXPRESS LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 312 AVJ – TOYOTA LAND CRUISER.** Chassis namba **JTELB71907007930.** Engine namba 0335008. Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 319 AVJ – TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba **JTLB71J807019163.** Engine namba **0371706.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/3655/2022.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**SHINYANGA EMPORIUM** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA PIAGGIO YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 484 CCA.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH /RB/ 07/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MANUMBU HEZRONE DAUDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T300CEX** aina ya Toyota Cresta, yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/495077/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KENNEDY AYARE ODOYO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 472 CKF** aina ya Rav 4, yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/2507/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LANZHOU LIMINGTIANMU BUILDING MATERIAL COMPANY LIMIT** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **FAW** yenye namba za usajili **T 217 DDF** chasis namba **LFNGBRJD4EAC23184** engine namba **52530057,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/2762/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na……01/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: KIBWANA NASSORO SEWANDO WA KIHONDA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA THENEY KIBWANA NASSORO**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 09 Mwezi 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 01 mwaka 2023**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BURUDANI

## MARIOO AMKOSOA DIAMOND



NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Omary Mwanga maarufu Marioo, amepuuzilia mbali madai ya bosi wa WCB, Diamond Platnumz, kuwa aliwahi kuomba kusainiwa kwenye lebo hiyo.

Marioo amebainisha kuwa madai ya Diamond yalikuwa ni kuteleza kwa ulimi tu na kudai hayana ukweli wowote.

"Hahaha mkubwa kateleza, mfupa hauna ulimi," alisema Marioo.

Hapo awali, Diamond akiwa kwenye mahojiano alidai kwamba Marioo alimfuata nyumbani kwake akiomba kusainiwa WCB.

"Kabla ya kutoa Beer tamu Marioo alikuja nyumbani. Alipokuja na tukazungumza alitaka nimsaini. Nilimwambia, Marioo nikikutazama naona unafanya vizuri, nahisi kama kukusaini si kukutendea haki maana wewe tayari unafanya vizuri.

"Nikikusaini unajua kuna watu wengine ambao wataleta chuki zao kwa sababu unafuatana na Diamond na wasikupigie nyimbo. Kuna redio nyingi ambazo hazipigi nyimbo zangu, watakuwa hawakupigii zako," alisema.

Bosi huyo wa WCB alisema alimwagiza Marioo kutafakari kuhusu hatua hiyo na mazungumzo yao kabla ya kufanya uamuzi.

## BUSHOKE AFUNGUKA KUHUSU UKIMYA



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Ruta Maximilian maarufu Bushoke, amefunguka sababu za ukimya wake kwa kipindi kirefu bila kutoa wimbo.

Bushoke amesema kuwa kwa kipindi kirefu amewekeza nguvu na akili yake kwenye upande wa muziki wa 'Live band', na kwamba ndio kitu pekee ambacho amekuwa akikifanya kwa kipindi chote, tangu alipositisha kuachia nyimbo redioni.

Ameweka wazi kuwa haikuwa rahisi kwa yeye kufanya uamuzi wa kuhamia kufanya muziki wa live band, na kusalia kutumbuiza kwenye mahoteli na kumbi mbalimbali za starehe, lakini ilimlazimu kufanya hivyo, kutokana na uhitaji mkubwa wa kujaribu uzoefu mpya nje ya alichokuwa akikifanya hapo awali.

"Muziki wa Live Band una manufaa, lakini si fedha, niliwahi kujiuliza nahitaji umaarufu wa kubakia naimba tu, au nataka kuimba muziki ambao inabidi pia nijifunze zaidi?

"Kwa maana kujulikana mwanamuziki si kuwa mwanamuziki, kwa hivyo mimi nilichunguza vyote viwili na nikasema nifuate hiki cha Live Band, na nilipiga hesabu nikakiona hakina hela, lakini kina manufaa mengine," amesema Bushoke.

"Ninachoweza kusema watu wasubiri kazi, na ninajua kwamba wamesubiri sana, lakini nawaambia sasa hivi hawatasubiri sana muda si mrefu nitawapatia kitu roho inapenda, nitajitahidi kuwa kitu kizuri cha kisasa naimani watafurahi," aliongeza.



## POSH QUEEN AKATAA AJIRA

MREMBO wa mitandaoni Bongo, Jacqueline Obeid 'Posh Queen' amesema yeye hawezi kukubali kuajiriwa.

Posh Queen ambaye amehitimu Stashahada ya Insurance and Risk Management katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), amesema akiajiriwa anajua atakavyosumbuliwa.

Posh alisema anamshukuru Mungu kwani hata alipokuwa chuoni alikuwa ameshaanza kufanya biashara, hivyo baada ya kumaliza chuo haitaji ajira.

"Sitaki kuajiriwa maana najua nitakayokutana nayo. Ni bora kujiajiri mwenyewe nitakuwa huru na umbo langu," alisema Posh.

# ZANZIBAR YATAJA VIONGOZI 22 WAKUSIMAMIA NGUMI

**Na Saada Akida, Zanzibar**

IDARA ya michezo Zanzibar imeteua viongozi 22 watakaosimamia Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa na Shirikisho la Ngumi za Ridhaa visiwani hapa, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kamishna wa Idara ya Michezo Zanzibar, Ameir Mohamed Makame, alisema katika viongozi hao, 11 watasimamia Kamisheni ya Ngumi na 11 watakuwa ndani ya shirikisho la mchezo huo kwa muda wa miezi saba.

Alisema viongozi hao walianza kazi rasmi tangu Desemba 28, mwaka jana, ilipoteuliwa kamati hiyo na watadumu hadi Juni 27, mwaka huu na wamepewa dondoo 10 zitakazowaongoza katika utendaji wao wa kazi kwa muda wote wa uongozi wa muda.

"Kwa mujibu wa kanuni ya 20 (1) Kanuni za Usajili wa Vyama vya Michezo za mwaka 2014, imetulazimu kuteua viongozi wa muda wa Kamisheni ya Mchezo wa Ngumi za Kulipwa na Ridhaa Zanzibar," alisema Ameir.

Alitaja viongozi wa kamisheni hiyo kuwa inaongozwa na Rais Dk. Ali Salum Ali, Makamu wa Rais, Edwin George, Katibu Mkuu, Hakeem Kimara akisaidiwa na Nassib Amour.

"Wajumbe ni Ahmed Burhani Msoma, Issa Said, Aman Boniface, Maryam Charles, Jambia Said, Mussa Said Sukwa na Abdillahi Juma," aliwataja.

Alisema viongozi wa Shirikisho la Ngumi za Ridhaa watasimamiwa na Rais Ahmed Burhan, makamu wake akiwa ni Suleiman Mhamoud Jabir, Katibu ni Kesi Said Mohamed akisaidiwa na Maryam Suleiman.

Aliwataja wajumbe kuwa ni Issa Chaap, Shafii Masoud, Aman Twaha, Omar Hamad, Rashid Said, Salha Rajab Mrisho na Said Ali Said.

"Viongozi hao wanatakiwa kuzingatia katiba kwani uongozi utakuwa na mamlaka ya kutekeleza yote yanayopaswa kutekelezwa kikatiba ikiwamo kuteua kamati ndogo ndogo kwa mujibu wa mahitaji ya kamisheni.

Alizitaja dondoo zingine ni Kufungua akaunti, kuendesha mafunzo kwa walimu, waamuzi na majaji, kuainisha na kuanzisha utaratibu wa kuwapata mabondia kwenye ngumi za ridhaa, kuandaa mapambano ya utambulisho/uzinduzi wa Shirikisho la Ngumi za Ridhaa, kuwasilisha ratiba inayoonyesha muda watakaotekeleza majukumu hayo, kuwasilisha ripoti ya utekelezaji kila mwisho wa mwezi na kufanya uchanguzi kwa kuwapata viongozi watakaongoza mchezo huo.

## HADI 2025...




Kipa wa Yanga, Djigui Diarra, akisaini mkataba mpya jijini Dar es Salaam jana, utakaomuweka klabuni hapo hadi 2025. Kulia ni rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said. **PICHA: YANGA**

# DRFA yaonya vijeba Ligi ya Vijana Ubungo

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Ligi ya Vijana wenye umri chini ya miaka 17 Wilaya ya Ubungo, ikitarajiwa kuanza kutimua vumbi Januari 15, Chama cha Soka Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), kimeonya kuhusu timu zitakazochezesha vijeba (wachezaji waliozidi umri huo).

Ligi hiyo itakayoshirikisha timu mbalimbali za vijana wilayani humo, inatarajiwa kupigwa katika Uwanja wa Kinesi uliopo Urafiki, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu Wilaya ya Ubungo (UFA), Frank Mchaki, alisema maandalizi kuelekea ligi hiyo yanaendelea vizuri na kwamba fomu za ushiriki zimeshaanza kutolewa.

"Tunajiandaa na ligi hiyo ambayo itafanyika kwenye Uwanja wa Kinesi, wachezaji wote wanaendelea kufanya mazoezi ili kuhakikisha wanafanya vizuri," alisema Mchaki.

Katibu huyo alisema DRFA, wamewataka viongozi wa timu zote kuhakikisha wanazingatia umri wa wachezaji kwani hawatakuwa tayari kulifumbia macho suala la udanganyifu wa umri.

"DRFA wametuhimiza tuwe makini kwenye masuala ya umri kwani wamebaini kuna baadhi ya wachezaji huwa wanachezeshwa wakiwa na umri mkubwa kitu ambacho hakitakiwi na kinaharibu mpira wetu," alisema Mchaki.

Alisema lengo la kuendesha ligi hiyo ni kupata wachezaji ambao wataiwakilisha vema Timu ya Taifa ya Vijana pamoja na kuibua vipaji vitakavyokuwa hazina ya baadaye na ya sasa kwa timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

# Simba Queens, Fountain Gate vitani Uhuru leo

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania Bara inaingia raundi ya nne leo, wakati Mabingwa Watetezi, Simba Queens, watakapokuwa wenyeji wa vinara wa ligi hiyo, Fountain Gate Princess, majira ya saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Kwenye mechi hiyo pia kutakuwa na mchuano mkali wa wachezaji ambao ni vinara wa kupachika mabao, Opa Clement wa Simba Queens na Cynthia Musungu wa Fountain Gate Princess ambao wote wametupia mabao matatu kila moja.

Mashabiki wa soka la wanawake watataka kuona kama wote watapachika tena mabao leo, au mmoja wapo atamuacha mwenzake.

Simba Queens itataka kurejesha imani kwa mashabiki wake baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga Princess, Desemba 12, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Timu hizo zinashuka dimbani leo huku Fountain Gate Princess ikiwa inaongoza ligi hiyo, ikicheza mechi tatu, ikishinda zote, mabao saba na haijaruhusu wavu wake kuguswa ikiwa na pointi tisa, hivyo haitakuwa mechi rahisi kwa Simba Queens, ikikumbukwa kuwa timu hiyo ndiyo iliyoichapa Yanga Princess bao 1-0 Desemba 7, mwaka jana na kutimua benchi lake la ufundi chini ya kocha Edma Lema.

Simba Queens inakamata nafasi ya nne kwenye msimamo ikiwa na pointi nne, kwa kushinda mechi moja, sare moja na kupoteza moja.

Mbali na mechi hiyo, leo kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, wenyeji, Baobab Queens wataikaribisha The Tigers Queens na Mkwawa Queens kwa mara ya kwanza itakuwa nyumbani Uwanja wa Samora, Iringa kucheza dhidi ya Amani Queens.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena kesho kwa Yanga Princess kucheza dhidi ya Alliance Girls kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na Ceasiaa Queens itacheza dhidi ya JKT Queens, Uwanja wa Samora, Iringa.

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUTUA NEWCASTLE

CRISTIANO Ronaldo ana kipengele katika mkataba wake na Al-Nassr kinachomruhusu mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 37, kujiunga na Newcastle United kwa mkopo ikiwa watafuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu. ***(Marca)***

### SAKA, SALIBA KUFUNGWA

KLABU ya Arsenal imeanzisha vipengele vya kuongeza mkataba kwa winga wa England, Bukayo Saka na beki wa kati wa Ufaransa, William Saliba, wote wakiwa na umri wa miaka 21. ***(ESPN)***

### BADIASHILE SAFI CHELSEA

MLINZI wa kati wa Ufaransa, Benoit Badiashile, mwenye umri wa miaka 21 yuko London kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu baada ya Chelsea kuafikiana na Monaco kwa mkataba wenye thamani ya euro milioni 38. ***(Football London)***

### NUNES ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanapanga kumnunua kiungo wa kati wa Ureno, Matheus Nunes, mwenye umri wa miaka 24 kutoka Wolves msimu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### BELLINGHAM NA DORTMUND

KIUNGO wa kati wa England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19, anatazamiwa kukutana na maofisa wa Borussia Dortmund kabla ya Januari 6, atakapowafahamisha kuhusu nia yake ya kuondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(AS)***

### FELIX KWA MKOPO

ARSENAL, Manchester United na Chelsea zimepewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23 kwa mkopo. ***(Athletic)***

### ARSENAL OFA YA PILI

ARSENAL wamewasilisha ofa ya pili kwa winga wa Ukraine, Mykhailo Mudryk, inayodhaniwa kuwa chini ya bei ya Shakhtar Donetsk ya euro milioni 100. ***(ESPN)***

### MUANI AWANIWA BAYERN

MANCHESTER United na Bayern Munich zinavutiwa na Randal Kolo Muani, lakini Eintracht Frankfurt wanataka euro milioni 60 hadi 70 kumuachia mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24. ***(Nicolo Schira)***

### PERRONE ANUKIA CITY

KLABU ya Manchester City inajiandaa kushinda katika kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa kati wa Argentina, Maximo Perrone, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Velez Sarsfield. ***(90 min)***

### FRANCA ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inatarajiwa kuendelea na mazungumzo na Flamengo kuhusu kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Matheus Franca,18. ***(90 Min)***

### ALLISTER KUBAKI BRIGHTON

KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi, anatumaini kiungo wa Argentina, Alexis Mac Allister mwenye umri wa miaka 24, atabakia katika klabu hiyo angalau hadi mwisho wa msimu. ***(Argus)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG: SITANUNUA STRAIKA MPYA UNITED

●●● Tuna timu nzuri, Anthony Martial, nina furaha sana na uchezaji wake katika michezo mingi, hivyo...

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag amesisitiza kwamba, Manchester United "haitachoma fedha" kumsajili mshambuliaji mpya Januari hii.

Baada ya mwanzo mgumu wa maisha kama kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao, timu ya Ten Hag imekuwa bora zaidi hivi karibuni na kwa sasa inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England kutokana na kushinda mara tatu mfululizo.

Cristiano Ronaldo alikuwa ndani na nje ya timu kabla ya mahojiano yake na Piers Morgan yaliyosababisha mkataba wake kusitishwa, huku Anthony Martial akikabiliwa na majeraha.

Lakini licha ya hitaji la mshambuliaji wa kati kusaidia United kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ten Hag anahisi United lazima iepuke makosa ya siku za nyuma kwa kupoteza fedha kwa kununua mshambuliaji mpya.

"Unahitaji mtu ambaye anaweza kuwa na mchango na si kuchoma fedha," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari.

"Tuna timu nzuri. Tuna mshambuliaji, Anthony Martial, nina furaha sana na uchezaji wake katika michezo mingi.

"Amekuwa na matokeo mazuri sana. Ukiona dakika zake na mchango wake umekuwa mkubwa."

"Tunazingatia kila kitu. Nina nafasi kidogo kwa sababu sitaki kusitisha mchakato huo.

"Tunapoamua kununua mchezaji ambaye anaweza kushindana na wachezaji 11 wa kuanzia au kwa uchache kucheza michezo mingi ili kuwa na mchango."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,063,6
MECHI KALI
ASTON VILLA
VERSUS
WOLVERHAMPTON
1 | 1.92
X | 3.41
2 | 3.76
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SILVA ADOKEZA KUONDOKA CITY

**MANCHESTER, England**

BERNARDO Silva anaweza kutafuta "mradi mpya" katika miaka michache ijayo, lakini atasubiri hadi mwishoni mwa msimu kabla ya kujadili mustakabali wake na Manchester City.

Tangu ajiunge na Man City kutoka Monaco 2017, Silva ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu England, huku akicheza kama mmoja wa wachezaji muhimu katika kikosi cha kocha, Pep Guardiola.

Barcelona iliripotiwa kuwa na nia ya kumnasa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno katika dirisha lililopita la usajili, lakini ikashindikana.

Ingawa Silva analenga kushinda mataji zaidi akiwa na City kabla ya mwishoni mwa msimu, amekataa kuondoa uwezekano wa kuhama kabla ya msimu ujao.

"Nimezingatia sana msimu huu na haina maana kuzungumza juu ya kuondoka kwa sababu tuko katikati ya msimu," alisema Silva akiiambia Record.

"Nimekuwa Manchester City kwa takriban miaka sita, naiheshimu sana klabu, habari zinaendelea kutoka na watu wanajua kuwa kumekuwa na mazungumzo kati yangu na klabu na, mwisho wa msimu, nitazungumza tena kuona ni nini bora kwa pande zote mbili.

"Nina umri wa miaka 28, nitakuwa na umri wa miaka 29 msimu wa majira ya joto, na nina miaka miwili zaidi kwenye mkataba wangu wa Manchester City. Mkataba wangu utaisha nikiwa na miaka 31.

"Sitaficha hilo lengo langu katika miaka ijayo, ikiwa kitu kizuri kitatokea mahali pengine, labda itakuwa kuhamia mradi mpya."

Wakati Barcelona ikionekana kuwa na uwezekano mkubwa wa Silva kutua huko, kiungo huyo hakuficha nia yake ya kutaka siku moja kurejea nchini kwao Ureno.

"Lengo langu lilikuwa kurejea Benfica nikiwa na umri wa miaka 32 zaidi," alisema. "Ninafikiria nini leo? Inategemea nini kitatokea msimu ujao wa majira ya joto.

"Sitasema uwongo, si kitu ambacho sifikirii, nafikiria kila mwaka. Limekuwa lengo. Sikuweza kutimiza ndoto yangu ya kuichezea Benfica nikiwa na umri wa miaka 19 au 20."




# Dumfries agombewa EPL

**LONDON, Engand**

KLABU za Chelsea, Manchester United na Tottenham zote zimeripotiwa kujaribu kumsajili beki wa Inter Milan, Denzel Dumfries, baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwenye Kombe la Dunia akiwa na Uholanzi.

Dumfries mwenye umri wa miaka 26, alicheza katika mechi zote tano za Kombe la Dunia kwa nchi yake.

Beki huyo wa kulia amecheza mechi zote 15 za Inter kwenye Serie A msimu huu, na kuanza mara 13, ingawa amecheza dakika 90 pekee mara nne.

Licha ya timu hiyo ya Italia kukataa ofa zote za kumuuza Dumfries katika dirisha lililopita la usajili, inasemekana anaweza kuondoka kwa ada ya euro milioni 60.

Kwa mujibu wa La Gazzetta dello Sport, Inter wako tayari kukubali ada ya euro milioni 60 kumuachia mchezaji huyo.

Chelsea inaripotiwa kumwona Dumfries kama jibu la masuala yao ya kina katika safu ya beki ya kulia wakati huu Reece James akipambana na majeraha.

United wanaamini kuwa anaweza kuchukua nafasi ya Diogo Dalot, na Tottenham wanahisi kuwa yeye ni chaguo bora zaidi.



605,974/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/01/23 | 18:00 | KAS Eupen vs Royal Charleroi SC | 2.65 | 3.55 | 2.44 |
| 02. 07/01/23 | 18:00 | Millwall FC vs Sheffield United | 2.90 | 3.20 | 2.43 |
| 03. 07/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Burnley FC | 2.32 | 3.40 | 2.90 |
| 04. 07/01/23 | 18:00 | Cambridge United vs Bristol Rovers | 2.85 | 3.30 | 2.41 |
| 05. 07/01/23 | 18:00 | Morecambe FC vs Cheltenham Town | 2.50 | 3.25 | 2.75 |
| 06. 07/01/23 | 18:30 | RKC Waalwijk vs SC Heerenveen | 2.43 | 3.50 | 2.70 |
| 07. 07/01/23 | 20:30 | Brentford FC vs West Ham United | 2.65 | 3.25 | 2.65 |
| 08. 07/01/23 | 22:00 | Fortuna Sittard vs Go Ahead Eagles | 2.60 | 3.30 | 2.65 |
| 09. 07/01/23 | 22:45 | Royal Antwerp FC vs KAA Gent | 2.44 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 07/01/23 | 23:00 | Espanyol Barcelona vs Girona FC | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 08/01/23 | 14:30 | US Salernitana vs Torino FC | 3.20 | 3.20 | 2.25 |
| 12. 08/01/23 | 15:30 | Bristol City vs Swansea City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 13. 08/01/23 | 17:00 | Spezia Calcio vs US Lecce | 2.55 | 3.10 | 2.85 |
| 14. 08/01/23 | 18:00 | SV Zulte Waregem vs Yellow-Red KV Mechelen | 2.70 | 3.70 | 2.32 |
| 15. 08/01/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs GD Chaves | 2.85 | 3.25 | 2.46 |
| 16. 08/01/23 | 18:45 | Excelsior Rotterdam vs FC Groningen | 2.65 | 3.55 | 2.45 |
| 17. 08/01/23 | 19:00 | Fenerbahce Istanbul vs Galatasaray Istanbul | 2.39 | 3.50 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 04/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 5055 | Salernitana vs AC Milan | 5.94 | 4.36 | 1.47 |
| 14:30 | 5537 | Sassuolo vs Sampdoria | 1.69 | 3.71 | 4.55 |
| 15:00 | 1019 | Tusker vs Vihiga Bullets FC | 1.25 | 5.60 | 11.00 |
| 15:00 | 1023 | AL Sahel SC vs AL Hazm | 4.37 | 3.25 | 1.78 |
| 15:00 | 1176 | Gor Mahia vs Kenya Commercial Bank | 2.19 | 2.78 | 3.51 |
| 15:00 | 1728 | Bidco United vs Nzoia United | 3.05 | 2.81 | 2.40 |
| 15:00 | 3180 | Ulinzi Stars vs Mathare United | 1.44 | 3.90 | 6.63 |
| 15:00 | 4687 | Nairobi City Stars FC vs AFC Leopards | 2.81 | 2.81 | 2.57 |
| 15:00 | 5327 | Bandari vs Posta Rangers | 1.85 | 2.92 | 4.58 |
| 15:00 | 5833 | KK Homeboyz vs Kariobangi Sharks | 2.18 | 2.82 | 3.50 |
| 15:15 | 4568 | Kenya Police vs Wazito | 2.00 | 2.93 | 3.86 |
| 15:45 | 5668 | AL Ain vs AL Arabi (SA) | 5.07 | 3.42 | 1.64 |
| 16:15 | 4301 | Lekhwiya SC vs Al Gharafa SC | 1.45 | 4.68 | 5.07 |
| 16:30 | 3154 | Spezia vs Atalanta | 4.57 | 3.92 | 1.65 |
| 16:30 | 5769 | Torino vs Verona | 1.77 | 3.51 | 4.35 |
| 17:00 | 2537 | Cotonsport vs Stade Renard | 2.13 | 2.77 | 3.70 |
| 17:00 | 2730 | Kasimpasa vs Alanyaspor | 2.30 | 3.48 | 2.84 |
| 17:00 | 3192 | Kayserispor vs Fatih Karagumruk | 1.93 | 3.64 | 3.54 |
| 18:00 | 3727 | Olympique Safi vs Maghreb Tetouan | 2.09 | 2.91 | 3.59 |
| 18:00 | 4001 | Malkiya Club vs Qalali | 1.80 | 3.46 | 3.90 |
| 18:00 | 4957 | Asteras Tripolis vs Lamia | 1.78 | 3.19 | 4.98 |
| 18:00 | 4976 | Farco FC vs Talaea El Gaish | 3.12 | 2.73 | 2.58 |
| 18:30 | 1858 | Lecce vs Lazio | 3.53 | 3.18 | 2.08 |
| 18:30 | 4389 | Roma vs Bologna | 1.58 | 3.75 | 5.53 |
| 19:00 | 3969 | Panetolikos vs Atromitos | 2.22 | 3.13 | 3.28 |
| 20:00 | 1454 | Akritas Chlorakas vs Anorthosis Famagusta | 4.40 | 3.65 | 1.76 |
| 20:00 | 2775 | AEK Larnaca vs Pafos FC | 2.50 | 3.14 | 2.85 |
| 20:00 | 4206 | Galatasaray vs Ankaragucu | 1.43 | 4.59 | 6.39 |
| 20:00 | 5789 | Konyaspor vs Sivasspor | 1.93 | 3.43 | 3.78 |
| 20:15 | 3884 | MAS Maghrib A Fes vs RS Berkane | 2.35 | 3.05 | 3.15 |
| 20:30 | 2649 | Sectzya Nes Ziona vs Maccabi Petach Tikva | 1.84 | 3.50 | 3.70 |
| 20:30 | 5337 | Cremonese vs Juventus | 4.72 | 3.55 | 1.71 |
| 20:30 | 5643 | Fiorentina vs Monza | 1.66 | 3.81 | 4.65 |
| 21:00 | 1074 | UD Logrones vs Real Sociedad | 6.76 | 4.57 | 1.41 |
| 21:00 | 2089 | CD Linares vs Sevilla FC | 7.57 | 4.88 | 1.35 |
| 21:00 | 3169 | Maccabi Bney Reine vs Hapoel Petah Tikva | 2.04 | 3.25 | 3.30 |
| 21:00 | 4108 | Pontevedra vs Mallorca | 5.99 | 4.09 | 1.51 |
| 21:00 | 5005 | PAOK vs Aris Salonica | 1.89 | 3.19 | 4.29 |
| 21:30 | 4920 | Maccabi Haifa vs Hapoel Haifa | 1.09 | 7.60 | 19.47 |
| 22:00 | 1935 | Real Oviedo vs Atletico Madrid | 6.37 | 4.18 | 1.47 |
| 22:30 | 3423 | Southampton vs Nottingham | 1.99 | 3.33 | 3.62 |
| 22:30 | 3952 | Chelmsford vs Wealdstone | 2.47 | 3.44 | 2.47 |
| 22:30 | 5304 | FUS Rabat vs Union Touarga | 1.79 | 3.06 | 4.67 |
| 22:45 | 1080 | Leeds vs West Ham | 2.49 | 3.34 | 2.64 |
| 22:45 | 1635 | Udinese vs Empoli | 1.58 | 3.95 | 5.14 |
| 22:45 | 2490 | Inter vs Napoli | 2.29 | 3.32 | 2.92 |
| 23:00 | 1239 | Crystal Palace vs Tottenham | 3.18 | 3.28 | 2.17 |
| 23:00 | 2359 | CF Intercity vs Barcelona | 17.87 | 6.81 | 1.15 |
| 23:00 | 4533 | Aston Villa vs Wolverhampton | 1.92 | 3.41 | 3.76 |
| 23:00 | 5669 | Alaves vs Valladolid | 3.04 | 3.14 | 2.34 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SINGIDA BIG STARS KUENDELEA KUTESTI MAJEMBE MAPINDUZI

**Na Saada Akida, Zanzibar**

KOCHA Msaidizi wa Singida Big Stars, Mathias Lule, amesema wataendelea kutumia wachezaji wapya katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa ajili ya kutengeneza muunganiko na wachezaji waliokuwapo mwanzoni mwa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Singida Big Stars imeanza vizuri kampeni yao michuano ya Kombe la Mapinduzi kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMKM, mchezo uliopigwa juzi usiku Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Mabao ya Singida Big Stars yalifungwa na Bruno Gomes dakika ya 19 na 33 kupitia nyota wake mpya waliomsajili kipindi cha dirisha dogo akitokea Geita Gold FC, Yussuph Kagoma.

Wachszaji wapya wa Singida waliochezeshwa juzi ni Yussuph Kagoma, Dickson Kibabage, Marcos Da Silva na Fancy Kazadi.

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya mchezo huo, Lule alisema wanafurahi kuanza vizuri na kufikia malengo yao ya kupata ushindi katika michuano hiyo ambayo wanaitumia kwa ajili ya kutengeneza muunganiko mzuri kwa wachezaji wapya waliowasajili katika dirisha dogo.

Aidha, alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri katika mchezo huo licha ya kipindi cha pili wapinzani wao KMKM kuwapa ushindani mkubwa kwa kufika eneo lao la hatari.

"Tumecheza vizuri na hii michuano imetusaidia kwa muda huu Ligi Kuu ikiwa imesimama, tumepata mwanga wa kuona madhaifu ya kikosi chetu na kutengeneza muunganiko mzuri kwa wachezaji wapya. Kuhusu malengo ya mashindano tumekuja kushinda na si kushiriki," alisema Lule.

Alisema baada ya kupata ushindi huo sasa wanaendelea na maandalizi ya mechi yao ijayo dhidi ya Yanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo unaotarajiwa kuwa na ushindani mkubwa.

Singida Big Stars itashuka tena dimbani keshokutwa, Alhamisi dhidi ya Yanga katika mchezo utakaopigwa Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

# ROBERTINHO AITAKA SIMBA FAINALI CAF

INATOKA UK. 32

Mabingwa Afrika hatua ya makundi, TP Mazembe kwa mikwaju 4-2 ya penalti Oktoba 15 mwaka jana, baada ya suluhu kwenye mechi zote mbili.

"Nikiwa mapumzikoni Brazil baada ya kuondoka Vipers, nilipokea maombi mengi ya timu wakitaka kufanya kazi na mimi, siku zote klabu kubwa zinazotaka mafanikio zinatafuta makocha wazuri.

"Nilikuwa mchezaji kabla ya kuwa kocha, huwa naamini kwenye mifumo na mbinu sahihi, kama una mpango mzuri unaweza kufika nusu fainali, fainali, ikiwezekana hata kutwaa Ligi ya Mabingwa Afrika kwa nini isiwezekane wakati nipo hapa Simba?" Alihoji kocha huyo raia wa Brazil na kuongeza;

"Hata tulipokuwa tunataka kucheza dhidi ya TP Mazembe wengi walitubeza, wakasema haiwezekani tunakwenda kutolea, lakini nilikuwa na mipango sahihi kama kocha na nikaweza kuiondosha. Nimekuja kubadilisha historia ya klabu hii kama nilivyofanya kwenye klabu zilizopita."

Kabla ya kumkaribisha kocha huyo, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, alisema kocha huyo anafahamu pia soka la Tanzania kwa sababu akiwa na Rayon Sport ya Rwanda na kisha Vipers aliwahi kuja nchini na kucheza na watani zao wa jadi, Yanga na mechi zote timu yake ilipata ushindi.

"Nipo hapa kumtambulisha kocha atakayeungana na benchi letu la ufundi kwa ajili ya michuano ya kimataifa na ya ndani, alikuwa anafundisha Vipers ya Uganda, yapo mambo mengi yaliyotushawishi, ana uzoefu mkubwa kwenye michuano ya Afrika, si mgeni kwenye eneo la Afrika Mashariki, ameishi Kenya, ameishi Uganda na Rwanda na amefanya mengi makubwa na moja ni kuipeleka Vipers hatua ya makundi, ile timu tangu ianzishwe ilikuwa haijawahi kufika na alishawahi kuifikisha Rayon Sports kwenye hatua kama hizo pia huko nyuma," alisema Mangungu.

Kocha huyo pia alikuja nchini na timu yake ya Vipers ilipoalikwa na Yanga kwenye tamasha la Siku ya Mwananchi na wageni wakashinda mabao 2-0.

Hata hivyo, Robertinho anayesifika kwa soka la kasi na kushambulia, alizaliwa Juni 22, 1960 jijini Rio de Janeiro nchini Brazil na ni kocha mwenye Leseni A.

Kwenye karia yake ya soka, amechezea klabu mbalimbali maarufu nchini Brazil kama Fluminense, Flamengo, Palmeiras, Madureiras RJ, kuanzia mwaka 1978 hadi alipomaliza soka lake mwaka 1996.

Kwenye kazi ya ukocha alianza kufundisha klabu mbalimbali nchini Brazil ikiwamo aliyoichezea, Fluminense, Rio Blanco, SV Grobenbach, Pelotas RS kuanzia mwaka 1997 hadi 2008 ambapo aliondoka nchini Brazil na kufundisha soka Afrika kwa mara ya kwanza kwenye Klabu ya Stade Tunisien, baadaye Kazma FC Club ya Kuwait, Al Shamal ya Qatar, Es Hammam ya Tunisia, Stade Gabesien, Grombalia Sports zote za Tunisia, mpaka 2016 alipokwenda kuifundisha AS Aviacao ya Angola, hadi 2020 alipotimkia, Rayon Sports ya Rwanda.

Mwaka mmoja baadaye akaenda Gor Mahia ya Kenya, kabla ya mwaka jana kutua Vipers na kufanya mambo makubwa.

# YANGA YAMPA KAZI

INATOKA UK. 32

mazuri katika mchezo dhidi ya Yanga.

Alisema anafahamu ubora wa Yanga, hivyo wataingia katika mchezo huo kwa mbinu tofauti na ile waliyoingia nayo dhidi ya Singida Big Stars.

"Tumejiandaa vizuri, tumefanyia kazi mapungufu yetu na ubora wa Yanga, kuhakikisha mechi hii hatufanyi makosa yaliyojitokeza mchezo wa kwanza na kupoteza, sasa tunaenda kuonyesha ushindani mkubwa na kutafuta matokeo dhidi ya Yanga," alisema Morocco.

Michezo
Jumatano Januari 4, 2023
Nipashe



UKURASA 29

**Ten Hag: Sitanunua straika mpya United**



KWAHERI PELE...

Mtoto wa nguli wa soka duniani, Edinho, akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa baba yake, Pele, kabla ya maziko kufanyika nchini Brazil jana. **PICHA: MTANDAO**

# ROBERTINHO AITAKA SIMBA FAINALI CAF

## ●●●Atoa sababu ya malengo hayo makubwa huku akianika mikakati yake mizito kuwa...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imemtangaza Robertinho Oliveira kuwa kocha wao mkuu mpya ikiwa ni siku chache tu baada ya kuvunja mkataba na klabu aliyokuwa akiifundisha ya Vipers FC ya Uganda, huku akiahidi kutaka kuifikisha timu hiyo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha huyo anachukua jukumu la kukinoa kikosi cha Simba baada ya kuondoka kwa Kocha Mkuu, Zoran Maki, na kwa kipindi chote kikosi hicho kilikuwa chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mgunda, ambaye alikiongoza kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini mpaka sasa inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba imeonekana kuvutiwa zaidi na kocha huyo baada ya kukiongoza kikosi cha Vipers FC kuisukumiza nje ya Ligi ya

INAENDELEA UK. 31




Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally (kulia), akimtambulisha Kocha Mkuu mpya wa klabu hiyo, Mbrazil Robertinho Oliveira, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yampa kazi Mziza kwa KMKM

**Na Saada Akida, Zanzibar**

YANGA inashuka Dimba la Amaan mjini Zanzibar majira ya saa 2:15 leo usiku kuivaa KMKM katika mechi yao ya kwanza ya Kombe la Mapinduzi msimu huu ikiwa bila mastaa wake wa kikosi cha kwanza.

KMKM wataivaa Yanga wakiwa na kumbukumbu mbaya ya kupoteza mechi ya kwanza kwa mabao 2-0 dhidi ya Singida Big Stars, hivyo watahitaji ushindi ili kuweka matumaini yao hai ya kutinga hatua inayofuata katika michuano hiyo.

Hata hivyo, Yanga itawakosa baadhi ya nyota wao wa kikosi cha kwanza akiwamo kinara wa kufumania nyavu Ligi Kuu Bara, Fiston Mayele, Stephane Aziz Ki, Yannick Bangala, huku wakitarajiwa kuonekana uwanjani Yacouba Songne na Lazarous Kambole.

Kwa upande wa KMKM itaongozwa na beki wa zamani wa Yanga, Haji Mwinyi, ambaye atakuwa na kazi ya kuhakikisha wanafanikiwa kuizuia safu ya ushambuliaji ya Yanga chini ya mshambuliaji kinda, Clement Mziza.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema timu yake inaundwa na mchanganyiko wa wachezaji kutoka kikosi cha kwanza ambao walikuwa wakianzia benchi pamoja na wa kikosi cha vijana.

Alisema wamejiandaa vizuri na wapo tayari kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya KMKM ambao amewaona juzi walivyocheza na Singida Big Stars.

“Mechi haitakuwa rahisi, utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwa sababu KMKM ina wachezaji wazuri na nimewaona ubora na udhaifu wao, hivyo nimeyafanyia kazi mazoezini kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika mchezo wetu wa kesho (leo),” alisema Kaze.

Kocha Mkuu wa KMKM, Hemed Morocco, alisema wamefanyia kazi madhaifu yao baada ya kupoteza mechi ya kwanza na sasa wako tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >